NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Hamsini na Sita –Tarehe 22 Juni, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaanza Kikao chetu cha 56. Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 470

**Daraja la Kigamboni**

**MHE. ZAINAB M. AMIRI** aliuliza:-

Daraja la Kigamboni ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na mawasiliano.

(a) Je, tangu daraja lianze kutumika Serikali imekusanya kiasi gani cha fedha kinachotokana na malipo kwa wanaovuka na vyombo vya moto?

(b) Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kutumia kadi maalum *(smart card)* kulipia kwa mwezi malipo kwa wanaovuka darajani hapo kwa vyombo vya moto?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ambao ndiyo wanasimamia uendeshaji wa daraja hilo hadi kufikia mwezi Machi, 2018 limeshakusanya kiasi cha Sh.19,734,655,482.70 tangu daraja hilo lilipoanza kutumika rasmi mwezi Mei, 2016. Aidha, katika mapato hayo, shilingi bilioni 15.2 ni makusanyo ya waliovuka na vyombo vya moto na shilingi bilioni 4.7 ni faida na pato la ziada la mtaji lililotokana na upatikanaji wa fedha hizo katika dhamana ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii lipo katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi wa kuweka mfumo utakaotumia kadi maalum *(smart card)* kwa malipo ya wanaovuka darajani hapo. Mvukaji atakuwa na hiari yake ya kulipia kwa siku, wiki au mwezi kulingana na uwezo wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zainab.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika madaraja yaliyopo nchini kwetu Tanzania yote huvuka bure isipokuwa daraja la Kigamboni na *NSSF* ilikusudia daraja hilo kutumika bure mara baada ya marejesho. Je, ni lini Serikali sasa itasitisha tozo la kupita daraja la Kigamboni ili liweze kutumika kama yalivyo madaraja mengine ya Mkapa, Kilombero, Ruvu, Wami na mengineyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kuna adha kubwa ya usafiri kwa wananchi wa Kigamboni hususan mabasi ya daladala na daladala ili ivuke inalipa Sh.7,000 ikivuka mara 10 ni Sh.70,000. Kwa hiyo, wamiliki wa daladala

huona hakuna haja ya kupeleka *route* ya Kigamboni, Machinga *Complex* na wananchi wanapata adha sana ya Usafiri. Je, Serikali haioni haja sasa kutafuta vyanzo vingine ili kuweza kulipa deni la *NSSF* watu wapite bure kuliko kufanya biashara maana imekaa kibiashara zaidi kuliko huduma?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA :** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niyajibu maswali yake kwa pamoja. Nikianza na swali la kwanza la kuhusiana na uwekezaji uliofanyika hapo, naomba tu ieleweke kwamba daraja hili ni sehemu pia ya uwekezaji wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii na fedha iliyotumika kwa ajili ya uwekezaji huo ni fedha ya wanachama ambao mwishoni pia ndiyo fedha hii hii huwa inatumika kwa ajili ya kwenda kulipia mafao kwa sababu ni sehemu ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kukisema tu ni kwamba, Shirika linategemea sana daraja hilo kwa ajili ya kupata kipato na hatuwezi katika hali ya kawaida kufuta kabisa tozo na watu wakapita bure katika eneo hilo kwa sababu ni eneo la *investment.* Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba huu ni uwekezaji ambao unafanywa na shirika na hii ni michango ya wanachama ambayo baadaye inarudi pia kwa ajili ya kulipia katika mafao mbalimbali.

Mheshimiwa wenyekiti, ukienda duniani kote utaratibu ndiyo uko hivi kwa sababu hii fedha ya uwekezaji, fedha lazima ipatikane kuja kulipia katika shughuli mbalimbali za shirika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwilima

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Kigamboni shida waliyokuwa

wanaipata kabla ya kujengwa daraja lile la Nyerere ilikuwa ni kubwa sana. Pia wananchi wangu wa Kata ya Ilagala na kata zingine za Ukanda wa *Lake* Tanganyika wanapata shida kubwa sana kwa Kivuko kilichopo pale, kila siku ajali za magari yanaingia kwenye Mto Malagarasi. Je, kwa nini Serikali sasa isiwajengee Daraja la Ilagala na wanajua kabisa waliahidi kujenga daraja hili tangu 2008?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwona Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali inaendelea kuboresha mawasiliano ya usafiri katika maeneo ya Mheshimiwa Mbunge ambayo anatoka na natambua kwamba uko usanifu wa kuunganisha barabara kupita kwenye daraja ambalo analizungumza kwa hiyo Mheshimiwa Mwilima nafikiri baadaye tunaweza tukazungumza ili aone mpango mahususi tuliokuwa nao kuhakikisha daraja hili linaweza kutengenezwa ili tuweze kuunganisha maeneo haya na maeneo mengine ya Kanyani kule tukiwa tuaelekea kule Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tulizungumze ili aone namna tulivyojipanga kwa ajili ya kutoa hii adha na najua na suala la kivuko kulikuwa na shida pia ya kuvuka usiku katika eneo hili, yote haya tunayashughulikia ili wananchi hawa wasipate adha ambayo ilikuwepo katika eneo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini kwa niaba.

**MHE. MICHAEL J. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Alfred Lwakatare, naomba swali lake namba 471 lipate majibu ya Serikali.

Na. 471

**Matokeo ya Kukua kwa Elimu ya Uraia na Siasa**

**MHE. MICHAEL J. MKUNDI - (K.n.y MHE. WILFRED M. LWAKATARE)** aliuliza:-

Kukua kwa elimu ya uraia na ufahamu wa mambo ya kisiasa kumefanya wananchi wengi kuupokea mfumo wa vyama vingi na kuchagua wawakilishi wengi wa Vyama vya Upinzani kuongoza Kamati za Maendeleo za Kata, Halmashauri za Miji, Miji Midogo, Wilaya, Manispaa, Majiji na Majimbo ya Ubunge na Udiwani:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza kanuni, utaratibu na mfumo wa kutoa elimu na maelekezo kwa watendaji na viongozi wa Kiserikali kuyakubali na kupata ufahamu wa mabadiliko ya kisiasa yanayokua kwa kasi ili kuepusha migogoro na migongano ya usimamizi wa kazi baina ya watendaji wa Serikali na wawakilishi wa wananchi?

(b) Je, kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuwa na uchaguzi huru na haki kama vile Tume Huru ya Uchaguzi na chombo huru cha kusimamia chaguzi za vitongoji, vijiji na mitaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kwanza uniruhusu nimsahihishe kidogo Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali kwa niaba, huyu Mheshimiwa haitwi Alfred Lwakatare anaitwa Wilfred Lwakatare. Naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji na viongozi wa Serikali wanafanya kazi kwa mujibu wa Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo iliyopo. Ni wajibu wa viongozi

na watumishi wote katika ngazi zote za Serikali kuzifahamu nyenzo hizo za kazi ili kuepusha migogoro na migongano baina yao. Serikali imekuwa ikiwaongezea uwezo wa kiutendaji na uongozi watendaji na viongozi wao kupitia mafunzo ya mara kwa mara na vikao vya kazi ili wawahudumie wananchi vizuri na kwa tija zaidi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya na Mamlaka za Miji, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa husimamia uchaguzi wa vitongoji, vijiji na mitaa ambao hufanyika ukiwa huru na haki kila baada ya miaka mitano kwa kushirikisha wadau wote wakiwemo viongozi wa vyama vya siasa ambao hutoa maoni yao kunzia kwenye maandalizi ya uchaguzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. MICHAEL J. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali bado kuna matatizo makubwa sana kwenye utendaji katika ngazi hizi za chini zinazotokana na ama na kutokuelewa wajibu wa kila upande katika kusimamia utendaji kwenye maeneo haya. Je, bado Serikali haioni sababu ya msingi kabisa kutoa elimu pamoja na majibu haya yaliyotolewa bado kuna tatizo kubwa sana kwenye usimamizi hasa nyakati za uchaguzi ambapo kumekuwa na migogoro mingi inayotokana na watendaji wanaosimamia chaguzi hizi kufanya au kutoa maamuzi kulingana na maelekezo yanayokuwa yametolewa na viongozi wa juu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kutokana na migogoro hii, Serikali haioni kwamba kuna sababu ya msingi kabisa kutokana na mapendekezo ya Katiba iliyopendekezwa kuwepo na umuhimu wa kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi ili kuondoa kabisa migogoro hii inayotokea nyakati za uchaguzi kwenye ngazi mbalimbali?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie kwanza uzoefu wangu kwamba kati ya mwaka 1996 mpaka mwaka 2000 mwenyewe nilikuwa Ofisa Mtendaji wa Kata, kwa hiyo nina uzoefu mkubwa na kile ninachokielezea na kata yenyewe ilikuwa ni Kata ya Manzese pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chaguzi za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa sheria na kama atatokea Msimamizi Msaidizi yeyote akatenda kinyume cha sheria, mdau yeyote anao uhuru wa kulalamika katika vyombo vinavyohusika ikiwemo kulalamika kwa Msimamizi wa Uchaguzi na hatua zimekuwa zikichukuliwa dhidi ya watu ambao wanatenda kinyume cha utaratibu wa sheria ya uchaguzi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, ameuliza kwamba kuna mapendekezo kwenye Katiba iliyopendekezwa. Sasa kwa sababu Katiba iliyopendekezwa bado hatua zake hazijakamilika, nashauri Bunge lako Tukufu kwamba tusiwahishe mambo, tusubiri kwanza huo mjadala wa Katiba Mpya Iliyopendekezwa ukamilike na mambo yaingizwe kwenye sheria basi hapo tutatekeleza baada ya sheria kuwa imekamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. ZITTO R. Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Serikali za Mitaa ni pamoja na sheria zinazohusiana na mabadiliko ya Sheria Ndogo za Tozo na Ushuru mbalimbali. Mpaka hapo tunapozungumza, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji haikusanyi ushuru, watendaji wamegoma kwa sababu ya amri ya Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi. Mara ya mwisho nilivyouliza Waziri alisema hana taarifa na nina uhakika sasa ana taarifa. Anatuambia nini kuhusiana na kutotekelezwa kwa sheria ambayo imetungwa na Baraza la Madiwani na imepitishwa na Waziri mwenye dhamana ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hoja ambayo ameileza Bunge lako tukufu kwa sasa naielewa vizuri sana baada ya kuwa ameigusia wiki iliyopita. Niseme tu kwamba Baraza la Madiwani la Manispaa ya Kigoma ambalo linaongozwa na *ACT* lilipandisha ushuru kutoka Sh.15,000 mpaka Sh.50,000 kama tozo kwa wafanyabiashara na hizo ni tozo halali ambazo zinatakiwa kukusanywa na sisi tulimuagiza Mkuu wa Wilaya asimamie tozo hizo ziendelee kukusanywa kama zilivyopitishwa na Baraza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi wa Kigoma wamekuwa wakilalamika na malalamiko yao mengine wameyapeleka kwa viongozi mbalimbali wakiwemo viongozi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumetuma timu ya watalaam kwenda Kigoma kuangalia kinachoendelea na taarifa yao hawajatuletea. Kwa hiyo, naamini wakituletea taarifa yao Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe tutampa majibu sahihi zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto linaulizwa na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 472

### Ujenzi wa Jengo la Ghorofa Tatu Hospitali ya Mkoa wa Mwanza

**MHE.KITETO Z. KOSHUMA** aliuliza:-

Katika vikao vya Ushauri vya Mkoa wa Mwanza *(RCC)*, moja ya kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni ujenzi wa jengo la ghorofa tatu katika Hospitali ya Mkoa linalohitaji shilingi bilioni nne na laki mbili (4.2 bilioni):-

Je, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kinachohitajika katika mwaka huu wa fedha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Mwanza kwa jitihada zake za kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa kuanzisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu katika hospitali ya rufaa ya Mkoa Sekou Toure ikiwa ni jengo mahususi kwa ajili ya kutoa huduma ya Mama na Mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni mbili na hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni moja kimeshatolewa na kulipwa kwa Wakala wa Majengo Tanzania kwa maana ya *TBA* ambaye ndiye msimamizi Mkuu wa jengo hili. Vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia tamko la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kuagiza hospitali za Mkoa kuwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto, Wizara imetenga kiasi cha shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika hospitali za rufaa za mikoa ikiwa ni pamoja na hospitali ya Mkoa wa Sekou Toure.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekiri kuwa ilitenga shilingi bilioni mbili kwa mwaka 2017/2018, lakini ikapeleka kiasi cha fedha shilingi bilioni moja. Mkoa umejiwekea malengo ya kumaliza jengo hili ifikapo mwaka 2020 lakini Serikali inapeleka fedha kidogo kidogo. Pia kwa mwaka 2018/2019 Serikali tumeona tena imetenga kiasi cha fedha shilingi bilioni mbili, uzoefu umekuwa ukionesha kwamba fedha zinapelekwa kidogo kidogo na hivyo kukwamisha ukamilishaji wa majengo mengi ambayo yanakuwa yanajengwa katika hospitali zetu za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, je, Serikali ina mpango gani mkakati wa kuhakikisha kuwa fedha hizi ambazo zimetengwa kwa mwaka 2018/2019 zinapelekwa zote lakini pia fedha ambazo zilitengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, bilioni moja iliyobaki na yenyewe pia inapelekwa na kumalizia fedha zingine ili jengo hili liweze kwisha na kuondoa msongamano uliopo pale katika hospitali ya Sekou Toure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, uzoefu unaoyesha kwamba majengo mengi yanajengwa lakini yanapokamilika, vifaa haviendi kwa wakati, watumishi hawapelekwi kwa wakati. Je, Serikali imejiwekea mpango gani mkakati kuhakikisha kwaba jengo hili litakapokamilika ifikapo 2020 basi watumishi wanapekwa, vifaa vinapelekwa ili kuweza kuokoa maisha ya mama na mtoto.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi Serikali imetenga jumla ya bilioni 30 ambazo katika hizo bilioni 30 kiasi cha bilioni 10 zinaenda kutumika kuhakikisha kwamba tunafanya ukarabati na pia bilioni 20 zinaenda kutumika kwa ajili ya kujenga hospitali za rufaa katika Mikoa ya Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ni azma ya Serikali kuhakikisha maeneo yote yale ambayo kuna msongamano kama ilivyo hospitali ya Sekou Toure ambayo nina hakika Serikali imeanza kutoa pesa na yeye mwenyewe amekiri bilioni moja imeshatoka. Nimhakikishie kwa kadri pesa itakavyokuwa imepatikana hiyo bilioni nyingine itatoka ili ziweze kumalizia kazi iliyokusudiwa, kwa sababu lazima tuhakikishe kwamba inakamilika kwa muda tuliojipangia 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anaulizia juu ya suala zima la kupatikana vifaa pamoja na watalaam wa kuweza kutoa huduma kama ambavyo tumetarajia. Naomba nimhakikishie yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge ni shuhuda kwamba sasa hivi Serikali imetangaza nafasi kwa ajili ya kuajiri watumishi kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lakini pia kupitia Wizara ya Afya. Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba watumishi wanapatikana, hilo naomba nimwondoe shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala zima la vifaa tumekuwa tukipeleka pesa moja kwa moja *MSD* ili pale ambapo hospitalii zinakamilika na vituo vya afya vinakamilika vifaa navyo vinapelekwa mara moja.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ukweli ni kwamba hospitali hii ya rufaa sio tu inahudumia wananchi wa Mkoa wa Mwanza, bali na wananchi wengi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu ya umuhimu huo, hospitali ya Sekou Toure ambayo kwa kweli inatoa huduma kubwa na nzuri kwa sasa, ni nini, mkakati wa Serikali kuwatumia hao hao Wakala wa Majengo *(TBA)* wakati wanaendelea na mikataba ikiwezekana kwa sababu wao ni Wakala wa Serikali, wawe wanatumia fedha zao za ndani

kuhakikisha miradi waliyopewa inakamilika na wao wanabaki kudaiana na Serikali ili kutoa huduma kwa wananchi kwa haraka?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa niaba ya Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBA* pesa ambazo wanazipata zinatokana na *project* mbalimbali, sasa nadhani sio busara sana ukasema watumie pesa walizonazo ambazo zitakuwa zimetokana na *project* fulani ambayo labda haijajengwa, waanze kutumia wakisubiri kwamba Serikali ikipeleka pesa ndio ziende sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kadri makusanyo yanavyokwenda na yeye mwenyewe ni shuhuda, kasi yetu katika ujenzi wa vituo vya afya na hospitali za Wilaya pamoja na hospitali za rufaa hautiliwi mashaka. Naomba avute subira haya mambo yatakwenda vizuri kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kusuasua kwa ujenzi wa hospitali ya rufaa Mkoa wa Mwanza, kunafanana na kusuasua kwa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini ambayo inajengwa Manispaa ya Mtwara. Sasa ningependa kujua Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo ya rufaa Kanda ya Kusini ili ianze kutumika haraka iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Jibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la swali la msingi kuna kiasi cha shilingi bilioni 10 ambazo zimetengwa mahususi kwa ajili ya kwenda kufanya ukarabati na kumalizia majengo ambayo tayari yalishaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie na hasa baada ya kutenganisha kwamba hospitali za rufaa zinakuwa chini ya Wizara ya Afya, kasi itaongezeka tofauti na ambavyo mwanzo zote zilikuwa chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuondoa huu mzigo naamini ni rahisi sana kwa Wizara ya Afya, kusimamia na kuhakikisha kwamba hiyo hospitali ambayo ilishaanza kujengwa inakamilika kwa wakati.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 473

**Ujenzi wa Nyumba za Askari Polisi Kata ya Loya**

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI** aliuliza:-

Wananchi Halmashauri ya Wilaya ya Tabora kwa kushirikiana na Mbunge wamejenga kituo kikubwa cha Polisi katika Kata ya Loya kilichogharimu zaidi ya Sh.100,000,000/= lakini mpaka sasa hakijaanza kufanya kazi:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kutenga bajeti kusaidia ujenzi wa nyumba za askari na kurekebisha upungufu mbalimbali uliopo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutoa gari jipya ili kusaidia kurahisisha kazi ya Ulinzi na Usalama katika eneo hilo kwani kituo hicho kipo kilomita 120 kutoka Makao Makuu ya Wilaya – Isikizya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itatenga fedha kwa ajili ya kumaliza Kituo cha Polisi cha Kata ya Loya ambapo nyumba, chumba cha kuhifadhi Mahabusu na chumba cha kuhifadhi silaha vitaimarishwa ili kituo hicho kianze kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, napenda kutoa pongezi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Wananchi pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwa kufanikisha ujenzi wa kituo hicho cha Polisi katika Kata ya Loya.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Uyui ambayo Makao Makuu yake yapo Kata ya Isikizya ina magari matatu na moja ni bovu ambalo linahitaji matengenezo. Serikali inaendelea na mchakato wa kutafuta magari kwa ajili ya Jeshi la Polisi na pindi yatakapopatikana yatagawiwa katika maeneo mbalimbali yenye mahitaji nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mussa Ntimizi

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pia nashukuru majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama alivyosema na kutupongeza wananchi, Mkurugenzi na mimi kwa nia nzuri ambayo tumeionesha ya kushirikiana na Jeshi la Polisi katika uhakikisha kero za ujambazi na usalama wa wananchi wetu zinatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki kimekamilika takribani miaka mitatu sasa na hayo marekebisho ambayo

Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema kama Mbunge nilikwishatoa fedha kwa maana mifuko ya simenti na nondo kurekebisha ile Amari ili kituo hiki kiweze kuanza kazi, takribani mwaka mmoja uliopita. Je, ananihakikishia vipi Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kituo hichi sasa kitaenda kufunguliwa haraka kutokana na mahitaji yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini (b) Wilaya yetu ya Uyui ni Wilaya kubwa katika Mkoa wa Tabora ina majimbo mawili ya Igalula, Tabora Kaskazini lakini katika majibu yake amesema tuna magari matatu ambayo kwa kweli hayakidhi haja ya mahitaji ya Wilaya yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kutuletea magari pamoja na mgao mkubwa wa mafuta ili kuweza kutoa huduma zilizo bora katika Wilaya yetu? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ntimizi nashauri uwe unaendelea kuvaa namna hiyo kila siku, umekaa vizuri sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihadi zake ambazo amekuwa akizifanya katika kuhakikisha kwamba kituo hiki kinakamilika haraka. Ni sahihi kabisa Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo nimesema awali kwamba, amechangia katika kukamilika ujenzi wa Kituo cha Loya, ni jambo jema. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi kwamba, si dhamira ya Serikali kuona jitihada zake na wananchi ambao wametumia nguvu zao kujenga kituo hiki ziende bure bure kwa kuchelewesha kukitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi ni kwamba, tatizo lililopo ni kwamba tunahitaji kukamilisha *Lockup* pamoja na amari ili ziwe katika hali nzuri kabla ya matumizi. Jambo hilo tunatarajia kulikamilisha katika muda mfupi sana ujao. Nitahakikisha

kwamba nitakapotoka hapa nitafuatilia ili katika kipindi cha mwezi mmoja tuweze kukamilisha vitu hivyo viwili na kituo hiki kianze kutumika mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na magari, ni sahihi kwamba katika Wilaya ambazo zina changamoto za magari mojawapo ni Wilaya ya Uyui katika Mkoa wa Tabora. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ikiwemo Wilaya ya Uyui hasa kulingana na ukubwa wa kijiografia wa Wilaya ile yanapata magari ya kutosha zaidi ya yale magari matatu ambayo nimeyazungumza katika jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tunaweza kusema kwamba sasa hivi kinatukwaza au kinatukwamisha kutekeleza hilo ni kwamba bado mgao huo haujafanyika kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zinakabili programu zima ya uletaji wa magari yaliyodhamiriwa kuletwa katika Serikali. Changamoto hizo zitakapopata ufumbuzi na magari hayo yatakapokuwa tayari kugawiwa, basi nina uhakika basi Mkoa wa Tabora ikiwemo Wilaya ya Uyui na Wilaya nyingine kama Nzega haina gari hata moja zitapewa kipaumbele.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Magige Catherine, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Arusha ni Mkoa ambao una shughuli nyingi sana haswa za kipolisi, zikiwemo na ku-*escort* viongozi mbalimbali, lakini inasikitisha sana Mkoa wa Arusha *RPC* wetu hana gari la polisi kutokana na gari lake lilipata ajali muda mrefu. Je, Serikali haioni ni muhimu kulichukulia jambo hili kama la dharura na kumpelekea *RPC* wetu wa Mkoa wa Arusha gari?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa *RPC* kuwa na gari. Nataka tu nimthibitishie kwamba kama gari la *RPC* limepata ajali basi tutaangalia uwezekano wa kulifanyia ukarabati gari hilo, likishindikana basi *RPC* wa Tabora tutampatia gari nyingine.

**MWENYEKITI:** Arusha!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Samahani ni *RPC* wa Arusha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ukizunguka Tanzania nzima kwenye vituo vya polisi vyote utakuta magari mengi sana mabovu ambayo ni ya polisi wenyewe kwa maana ya kwamba ni ya Serikali hayajatengenezwa na hayafai tena kutengenezwa yanavyoonekana mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ukija Jimbo la Ndanda, Kituo cha Polisi cha Ndanda ambacho kinahudumia jimbo zima na tuna kituo kimoja tu cha polisi hivi karibuni tuliletewa gari ambalo nalo linaonekana ni bovu kwa sababu toka limefika halijawahi kutumika. Sasa nataka Waziri atuambie ni lini mahususi kabisa wataamua kutengeneza gari la Kituo cha Polisi cha Ndanda kwa ajili ya kuweza kutoa huduma maeneo ya Jimbo la Ndanda ambayo yanasaidia pia na Jimbo la Ruangwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumze kwa ujumla kwamba, tunakiri juu ya uwepo wa baadhi ya magari chakavu katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge

wengine wote waliopo humu ndani na wananchi kwa ujumla kwamba tuna jitihada mbalimbali zinafanyika. Nyingine zinafanyika katika mikoa lakini nyingine zinafanyika katika ngazi ya Kitaifa kuhakikisha kwamba magari haya yanakuwa katika hali nzuri. Magari mengi tu ambayo yapo katika maeneo mbalimbali nchini tumeanza kuyafufua yanatumika, yale ambayo yanawezekana kufufulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la gari hii ya Ndanda *specifically* kwanza nataka nilichukue hili suala kwa sababu ni jambo ambalo haliingii akilini kwamba gari inapelekwa katika kituo na wakati huo gari haijaanza kutumika inakuwa mbovu. Kwa hiyo, nijue kwanza gari hii ilitoka wapi na kwa nini iwe haitumiki? Halafu tuangalie sasa baada ya hapo nini kifanyike ili kuweza kurekebisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHANCE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vituo vya polisi vya Nyamuswa, Mgeta vimejengwa miaka ya 60, majengo yake sasa hivi ni hatarishi na wananchi wako tayari kusaidiana na Serikali kujenga vituo vile kwa kutoa nguvu kazi ya tofali, maji, kokoto na mawe. Je, Serikali iko tayari kushirikiana na wananchi kujenga vituo hivyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kifupi mko tayari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Getere kwa jitihada zake za kuhamasisha wananchi kuweza kupata vifaa ambavyo amevizungumza kwa ajili ya ujenzi wa vituo. Nataka nimhakikishie kwamba, Serikali itahakikisha kwamba tunaunga mkono jitihada hizo ili kuweza kufanikisha malengo ambayo wameyakusudia.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Hali ya vituo vya Polisi vya Kata pale Temeke ni mbaya sana, mapaa yameoza kabisa na Polisi muda mwingi wanafanya kazi chini ya miti badala ya kukaa kwenye ofisi kwa sababu hazikaliki. Hata hivyo, hata zile ofisi chache ambazo tumezijenga kwa nguvu za wananchi kama pale Makangalawe na Buza ambazo tumeshindwa kumalizia vyumba vya mahabusu na vya kutunzia silaha Serikali nayo imeshindwa kuvimalizia ili viweze kufanya kazi masaa 24. Sasa labda kwa sababu Mawaziri hawafahamu hali halisi iliyopo huko kwenye vituo hivyo ndio maana kila siku wamekuwa wakisema wanasubiri bajeti.

**MWENYEKITI:** Uliza swali sasa Mheshimiwa.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa kadri watakavyoweza kujipanga ni lini watakuwa tayari kuja kufanya ziara Temeke ili wakajionee hali halisi ya vituo hivi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ni lini utaenda kuona hali yenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si sahihi kwamba hatufahamu au hatujafika. Binafsi nimeshafanya ziara katika Jimbo lake na Wilaya yake na nimeshiriki katika ujenzi wa kituo pale nimesahau jina la kile kituo, lakini ni maeneo ya Mbagala. Hali kadhalika nikashiriki katika uzinduzi wa kituo kingine cha Polisi nikizindua maeneo ya kule Wilaya hiyo ya Temeke lakini Jimbo la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwamba hali ya vituo vya Polisi vya Temeke tunaifahamu vizuri, kwa sababu *physically* nimekwenda na nimeshuhudia na tumeshiriki na wananchi kuweza kufanya kazi ya kuvijenga na kuvikarabati vituo vingine ambavyo ni vichakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ningemwomba Mheshimiwa Mbunge atusaidie ni kwamba, naye aendelee kuunga jitihada zetu hizi mkono kwa sababu si rahisi kuweza kukabiliana na changamoto hizi za vituo kwa wakati mmoja. Ndio maana tunafanya kazi hizi kwa awamu na kuhamasisha wadau kama sio wananchi na Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo niliwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliopita hapa, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Ntimizi katika suala hili hili la msingi ambalo nimejibu, basi na Mheshimiwa Mtolea naye tunakukaribisha aweze kuhamasisha wananchi hata kama akiamua fedha yake ya Mfuko wa Jimbo aingize katika kukarabati vituo hivi, tutamshukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge tumechukua muda mrefu wa swali hili. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Hawa Bananga Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum na linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Katibu na Sheria.

Mheshimiwa Mwaifunga.

**WABUNGE FULANI:** Hilo jna la Bananga umelitoa wapi?

**MWENYEKITI:** Hawa Bananga imeandikwa hivyo.

Na. 474

**Tatizo la Ndoa za Utotoni**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Mkoa wa Tabora ni moja kati ya mikoa inayokabiliwa na tatizo kubwa la ndoa za utotoni na kusababisha watoto wengi wa kike kushindwa kumaliza elimu ya msingi au ya sekondari. Aidha, hivi karibuni Serikali ilikata rufaa juu ya ndoa za utotoni ikitaka iruhusiwe watoto wa kike kuolewa na umri kuanzia miaka 14 ambapo hii ni kinyume cha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia watoto wa kike wa Mkoa wa Tabora angalau wengi waweze kwenda kupata elimu ya msingi na sekondari kwa kupunguza ndoa za utotoni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa elimu kwa watoto wote wa kike na kiume wa Tanzania. Hii inadhihirishwa na uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kuifanya elimu ya msingi na ya sekondari kuwa ni elimu ya lazima na kutolewa bila malipo. Lengo la mpango huu ni kuhakikisha watoto wetu wote ikiwa ni pamoja na watoto wa kike wanaipata elimu hiyo bila kikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu ya mtoto wa kike Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Elimu ambayo inalinda haki za mtoto kusoma hadi sekondari. Kupitia marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Elimu na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya mwaka 2016, ni marufuku kwa mtu yeyote na katika mazingira yoyote kuoana na msichana au mvualana anayesoma shule ya msingi au sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni kosa kumpa mimba msichana anayesoma au sekondari na kwa yeyote anayesaidia msichana au mvulana anayesoma kuoa au kuolewa anakuwa ametenda kosa. Marekebisho haya yameweka adhabu kali kwa yeyote anayetenda makosa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kumlinda mtoto wa kike na ndoa za utotoni, licha ya Sheria ya Ndoa kuweka mazingira  na vigezo vya mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 15, Serikali imeendelea kuchukua hatua za

kuhakikisha mtoto huyu analindwa. Katika kulisimamia hilo, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo pamoja mambo mengine imeainisha haki za mtoto ikiwemo haki ya kupata elimu na kutoa wajibu wa haki hizo kulindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuzuia vitendo vya kuwaozesha watoto wa kike. Si tu kwa mkoa wa Tabora bali katika nchi yote ili kuwawezesha watoto wetu wa kike kupata elimu ya msingi na sekondari na pale ambapo vitendo hivyo vinajitokeza wananchi wana wajibu wa kutoa taarifa na kushirikiana na vyombo vya Serikali ili kuhakikisha wanaofanya makosa hayo wanachukuliwa hatua za kisheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Serikali imetoa majibu kwamba na wamekiri kwamba kweli sheria ya mtoto ya kuolewa kwa maiaka 15 ipo na inaendelea kuwepo na wanasema kwamba wanataka kumlinda mtoto huyu asiolewe akiwa na umri huo wakati sheria inasema kwamba anaweza kuolewa akiwa na umri huo. Mkoa wa Tabora ni moja kati ya mikoa ambayo ndoa nyingi za utotoni na watoto kujifungua watoto wenzao wakiwa na umri mdogo na kusababisha vifo vingi vya watoto. Serikali ina mpango gani wa kuibadilisha sheria hii ili watoto hawa waweze kuendelea na masomo yao kisheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, asilimia 63 ya wanaoathirika na ndoa za utotoni ni watoto wa kike, kesi nyingi zimekuwepo mahakamani kuhusiana na suala hili, lakini kutokana na sheria kuwepo ya watoto kuolewa na umri wa miaka 15 wanaofanya makosa hayo wamekuwa hawaadhibiwi kwa sababu sheria haisemi ni adhabu gani wanaweza wakapatiwa, Serikali inasemaje kuhusiana na suala hili ili kunusuru watoto wetu wanaolewa wakiwa na umri mdogo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) :** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la kwanza amezungumza kuhusu mkinzano na kuitaka Serikali kubadilisha sheria. Suala hili limekwishazungumzwa sana na Serikali mkishatoa maelezo yake na ikumbukwe kwamba yalitolewa maamuzi ya kesi Na.5 ya mwaka 2016 ambayo ni kesi kati ya Rebeka Jumi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali imekata rufaa, kwa hiyo tunasubiri maamuzi ya kesi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache anachokisema Mheshimiwa Mbunge kama mkinzano, mkinzano huu haupo kwa sababu suala la umri, umri wa mtoto unatafsiri katika sheria tofauti na katika maeneo tofauti. Kuna umri *biological*, kuna umri *contextual* na kuna umri *situational*.

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi tu Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) :** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tunasema hapa katika sheria zetu hizi sheria ambayo anahisi yeye inakinzana hakuna upinzani wowote, Kwa sababu mwanafunzi yoyote ambaye yuko shuleni ambaye akipata ujauzito pale Hatuangalii *biological age* yake tunaangalia umri wa muktadha, ndio maana tunasema hata kama akiwa yupo *form six* ana miaka 18 akipewa ujauzito sheria ambayo tulifanya wenyewe marekebisho hapa Bungeni ukienda kwenye Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 kifungu imeongezwa kifungu cha 60A imeweka adhabu ya kwamba mtu anayefanya akosa hilo adhabu yake ni miaka 30. Kwa hiyo hakuna mkinzano katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, Mheshimiwa Mbunge amezungumza kuhusu Serikali ifute sheria na

amesema kwa sababu ndio sehemu pekee ya kuweza kulinda haki ya mtoto wa kike hasa katika eneo ambalo ametokea yeye kutokana na kwamba kulikuwa na idadi kubwa sana ya watoto ambao wanapata ujauzito na akasema ni sheria gani ambayo inamchukulia hatua mtu huyu ambaye anafanya kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii imesema dhahiri kabisa ukienda kwenye Sheria Na. 21 ya mwaka 2009, sheria ambayo inalinda haki ya mtoto imezungumza juu ya kosa hilo la mtu yoyote ambaye anatenda kosa la kuzuia haki ya mtoto, baadaye sheria hiyo inaweza kuchukua mkondo na kuhakikisha kwamba mtu huyo anatiwa katika mikono ya sheria. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa kwamba si kweli kwamba Serikali hatu fahamu na hatulindi haki za mtoto na ndio maana tumechukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba tunalinda haki ya mtoto na watupe muda tuendelee kufanyia kazi suala hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Naibu wakati akijibu swali nilikuwa nataka nimuulize tu ikitokea mwanafunzi wa kiume akamchukua Mwalimu wa kike sheria inasemaje?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002, Sura ya 353 imezungumza katika kifungu cha 60A(2) kwamba ni kosa pia kwa mtoto wa kiume yeyote ambaye yuko shule kuoa. Kwa hiyo, kosa linabaki pale pale na kwa upande wa wanaume imezungumza kama ni kosa, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Ndassa bado inabaki pale pale mtoto wa kiume pia na yeye akioa akiwa bado yuko shuleni ni kosa pia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Watoto wakike wengi wanaoshindwa kuendelea na masomo baada ya kumaliza kidato cha nne na cha sita wanaolewa kwa kukosa fursa ya kujifunza katika vyuo vyetu vya ufundi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha kambi la vijana ili hawa watoto wanaomaliza kidato cha nne wakiwa wadogo na hawaruhusiwi wakiwa chini ya miaka 14 au wakiwa na miaka 14 wakajifunze shughuli za ufundi, ufugaji bora wakajifunze ujasiriamali na mambo mengine?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu kwa swali hilo, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) :** Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi ya Waziri Mkuu ina *program* ya ukuzaji ujuzi nchini ambao lengo lake kubwa ni kuhakikisha tunaisadia nguvu kazi yetu hasa vijana wengi kupata fursa ya kujifunza kwa vitendo hasa katika mafunzo mbalimbali ya ufundi. *Program* hii inaendelea na mpaka ninavyozungumza hivi sasa takribani vijana 22,000 nchi nzima wameshawasilisha maombi. Kwa hiyo, ni program ambayo inawagusa watu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni *program* endelevu mpaka mwaka 2021 tutaendelea kuwachukua watoto wengi hasa wa kike kuingia kwenye *program* hii kujifunza ili waweze kujitegemea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumuuliza Naibu Waziri suala dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna watu wazima ambao wana akili zao timamu na wana kazi zao, lakini wamekuwa

wakikiuka maadili na kuwachukua hawa mabinti wakiwa katika umri mdogo na sana kuwazalisha watoto na kuongeza ongezeko la watoto wa mitaani. Je, Serikali ina mikakati gani kuchukua sheria na mikakati ili kuhakikisha tunakomesha vitendo hivi na hawa watoto wa kike kupata haki zao stahiki?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) :** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria imeeleza vyema ni katika mazingira gani mtoto wa kike anaweza kuolewa na kinyume chake maana yake ni kosa linatengenezwa. Kwa hiyo, kwa wale wote ambao wanafanya vitendo hivyo vya kukiuka sheria, sheria zetu zipo, watachukuliwa hatua na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria ili haki ionekane imetendeka kwa mtoto huyu ambaye anakuwa amekatishwa shughuli mbalimbali ikiwemo masomo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linaofuata linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na linaulizwa na Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Chikambo.

Na. 475

**Kurudisha Kambi ya Jeshi Wilayani Tunduru**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Katika Wilayani Tunduru kulikuwa na Kambi ya Jeshi ambayo pamoja na mambo mengine ilishughulika na ulinzi katika Vijiji vya Wenje na Makande vilivyopo mpakani na Nchi ya Msumbiji:-

(a) Je, Serikali haloni haja ya kurudisha Kambi hiyo ya Jeshi Wilayani Tunduru?

(b) Kambi iliyokuwepo ilikuwa na hekta za ardhi zisizopungua 18,000, je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza maeneo hayo ambayo sasa yamekuwa vichaka?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Chikambo kama ifautavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ulinzi wananchi wa Tanzania liliweka kituo cha ulinzi cha Kombania ya sita ya 691 kikosi cha Jeshi (06/691 KJ) katika eneo la Chitanda, Wilayani Tunduru. Kutokana na sababu ambazo zilikuwa za msingi kwa wakati huo kituo hicho kilifungwa na eneo hilo likarudishwa rasmi kwa uongozi wa Serikali ya Wilaya ya Tunduru mwaka 1998. Aidha, mwaka 2006 eneo hilo liliombwa upya na JWTZ kwa uongozi wa Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya kuendelea kulitumia katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu katika eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Makao Makuu ya Jeshi linaandaa mpango kwa kutumia wataalam wake kuwatuma kwenda Wilayani Tunduru kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Tunduru kutathmini na kulipima upya eneo hilo na kulifanyia mchakato wa kulimiliki kwa misingi ya sheria za ardhi zilizopo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa mwenye swali.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jeshi la Wananchi liliweka kambi katika Vijiji vya Wenje na Makande kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika mipaka yetu na kama inavyofahamika kwamba Wilaya ya Tunduru ni miongoni mwa Wilaya zilizoko mpakani mwa Msumbiji. Je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kurudisha kambi katika maeneo yale ili kuendeleza ulinzi kama ilivyokusudiwa awali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, hivi karibuni Serikali imetangaza halmashauri ya mji katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru; kutangaza halmashauri ya mji ni wazi kwamba tunaongeza maeneo ya utawala. Kuongeza maeneo ya utawala ni wazi pia kwamba idadi ya watu inaongezeka. Je, nini sasa kauli ya Serikali katika kuandaa mpango huo rasmi wa kukabidhi maeneo yale ya Kitanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili wananchi sasa wapate kuyaendeleza maeneo yale? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa anafuatilia sana jambo hili. Niseme tu Mikoa ya Kusini ikiwemo Mtwara na Ruvuma, Kamati za Ulinzi na Usalama zilishafanya maombi ya uimarishwaji wa masuala ya kiulinzi mpakani. Kwa kuwa wamefanya maombi hayo, mawasiliano yanaendelea kufanyika kuona namna bora ya kuimarisha ulinzi huko mipakani. Jambo litakalokuwa limeamuliwa Kamati za Ulinzi na Usalama pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa wanafuatilia wataweza kujulishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili aliloliuliza, nisema tu kama ambavyo nimejibu kwenye jibu la msingi kwamba Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Jeshi la Wananchi watatuma timu ya wataalam. Wakishamaliza kufanyia vipimo kwa kushirikiana na halmashauri wataweka matumizi bora ya ardhi na kuweza kukidhi kile alichokisemea kuhusu ongezeko la watu pamoja na uwepo wa halmashauri ya mji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kutokana na swali la msingi naomba kuuliza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa,

wananchi wa Makoko katika mji wa Musoma waliachia eneo wananchi 95 mwaka 1982 mpaka leo ni miaka 36 hawajalipwa haki yao ya bilioni 1.4 Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa swali hilo kwa sababu mimi nimesomea Makoko.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bulembo kwa sababu amelisemea jambo mahususi ambalo linahusu fidia, niseme tu nimelipokea na nitalishughulikia kujua *status* yake kwa maana ya jambo ambalo linahusisha fidia ili kuweza kujua kama tathmini na masuala yote ya uhakiki yalishafanyika na kama inastahili kutakiwa kulipwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. LYMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa mwaka 1994 Serikali ilifuta ile kwenda jeshini watoto wanaomaliza kidato cha sita kwa lazima na moja ya sababu hiyo ilikuwa ni pamoja na ukosefu wa fedha. Sasa hivi nchi yetu ina fedha na nikikukumbuka maneno ya Mheshimiwa Profesa Kabudi alisema nyumba yenye fedha ndio inaingiliwa na wezi. Sasa je, Serikali haioni kwa kuwa sasa tuna fedha nyingi, fedha hizo zitumike kupeleka wanafunzi wote wanaomaliza kidato cha sita kwenda jeshini ili kuwajengea ujasiri, ukakamavu na uzalendo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa Swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, wa kifupi tu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo aliloliuliza Mheshimiwa Mbunge hata sasa linafanyika mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria

yalisharejeshwa na hivi ambavyo yanafanyika kufuatana na utaratibu wa kwenye makambi ambayo yanaendesha mafunzo hayo. Kutokana na bajeti zilivyotengwa idadi ya wanafunzi na wale wanaoenda kwa mujibu pamoja na wale wanaoenda kujitolea itaendelea kuongezea mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Bajeti inayomalizika hivi sasa ya 2017/2018, kulikuwa na tathmini ya fidia juu ya maeneo ambayo ya jeshi yalichukuliwa kwa wananchi, bilioni 27 na eneo mahususi Jimbo la kilwa masoko la Mheshimiwa Bwege na linaloitwa Rasi Mshindo, Mtaa wa Mpala ni eneo muhimu nyeti ambalo Jeshi wanataka kufanyia kazi kwa ajili ya shughuli zao. Je, nini mkakati wa Serikali kuweza kulipa kwa dharura eneo la Rasi Mshindo, Mtaa wa Mpala, Kilwa Masoko? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masoud ni mjumbe Veterani kwenye Kamati inayosimamia Wizara hizi. Mapendekezo yaliyoletwa na Mheshimiwa Waziri yalikubaliwa na Bunge hili bila hata shilingi moja kushikwa. Niseme tu kwa sababu ndio tunamaliza bajeti tumpe tu Mheshimiwa Waziri muda wa kwenda kuyatekeleza hayo na haya yote ambayo ya kipaumbele kama ambavyo Mjumbe wa Kamati amesema yatapewa uzito unaostahili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, swali linalofuta linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na linaulizwa na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa.

Na. 476

**Kituo cha Utafiti Uyole Kuachia Ardhi ya Kitongoji cha Nkana Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Shirika la Kilimo Uyole lina Kituo cha Utafiti katika Kitongoji cha Nkena, Kata ya Mtanila, Wilayani Chunya; na kwa kuwa kituo hicho kimehodhi eneo kubwa sana na hakijafanya kazi kwa zaidi ya miaka kumi na tano (15):-

Je, ni lini Serikali italiacha eneo hilo kwa wananchi kwa shughuli zao za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa kilimo, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, nianze kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lililokuwa linajulikana kama Shirika la Kilimo Uyole sasa hivi ni Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole ambacho makao yake yapo Uyole Mbeya. Kituo hiki kiko chini ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(TARI - Tanzania Agricultural Research Institute)* chini ya Wizara ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti Tumbaku Tanzania *(TORITA - Tobacco Research Insitute of* Tanzania) inatumia maeneo ya ardhi yaliyopo Tumbi, Tabora pamoja na Mtanila, Chunya na Seatondale kule Iringa kwa ajili ya shughuli za utafiti wa tumbaku kwa lengo la kuwapatia wakulima wa tumbaku teknolojia bora ikiwemo mbegu bora

zinazostahili visumbufu vya tumbaku na ujengaji wa mabani bora. Aidha, watafiti kutoka Uyole Mbeya wamekuwa wakitumia kituo hiki kwa nyakati tofauti kufanya utafiti kwa mazao mbalimbali ikijumuisha mahindi na maharage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya utafiti wa Tumbaku Tanzania *TORITA* bado inahitaji rasilimali ardhi hiyo kwa ajili ya shughuli za utafiti kwa mahitaji ya sasa na ya baadaye. Ikumbukwe rasilimali ardhi kwa ajili ya matumizi ya utafiti huwa inatengwa kwa kuzingatia mahitaji ya miaka mia mbili ijayo. Taasisi hii ina mikakati mikubwa ya kuwezesha wakulima kupata mbegu bora suala ambalo litahitaji eneo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hivi sasa inaendelea kuboresha huduma zake mbalimbali za utafiti kupitia *TARI* ambayo itakuwa na msukumo mkubwa na kujiendesha yenyewe ikishirikiana na sekta binafsi. Hivyo, kuhitaji eneo hilo kwa ajili ya kupanua shughuli zake zote za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambalaswa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo nimeyaelewa yameeleweka nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, utafiti ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kilimo lakini nao ustawi wa wananchi kwa kujipatia kipato nayo ni muhimu. Kwa kuwa wananchi hawa wana eneo dogo la kulima na nyuma ya kitongoji hicho ni hifadhi. Je, Serikali haioni umuhimu wa angalau kugawa pori hili ambalo ni zaidi ya heka mia tano, kugawa kidogo kuwapatia wananchi waweze kulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu sana kitongoji hicho na hiyo kata

anaifahamu kwani wapiga kura wake wako huko. Je, yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kwenye kitongoji hicho kwenda kuwaelimisha wananchi hao kwamba utafiti ni bora?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana, kwa sababu ni Mbunge ambaye anajitoa kwa dhati katika lile Jimbo lake la Chunya kuhakikisha kwamba wakulima wote hususani wa zao la tumbaku na hata hiki kituo kidogo cha utafiti wanatendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba niseme tu kwamba, kile kituo chetu cha utafiti pale Mtanila ni kweli kuna wapiga kura wangu wako pale na mimi nakifahamu na nimefika lakini kinachukua eneo la hekari mia tano na ni hekari tatu tu zinatumika tu kwa ajili ya kituo hicho kwa sababu vituo vya utafiti huwa vinachukua eneo kubwa sana. Kwa maana hiyo nimtake kabisa Mheshimiwa Mzee wangu Kilasile Mwambalaswa kwamba eneo hilo linatumika kwa ajili ya utafiti na ndio maana hata Kituo chetu kile cha Uyole kinatumia eneo hilo katika suala zima la mazao ya mahindi na maharage pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la nyongeza la pili niko tayari kufika Chunya na baada ya Bunge lako Tukufu nitafanya ziara ya kwenda huko. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kafumu na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza; kwa kuwa Vituo vya Utafiti wa Kilimo kama Uyole kama alivyoeleza Mheshimiwa kwenye jibu lake vina umuhimu wa pekee katika kuendeleza mazao yote. Ni lini basi Serikali itafikiria kuja katika

Mikoa ya Kanda ya Ziwa ambako sisi maeneo sio tatizo, wakajenga kituo cha kushughulikia zao la pamba kama ilivyo Uyole na Naliendele kwenye zao la korosho?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Igunga sisi tuna kituo kidogo cha Mbegu na ardhi yao ni nzuri lakini kama Serikali tunajipanga kuhakikisha kwamba tunapanua suala zima la vituo vyetu vya utafiti na hata ukizingatia kwamba sasa hivi tumehakikisha kwamba tuna Taasisi yetu ya *TARI* ambayo itakuwa inajitegemea kwa masuala yote ya utafiti kwa ajili ya kuboresha na kuweza kuandika maandiko mbalimbali ili waweze kupata pesa nyingi zaidi kutoka kwa wahisani mbalimbali katika kuhakikisha suala zima la utafiti linatendewa ubora na haki inayostahili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Ahsante, kwa kuwa jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri, suala la tafiti katika vyuo hivi ni kutokana na ucheleweshwaji wa pesa za maendeleo na ndio maana ardhi inabaki kubwa kwa muda mrefu bila kutumika. Je, Serikali imejipanga vipi katika bajeti hii kupeleka pesa katika Wizara hii hasa eneo la Uyole kwenye hicho Kijiji cha Nkena, lakini na Uyole Mbeya Mjini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majibu yangu ya msingi nimejibu, lakini vilevile wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kafumu kuhusu Igunga nimesema hapa kwamba sisi kama Wizara ya Kilimo tumeboresha kuhakikisha kwamba ile *directorate* yetu ya utafiti sasa hivi itakuwa ni taasisi inayojitegemea kwa maana

ya *TARI*. Pia nimetoa maagizo kwamba *TARI* ama vituo vyetu vya utafiti vyote visitegemee tu pesa za Serikali, lakini pia vijiongeze kuhakikisha vinaandika maandiko *(proposals)* ili waweze kupata pesa za ziada kwa ajili ya kuhakikisha tafiti zetu zinaboreshwa na zinatendewa haki. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea tuko Wizara hiyo hiyo ya Kilimo, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini.

Na. 477

**Kituo cha Mafunzo cha Wanyamakazi Tabora**

**MHE. ALMAS A. MAIGE** aliuliza:-

Kituo cha mafunzo ya Wanyamakazi na utengenezaji wa zana za kilimo katika Kata ya Upuge, Wilayani Uyui, Mkoani Tabora kimechakaa sana na hakifanyi kazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua Kituo muhimu sana kwa mafunzo na zana zake vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athumani Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2002/2003 hadi 2006/2007, ilikarabati vituo sitini na nane vya mradi wa wanyamakazi katika mikoa kumi na nane nchini kikiwemo Kituo cha Upuge kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na kupewa zana kwa ajii ya kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima. Zana hizo ni pamoja na plau, majembe ya palizi, majembe ya matuta, tindo (*rippers*) na mikokoteni kwa ajili ya kutoa mafunzo na kufanya maonesho kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la ukarabati huo ni kuvifanya vituo hivyo kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima katika maeneo yao kwa kushirikiana na Maafisa Ugani waliopatiwa mafunzo juu ya wanyamakazi kwa ajili ya kufundisha wakulima katika vijiji. Aidha, eneo linalolimwa na wanyamakazi limeongezeka kutoka asilimia ishirini hadi asilimia ishirini na nne hivyo, kupunguza matumizi ya jembe la mkono kutoka asilimia sabini hadi asilimia 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia lengo la kuongeza uzalishaji na tija, Wizara ina jukumu la kusimamia upatikanaji wa Zana za Kilimo, utoaji mafunzo yahusuyo Zana za Kilimo, udhibiti wa ubora wa zana zinazoingia nchini kwa kushirikiana na *CAMARTEC,* utafiti na huduma za ugani, pamoja na kuainisha zana mbalimbali kwa matumizi ya mashamba kabla na baada ya kuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Wanyamakazi cha Upuge kwa sasa kina maksai ishirini na mbili na eneo lenye ukubwa wa hekta themanini kwa maana ya (ekari 200), hivyo, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui inakusudia kufanya ukarabati wa zana hizo na kuanza kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani ishirini na Wakulima mia moja katika msimu wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara ya Kilimo inaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Uyui kukitumia Kituo cha Upuge kwa mafunzo na uzalishaji wa mazao ya kilimo ili kupata fedha zitakazosaidia kumudu gharama za kuendesha kituo hicho. Wizara ya Kilimo inasisitiza kuwa Halmashauri za Wilaya zote nchini ni lazima zisimamie na kuendeleza vituo vya wanyamakazi vilivyopo katika Halmashauri zao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maige Almas.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya mdogo wangu Mheshimiwa Waziri Dkt. na pamoja na kunikaribisha Ofisini

kwake na kulijadili suala hili nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa vile kituo hiki kina mfanyakazi mmoja tu. Huyu mfanyakazi mmoja atafundisha wanyama yeye, atatengeneza zana za kilimo yeye na hili ndio ninalosema suala la mzigo mzito kumpa Mnyamwezi hebu tuache, mzigo mzito wapunguze wabebe wenye mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza wataalam kituoni pale ili waweze kufundisha na kutengeneza vifaa vingi au zana za kilimo kwa ajili ya wanyamakazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je Serikali ina mpango gani sasa wa kupeleka mitambo mipya baada ya kupata umeme ili waweze kutengeneza zana za kilimo kwa ajili ya wakulima wangu jimboni kaskazini?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akifuatilia suala hili kwa kipindi kirefu na pia ameweza kufika hata ofisini kwetu kwa ajili tu ya wananchi wake wa kule Upuge pale Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikija katika maswali madogo mawili ya nyongeza ni kweli kabisa kwamba kituo hiki cha Upuge kina mtaalam mmoja, lakini kama Serikali kama Wizara ya Kilimo tulishatoa vituo vyote hivi vya zana za kilimo kwenye halmashauri zote nchini. Kwa maana hiyo nihase halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba zinatilia mkazo vituo vya zana vya kilimo ili viweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhesimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine katika swali lake la pili la nyongeza, ni kweli kulikuwa hakuna umeme na kwa sababu umeme umeshapatikana, Wizara yangu nitatuma wataalam kwenda pale Upuge kufanya *assessment*

kabla ya mwezi wa Nane, kwa sababu kuna mashine zingine pale hazijawahi kutumika kama ile ya vipuri vile vya kuchongea. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Suala la wakulima limekuwa ni tatizo kubwa, kilio hawana mbolea, hawana pembejeo, hawana mbegu kwa wakati, lakini hata hiki kituo cha kilimo ambacho kinawasaidia wakulima kupata unafuu katika kilimo chao kimekuwa nacho ni tatizo. Je, Mheshimiwa Waziri hebu atuambie hasa ni upi mkakati wa Serikali? Nami naipongeza Serikali kwa kuweka kituo hiki hapa Tabora, ni upi mkakati wa Serikali sasa? Wa kuwapunguzia watoto wangu hawa Wanyamwezi na Wasukuma ugumu wa kilimo cha kutumia zana duni?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshikiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la wanyamakazi kwa mfano kule Nyanda za Juu Kusini, kilimo la maksai kimeimarika sana. Ni kweli upande wa huku Mikoa ya Magharibi hakijaimarika, lakini kwenye jibu langu la msingi nilisema kabisa kwamba, Wizara ya Kilimo kupitia *TARI,* tumeanzisha *TARI* ili kuhakikisha kabisa kwamba tunaimarisha na kuboresha vituo vyetu vyote vile vya utafiti pamoja na vya zana za kilimo ambavyo vinasimamiwa na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Mheshimiwa Yussuf mpango mkakati wa Serikali upo imara, hususan Serikali hii ya Awamu ya Tano na ndio maana tumesema tuwe na *TARI* kuboresha na kuimarisha vituo vyetu vyote vya utafiti na nimesisitiza waandike *proposals* wasitegemee tu kabisa pesa ya Serikali au fungu la Serikali, wajiongeze. Nakushukuru**.**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa muda wetu, Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kulikuwa na kiwanda kinachozalisha zana za kilimo kwenye Mkoa wa Mbeya mpaka sasa hatujui nini kinaendelea. Tunaomba kujua kwenye Wizara ya Kilimo nini mkakati wa Wizara kuweza kufufua kiwanda hicho ili kuendeleza zana za kilimo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, hapana, Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, Naibu Waziri wa Viwanda.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho nilitembelea Kiwanda hiki cha Zana za Kilimo pale Mbeya, ni kweli bado kinaendelea kutengeneza zana za kilimo, lakini pia kimejikita kuanza kutengeneza nguzo za *cement* za umeme. Kwa hiyo, kimsingi mwekezaji bado anaendelea na kazi na tunazidi kumshauri aendelee kuongeza jitihada.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda Mbunge wa Malinyi na linaulizwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 478

## Ujenzi wa Barabara Inayounganisha Mikoa ya Morogoro na Ruvuma

**MHE.DKT. HADJI HUSSEIN MPONDA** aliuliza:-

Serikali imekuwa akiahidi kufungua barabara ya Miku1mi – Ifakara –Lupiro - Kilosa kwa Mpepo – Londo – Namtumbo (T16) yenye urefu wa kilomita 396 inayounganisha Mikoa ya Morogoro na Ruvuma:-

(a) Je, ni lini barabara hii itafunguliwa ili ianze kutumika kwa kuwaunganisha wakazi wa mikoa hii miwili?

(b) Je, ni lini kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ya T16 utakamilika na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali imepanga kuunganisha mikoa yote nchini kwa barabara za lami ikiwa ni pamoja na barabara ya kuunganisha Mikoa ya Morogoro na Ruvuma, kwa kupitia Barabara Kuu ya Mikumi – Kidatu- Ifakara – Mahenge/Lupiro – Londo hadi Lumecha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa barabara hii imekwishafunguliwa na inapitika wakati wa kiangazi tu kutokana na baadhi ya maeneo kutopitika wakati wa masika. Kazi ya kuimarisha sehemu zisizopitika inaendelea kadri Serikali inavyopata fedha. Serikali imeanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu na itaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu ya Kwanza, Serikali ilijenga sehemu ya barabara kutoka Mikumi hadi Kidatu (kilomita 35.2); Awamu ya Pili, Serikali imekamilisha ujenzi wa Daraja la Kilombero lenye urefu wa mita mia tatu na themanini na nne pamoja na barabara unganishi yenye urefu wa (kilomita 9.142) inayoishia kwenye Kijiji cha Kivukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa awamu ya tatu inayojumuisha ujenzi kwa kiwango cha

Lami sehemu ya barabara kutoka Kidatu hadi Ifakara yenye urefu wa kilomita 66.9 ambapo Mkandarasi *Reynolds Construction* amekabidhiwa *site* ya kazi na kazi hii imepangwa kukamilika ifikapo tarehe 4 April, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Ifakara Mjini – Mahenge/Lupiro-Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha (kilomita 426,) usanifu wa kina ulikamilika mwezi Juni, 2017. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mponda.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa mchakato unaoendelea kuibadilisha barabara hii kuwa kiwango cha lami. Barabara hii kuanzia Ifakara – Lupiro – Malinyi mpaka Kilosa kwa Mpepo kutokana na mvua za mwaka huu, barabara hii kwa kiasi kikubwa sana imeharibika sana na bajeti ambayo tumeipitisha hapa ya Wazara ya Ujenzi haitoshelezi kabisa kipande kile ambacho wamewekea bajeti. Swali langu hapa, Je, Waziri yupo tayari kutumia hela ya dharura kuongezea bajeti kipande hicho cha barabara kuanzia Ifakara mpaka Malinyi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sera ya barabara inaelekeza Makao Makuu ya Wilaya zote zijengewe barabara kwa kiwango cha lami. Wilaya yetu ya Malinyi haina hata chembe ya lami; je, Serikali ni lini watatekeleza sera hiyo ya ujenzi wa barabara ya lami katika Makao Makuu ya Malinyi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri na hii ni barabara muhimu sana Waheshimiwa Wabunge kwa Tanzania.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizipokee pongezi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitoa

kwa sababu nafahamu kwamba sasa ujenzi wa barabara hii muhimu kama unavyosema umekwishaanza na unakwenda kwa hatua na tupo hatua nzuri. Pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia barabara hii muhimu na katika kufuatilia kwake nilipita barabara hii ili kujionea mwenyewe namna changamoto ilivyokuwa, lakini tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kuhusu swali lake lwa kwanza ni kweli fedha hazitoshelezi kwa mujibu wa bajeti na kwa hali ya mvua iliyokuwa imetokea katika kipindi hiki na niseme tu kwamba tulikuwa tumetoa maagizo kwa Mameneja wa *TANROADS* mikoa yote ili kuweza kutumia hiyo fursa ya bajeti tuliyokuwa nayo kwenye dharura kuweza kutengeneza maeneo korofi nchini kote ili kuhakikisha kwamba barabara zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kusisitiza kumwomba Meneja wa *TANROADS,* Mkoa wa Morogoro kwa namna tunavyoendelea kwamba aendelee kutazama kwa macho mawili barabara hii na kwa sababu tumeshatoa maelekezo naamini kwamba utaratibu wa kukurejeshea hali ilivyoharibika unaendelea. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi Mheshimiwa Mponda na wananchi wa Malinyi na nitahakikisha kwamba maeneo ambayo yamekuwa korofi tunaendelea kuyashughulikia wakati utaratibu wa kujenga kwa kiwango cha lami unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kweli Serikali ina mpango wa kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Mikoa na niseme tu eneo hili la Malinyi na mwenyewe nilipita kama ninavyosema nimeona hiki kipande kidogo sana kwenda kuunganisha na Makao Makuu ya Wilaya hii ambapo pale njia panda ya kwenda Londo, Kilosa kwa Mpepo kuna kipande hiki cha barabara ambacho ni korofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nielekeze tu kwamba kwenye mipango yetu upande wa *TANROADS* Mkoa

wa Morgoro, tutaendelea kuitazama ili tuweze kutibu eneo hili tuweze kuunganisha ili wakati tukipata barabara hii inayokwenda Lumecha kule Namtumbo basi itukute tayari kipande hiki cha barabara kuunganisha na hii barabara kubwa kinaunganika ili Wilaya hii ya Malinyi iweze kuunganika kama ilivyokuwa kwenye sera yetu ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali. Kwa kuwa barabara ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi imeshaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kilometa 50, je, ni lini wananchi wa maeneo ya Nagaga, Mbuyuni, Chiungutwa pamoja na Mpeta watalipwa fidia zao ili barabara hii iweze kuendelea kufanyiwa kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J.KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inafanya juhudi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba tunaboresha barabara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameizungumza. Sasa yupo mkandarasi anatengeneza barabara kutoka Mtwara kuja Mnivata, lakini tutatoka Mnivata – Tandahimba – Newala mpaka Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge anauliza, ni muhimu ili utaratibu wetu uweze kuendelea wa kutengeneza hii barabara kuiunganisha na Mtwara, tuhakikishe tunalipa fidia. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu suala hili la fidia tumelizungumza na nilimwambia kwamba muda sio mrefu nitampa majibu kwa sababu nilikuwa naweka msukumo ili wananchi waweze kulipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli fidia hii ikilipwa pia inatupa sasa fursa ya kuendelea kuboresha barabara hii

ili tuweze kuiunganisha kutoka Mtwara kuja Masasi iweze kukamilika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bwanausi naomba avute subira na kweli najua kwamba kasi iko kubwa ya Serikali kulipa fidia na katika maeneo mbalimbali tunaendelea kulipa fidia lakini na wananchi wa eneo hili la kwako tutaweza kuwalipa mara moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Atupele Fredy.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Mkoa wa Mbeya ni mkoa wa pili kwa wananchi wake kuwa na pato la Taifa ukitanguliwa na Mkoa wa Dar es Salaam, lakini miundombinu yake si rafiki kwa wananchi wake. Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara iliyoahidi kutoka mchepuo wa Uyole kwenda Mbalizi pamoja na barabara kutoka Katumba, Ruangwa, Masoko mpaka Mbambo na Tukuyu yenye kilometa 83? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ni lini mtaiangalia barabara hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu barabara hii amekuwa akiizungumza kweli. Tumezungumza naye hapa ndani ya Bunge, tumezungumza naye nje ya Bunge na hata wakati akitoa mchango wake wakati wa Wizara hii tulivyowasilisha bajeti aliizungumza barabara hii, hata akasema kama hatutengenezi basi yuko tayari kutupeleka shambani tukashirikiane naye kulima, nami nilikuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niwapongeze pia wananchi wa Busokelo kwamba wamepata mwakilishi mzuri kwa sababu anashughulikia sana mipango na mambo mbalimbali kuhakikisha wananchi wake wananufaika na rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu barabara hii ya Katumba – Suma – Ruangwa – Mbambo kuja Tukuyu ni kati ya barabara ambazo pia tumezitengea fedha. Natambua kwamba mwaka 2017/2018 pia tulitenga fedha na mwaka huu tumetenga fedha. Niseme tu kwamba ukiangalia kwenye kitabu cha bajeti huu mradi namba 4150, tumetenga bilioni 17 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mwakibete na kwamba barabara hii tunakwenda kuijenga, muda sio mrefu harakati za ujenzi zitakuwa zimeanza, fedha zipo na nalishukuru Bunge kwa kutenga fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya kutoka Puge – Ndala – Nkinga – Ziba inapita kwenye hospitali kubwa sana za *Mission,* je, ni lini sasa hizo barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, hii barabara tumeizungumza mara nyingi sana ili tuweze kuiweka kwenye usanifu. Nami nitumie nafasi hii kumkumbusha tu kwa sababu niliongea na Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Tabora kwamba kipande hiki cha barabara ni muhimu na anawatambua kwamba wananchi wengi wanakwenda Nkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni muhimu sana kwa barabara kuja Ziba kwa sababu wananchi pia wanatoka maeneo ya Tabora wengine wanakuja Nkinga kutokea Ziba. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tutaiweka kwenye mpango ili barabara iweze kutengenezwa na pia iweze kuongeza huduma muhimu katika maeneo haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ninayo barabara ya Kitunda – Kivule – Msongola, mkandarasi yupo *site* kwa zaidi ya miezi 10 sasa na barabara hii inahudumia kata tano na magari yanakwama hata wakati wa jua kali. Ningeomba nipate kauli ya Waziri kwa nini mkandarasi asilipwe fedha ili aendelee na kazi kuondoa kero kwa wananchi wa Jimbo la Ukonga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara anatambua barabara hii tumezungumza mara nyingi na hata tulikuwa na utaratibu wa kutembelea maeneo haya na wakati wa mvua kwa kweli eneo hili limeharibika sana na nilikuwa nimeelekeza kwamba sasa mkandarasi alipwe pamoja na juhudi kubwa za kulipa wakandarasi sehemu zote nchini lakini alipwe ili barabara hii iendelee kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaendelea kufuatilia kuhakikisha kwamba mkandarasi anapata fedha na binafsi nimeongea na mkandarasi ili ajiandae kwamba atakapolipwa tu mara moja aingie kazini ili sehemu hii korofi iweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mkakati wa Serikali kuhakikisha mikoa yote inaungana inakuwa na mtandao wa barabara; kuna barabara inayoanzia Mahenge – Mbuga

kupitia Mbuga ya Selous mpaka Liwale. Rais aliahidi wakati wa kipindi cha kampeni, lakini sijaona mahali popote katika Wizara kama kuna mchakato wa kutoboa barabara hii kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Lindi. Je, Serikali inatoa kauli gani kutokana na hili?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu kwa swali hilo, kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inafanya utaratibu na ni sera kwa kweli kuunganisha mikoa yote. Mheshimiwa Mlinga tumezungumza kwamba barabara hii niliyojibu swali la msingi pia urefu wa kilometa alizozitaja unaunganisha pia sehemu ya Mahenge kuja pale Lupiro. Pia iko haja ya kuunganisha Mahenge na wenzetu wa kule Liwale, lakini kunahitaji *logistics* nyingi sana kwa sababu inapita katika hifadhi ya mbuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mlinga avute subira, tutaendelea kuzungumza wakati tunaangalia *logistics* nzuri ili tuweze kuwaunganisha wananchi wa Mahenge na eneo la Liwale kwa maana ya Mkoa wa Lindi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimia Devota Minja.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kumekuwa na ahadi ya Serikali ya kujenga barabara ya Bigwa – Kisaki –Mvuha kwa kiwango cha lami kwa miaka takriban 14, lakini…

**MWENYEKITI:** Uliza swali tu!

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali iliwazuia wananchi wa Kata ya Bigwa, Kilakala na Kola wasifanye maendeleo yoyote kwenye maeneo yao ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo. Nataka kujua, kwa kuwa tathmini imekwishafanyika, ni kwa nini Serikali isiwalipe

fidia wananchi hawa badala ya kuwaacha kwa zaidi ya miaka 14 mpaka sasa wanashindwa kuendeleza maeneo yao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ina mpango wa kujenga barabara hii muhimu sana kutoka Biggwa kwenda mpaka Kisaki. Barabara hii niliipita kutoka Biggwa nimeenda mpaka Dutumi kuangalia miundombinu iliyopo katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimfahamishe tu Mheshimiwa Devota kwamba pia tutaitumia hii barabara kwa ajili ya kupitisha vifaa na huduma mbalimbali kwa ajili ya *access* ya kwenda kwenye ujenzi wa Stiegler's *Gorge* kule tunapokwenda kutengeneza umeme. Kwa hiyo, tunaona umuhimu wa barabara hii pamoja na barabara inayotokea Ngerengere kuja Mvuha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wananchi kwa kweli kwa kuacha maeneo wazi kwa sababu itatuwia urahisi wa sisi kuanza taratibu kwa sababu ujenzi wa barabara unaanza katika hatua ya usanifu, kufanya michoro na hatua ambayo ilikuwa inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Devotha avute subira na nitalifuatilia suala hili kuona wananchi wanalipwa haki zao, lakini pia ni fursa kwetu kuweza kushughulikia barabara hii kwa sababu barabara ni huduma. Tutakapowapa barabara wananchi wake pia watanufaika na barabara hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza moja la nyongeza. Mkandarasi aliyepewa barabara

ya Urambo – Kaliua kilometa 28 tu ameonesha udhaifu mkubwa kuanzia mwanzoni sasa hivi ni karibu miezi 10 kazi iliyofanyika ni ndogo sana. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri anaweka vyombo kwenye *site,* Waziri akiondoka anaondoa vyombo. Serikali haioni sasa sababu ya kubadilisha mkandarasi huyu ili wananchi wa Kaliua na Urambo waweze kupata barabara ambayo ni kubwa sana kwa ajili ya uchumi wa Kaliua na Urambo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, huyo mkandarasi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi taarifa nizipokee kama ni taarifa mpya kwangu kwa maana kwamba tutafanyia kazi ili tuone kama kuna huu mchezo unafanyika wa kuweka vifaa *site* wakati wa ukaguzi halafu baadaye vinaondolewa ili tuweze kuangalia na tuchukue hatua. Kwa sababu ujenzi wa barabara hii na mkandarasi kuwepo *site* ni kwa mujibu wa taratibu na pia iko mikataba na kama kuna mchezo huu tutaona *rooms* zilizoko kwenye mkataba wetu ili tuweze kuchukua hatua stahiki na mwenyewe nitahakikisha nalifuatilia hili mguu kwa mguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara kutoka Mpwapwa – Lupeta kwenda Matomondo – Mlali mpaka Pandambili ni barabara ya mkoa. Namshukuru sana Meneja wa Mkoa anajitahidi lakini kwa kuwa kuna daraja la Matomondo la Tambi linashindikana kujengwa kwa sababu ya gharama kubwa. Je, Waziri anasemaje kuhusu daraja hilo na yuko tayari kutembelea hiyo barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu swali moja tu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mara kwa mara nimetembelea eneo hili la Mpwapwa ili kuweza kujionea hali ya uharibifu kwa sababu tuko karibu hapa na nimeweza kuona kwamba ziko changamoto. Ni kweli daraja ambalo Mheshimiwa Mbunge anazungumza ni daraja kubwa, iko nafasi ya kuweza kuhamisha ili daraja liwekwe sehemu ambapo gharama za ujenzi zitakuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali tuweze kujenga kwa tija lakini pia kupunguza gharama, gharama zikipunguza zitatuwezesha kutoa huduma maeneo mengine. Kwa hiyo, namwambia Mheshimiwa Mbunge, nitakuwa tayari kutembelea eneo hili ili wakati mwingine mimi na yeye tukiwa na wataalam tuweze kuona kwamba ni wapi tunaweza tukahamishia daraja hili ili tusaidiane pale itakapohitajika saa nyingine wananchi kuachia maeneo haya. Lengo tuweze kupata daraja ambalo linawapa huduma wananchi hawa wa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumevuta sana muda wetu, mnaelewa kwa nini hasa kwenye swali la barabara, ndiyo maana nimetoa nafasi nyingi kidogo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; nitaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika. Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Spika Mbunge ambao wanatoka Tanganyika *Law Society* wakiongozwa na Rais wa Taasisi hiyo ndugu Fatma Amani Karume, Ndugu Fatma Karume hebu simama wakuone. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiyo Rais wa *TLS (Tanganyika Law Society).* Tunampongeza sana, ni miongoni mwa Wanasheria shupavu wa nchi hii. Amefuatana na wafuatao; ndugu Joseph Mntimbwa ambaye ni *Vice Chapter Convener* wa Dodoma. Mwingine ni Nicolaus Duhia ambaye ni *Honorary Treasury* wa *TLS;* Ndugu Joseph Mnzava, *Treasure;* Ndugu Stephen Awesso, *Council Member;* ndugu Asha Ally Sinda, *Council Member;* Ndugu Jebra Kambore, *Council Member;* Ndugu Mary Munisi, *Chapter Convener;* ndugu Kaleb Gamaya, *TLS CEO,* huyu ndiyo Mtendaji Mkuu wa chombo hiki; ndugu Mariam Othman, *TLS Corporate Secretary;* Ndugu Mackhason Bunerwa, huyu anatokea Dodoma hapa; na ndugu John Mwang'ombola, *Finance Manager.* Hao ndiyo wageni wa Spika. *(Makofi)*

Halafu tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni viongozi na wachezaji wa timu ya mpira wa miguu ya Mbeya wakiongozwa na kocha mchezaji na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mheshimiwa Amos Makalla. Karibuni sana Waheshimiwa wageni wetu pamoja na Mkuu wetu wa Mkoa wa Mbeya, Mheshimiwa Amos Makalla. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wafanyakazi wa Kituo cha Redio cha *FM* kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Meneja Mkuu wa Redio hiyo Mheshimiwa Tantenda Nyawo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Alex Gashaza, Mbunge wa Ngara ambao ni rafiki zake kutoka Mkoani Kagera. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni watumishi wa *SDA,* Jimbo la Kaskazini mwa Tanzania kutoka Jijini Arusha. Karibuni sana wageni wetu kutoka Arusha. *(Makofi)*

Wageni 22 wa Mheshimiwa Atupele Mwakibete, ambao ni Timu ya Inuka Uangaze *(Rise and Shine)* ya Mtume Boniface Mwamposa toka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Atupele Mwakibete ni waliokuwa wafanyakazi wenzake tisa kutoka *Henry Jackson Foundation Collaboration with us (Department of Defence)* iliyoko nchini Marekani. Wako wapi wageni wetu? Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza, ambao ni Kwaya ya Maruku kutoka Kanisa la KKKT Mkoani Bukoba. Maruku Kwaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Oscar Mukasa, kutoka Baraza la watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania *(NACOPHA).* Wako wapi? Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 23 wa Mheshimiwa Almas Maige, ambao ni Wenyeviti wa CCM wa Kata, Jimboni Uyui Mkoani Tabora. Naona Mheshimiwa Masoud amenuna ghafla. Hao ni wageni wa CCM. *(Kicheko/Makofi)*

Pia tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoani Mara. Wako wapi? Haya kutoka Mara, someni sana vijana. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Wilaya ya Malinyi Mkoani Morogoro. Wito wangu ni huo huo kwenu wanafunzi. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, ambao ni binti yake na familia yake kutoka Chuo Kikuu cha *Virginia State* iliyopo nchini Marekani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambaye ni Ndugu Jailos Mwaijande kutoka Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Ally Ungando, ambao ni wapiga kura wake kutoka Kata ya Salale Mkoani Pwani. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Chikota, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimboni kwake Nanyamba, Mkoani Mtwara, Ndugu Ramadhani Nahonyo. *(Makofi)*

Pia tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula, ambao ni Viongozi wa Serikali za Mitaa na Makada wa CCM kutoka Jimboni kwake Nyamagana Mkoani Mwanza. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Mashimba Ndaki, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango Jijini Dodoma. Wako wapi? Karibuni sana wageni. *(Makofi)*

Kundi la tatu ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kwa hiyo, tuna wageni 44 kutoka KKKT Dayosisi ya Dodoma Usharika wa Kanisa Kuu wakiongozwa na Mchungaji Hosea Mbaga. Hawa wamekuja kwa mafunzo. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi wengine 46 na Walimu wanne kutoka Shule ya Msingi *Dar-ul-Muslimeen* ya Jijini Dodoma. Sijui kama nimetamka vizuri jina hilo, mtaniwia radhi kama nimelikosea. *(Makofi)*

Matangazo mengine; Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* anawatangazia Wabunge wote kuwa kesho siku ya Jumamosi tarehe 23 Juni, kwenye kiwanja cha Kilimani Jijini Dodoma kutakuwa na Bonanza la mpira wa miguu kati *ya Bunge Sports Club* (*Ndugai Boys*) wakicheza na *Mbeya Veteran*. Mechi hiyo itaanza saa 9.30 Alasiri. Baada ya mechi hiyo, timu yetu ya

*Bunge Sports Club* itacheza tena na Timu ya *NACOPHA Football Club*. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwa tukio hilo, mhudhurie kwa wingi. *(Makofi)*

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, linasema: "Waheshimiwa Wabunge, nawatangazia kuwa leo Ijumaa tarehe 22 mwezi wa Sita kutakuwa na tukio la uchangishaji fedha *(fund rising)* kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya mfano kwa watoto wa kike kwenye kila Jimbo hapa nchini. Tukio hili litaanza saa 12.00 jioni katika eneo la sherehe maalum za Bunge, karibu na Zahanati ya Bunge. *(Makofi)*

Kufuatia hafla hiyo, mambo yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa. Waheshimiwa Wabunge wote wanaombwa kuhudhuria kwenye hafla hiyo bila kuambatana na wageni wao wowote na kutakuwa na *roll call*. Narudia. Wabunge wote, wanaombwa kuhudhuria kwenye hafla hiyo bila kuambatana na wageni wao wowote. Mnaelewa maana yake? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** La pili, kwa kipindi cha jioni cha Bunge hakutakuwa na wageni watakaoruhusiwa kuingia Bungeni kwa ajili ya mafunzo au wageni wa Wabunge. Mnataka nirudie na hilo? Limeeleweka hilo. *(Makofi)*

Tatu, Wabunge watakaoshiriki kwenye kucheza na kuimba muziki, watakaofanya sarakasi, vichekesho, maonyesho ya mavazi na kwaya wanaombwa kuhudhuria maandalizi *(rehearsal)* itakayofanyika kwenye eneo la tukio kuanzia saa 7.00 mchana.

Hii ni muhimu sana kwa sababu unaweza ukafika pale ukapata ile *stage fright*, unaogopa. Kwa hiyo, lazima ulizoee kidogo hilo. Wengine leo mtafurahi sana. Ndiyo maana Mheshimiwa Spika anataka wote tuhudhurie. Atakayeshindwa ni yule ambaye tunampeleka Hospitali na machela.

Pia mjiandae na michango, hili ni tukio kubwa, haijawahi kutokea na litarushwa moja kwa moja kwenye Majimbo yetu, *(live)* ni nchi nzima inaona siku hizi, siyo kama zamani. *(Makofi)*

Nimemaliza matangazo. Sasa ili tufanikishe tukio hilo ambalo lazima lianze saa 12.00, sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ambaye ni *Chief Whip* wa Serikali Bungeni, aweze kuandaa vizuri shughuli hiyo kwa Kanuni za Bunge. Mheshimiwa Jenista.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) Bunge litakutana hadi saa 7.00 mchana ambapo husitishwa mpaka saa 11.00 jioni;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Kanuni ya 28(4) Bunge huendelea kukaa mpaka saa 1.45 usiku ambapo huahirishwa hadi kesho yake au siku nyingine itakayotajwa;

NA KWA KUWA leo Ijumaa tarehe 22 Juni, 2018 kumepangwa kufanyika tukio kubwa la uchangishaji fedha *(fund raising)* zitakazotumika kwenye ujenzi wa vyoo vya mfano kwa ajili ya mtoto wa kike kwa kila Jimbo hapa nchini; na tukio linaratibiwa na Chama cha Wabunge wote Wanawake Tanzania *(TWPG)* ambapo Waheshimiwa Wabunge wote wamealikwa kuhudhuria ili kujumuika na wageni wengine pamoja na wadau mbalimbali waliyopewa mwaliko wa kuhudhuria shughuli hiyo; *(Makofi)*

NA KWA KUWA tukio hilo la uchangishaji fedha limepangwa kuanza kufanyika saa 12.00 jioni na ufanisi wake

kwa kiasi kikubwa unategemea ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge wote; Inabidi Bunge litengue Kanuni ya 28 ya Kanuni za Bunge inayohusu muda wa Vikao vya Bunge kwa Mujibu wa Kanuni ya 153(1);

NA KWA KUWA Mheshimiwa Spika amekubali na kuona umuhimu mkubwa wa kutengua Kanuni husika ili kutoa fursa kwa Wabunge kushiriki katika tukio hili la kihistoria lenye manufaa makubwa kwa wananchi wote wa Tanzania; *(Makofi)*

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya kufanikisha tukio la uchangishaji fedha zitakazotumika kwenye ujenzi wa vyoo vya mfano kwa ajili ya mtoto wa kike katika kila Jimbo hapa nchini, Kanuni ya 28(2) na Kanuni ya 28(4) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 28(2) ambayo inaelekeza kwamba Bunge linapositishwa saa 7.00 mchana lirejee tena saa 11.00 jioni, itenguliwe na badala yake Bunge lirejee saa 10.00 alasiri. Kanuni ya 28(4) ambayo inaelekeza kwamba Bunge liendelee kukaa hadi saa 1.45 usiku itenguliwe na badala yake Bunge liendelee kukaa hadi saa 12.00 jioni ambapo litaahirishwa hadi siku nyingine itakayotajwa. Mabadiliko haya ya muda wa vikao yatatumika kwa siku ya leo ambayo ni siku muhimu, yaani Ijumaa, tarehe 22 Juni, 2018 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni za Bunge ili kuwezesha shughuli za uchangishaji fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya mfano kwa ajili ya mtoto wa kike katika kila Jimbo ilikubaliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, leo Waheshimiwa Wabunge saa 10.00 badala ya saa 11.00; mpaka saa 12.00 badala ya saa mbili kasorobo; na ni kwa leo tu kama hoja ilivyotolewa na kuamuliwa na Bunge. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na**

**Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Cecil.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 68, nikiomba mwongozo wako kutokana na mambo yanayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kushangaza sana, Serikali tunatambua ndiyo ambayo ina-*regulate* mambo mbalimbali, inasimamia masuala ya amani, ikiwemo masuala ya kidini, lakini pia masuala yote ya *affairs* za wananchi. Siku za karibuni pameibuka mambo na mivutano, ambayo tulimwona Mheshimiwa Jenista alikuwa anajaribu kuikemea hasa zaidi inayogusa masuala ya imani za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna gazeti moja linaitwa Jamvi la Habari; kwa muda wa wiki moja mfululizo au mbili limekuwa likiandika sana habari za dini na zinazoelekeza kwenye uchochezi kutaka kuwagombanisha watu na makabila yao, kutaka kuwagombani watu wenye imani ya Kikristo hasa Wakatoliki; na Serikali hii imelifumbia macho

kwa jinsi ambavyo tunaona. Hatujasikia kauli ya Serikali, hatujamsikia Mheshimiwa Mwakyembe ambaye ana-*regulate* hivi vyombo na huu ni uchochezi mkubwa unaoweza kufarakanisha sana watu hasa ndani ya Kanisa Katoliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mwongozo wako, kutokana na jambo hili, nini kauli na nini mwongozo wako kwa uchochezi unaofanywa na gazeti la Jamvi la Habari kwa kuwachochea Wakristo wa Kanisa Katoliki na Maaskofu wasiowaamini Wachaga, pamoja na wengine; na wanataka kugombanisha na Dola?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba Mwongozo wako ili tuweze kujua nini kinaweza kikafanyika kwenye hali kama hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kwa hayo aliyoyaeleza, lakini kama mlivyomsikia ninyi wenyewe, kwa suala ambalo amelilezea halikutokea hapa mapema Bungeni. Amemtaja Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na hilo gazeti analolitaja Jamvi la Habari, kwa taarifa linazoandika.

Mimi Mwongozo wangu, kwa kuwa halikutokea mapema humu Bungeni, siwezi kusema kama linaruhusiwa na Kanuni zetu au la, maana halijatokea humu Bungeni. Serikali ipo humu na Serikali ina mikono mirefu sana na macho yanayoona mbali sana, nasi tumeweka msimamo kabisa. Isipokuwa kama kuna hoja mahsusi iliyofika Bungeni kwa taratibu zinazokubalika na Kanuni za Bunge, Bunge haliwezi kutumika kama uwanja wa kuongea masuala ya dini.

Kwa hiyo, naiachia Serikali, kama wao wanaona kuna haja ya kulisemea hapa, wamo humu ndani. Kama hawako tayari kulisemea, naamini umesema kitu ambacho watakichukua waendelee kwenda kukifanyia kazi kwa taratibu za kawaida zilizopo. Mambo ya imani yangu ni yangu

mimi mwenyewe. Kwa hiyo, Mwongozo wangu ulikuwa ni huo, halijatokea mapema hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wachangiaji wetu walioletwa kwa taratibu zetu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hebu tuache uchokozi. *(Kicheko)*

Tunaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza kwa sababu ya majukumu yetu ya leo, naye ni kiongozi muhimu kwa maandalizi hayo, nataka nimpe heshima ya kwanza afungue dimba. Mheshimiwa William Ngeleja, atafuatiwa na Profesa Anna Tibaijuka na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtemi Chenge, ahsante sana kwa fursa hii. Nimesimama hapa nikiungana na Waheshimiwa Wabunge walio wengi kuipongeza sana Serikali. Kwa kuanza kabisa, naunga mkono hoja ya Serikali iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utangulizi wetu kwenye hotuba hii ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi inasema namna ambavyo hotuba hii imeandaliwa, lakini moja ya mambo yaliyozingatiwa ni pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, nikiwawakilisha pia Watanzania kwa ujumla wake kwamba, hivi karibuni tumesikia taarifa zilizoenea kupitia vyombo vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii, kwamba ule utengenezaji wa kivuko cha pale Kigongo Busisi, eneo ambalo linaunganisha Wilaya ya Misungwi kwa Mheshimiwa Charles Kitwanga pamoja na Busisi upande wa Sengerema sasa uko hatua za mwisho kabisa na kile kivuko kimeshaanza majaribio kwa sababu, kimeshashushwa ziwani tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 hadi mwaka 2020. Kwa hiyo, kwa dhati kabisa naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, natumia fursa hii kuishukuru sana Serikali na nitataja baadhi ya Mawaziri kwa mambo ambayo wameiwezesha hivi karibuni kwa taarifa nilizonazo. Kwanza ni Mheshimiwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo. Wanakatunguru pale Jimboni Sengerema kwenye Kituo chetu cha Afya, mjiandae tumepata fedha za maboresho shilingi milioni 400 zinakuja. Sengerema Sekondari tumepata zaidi ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia utekelezaji wa miradi ya maji Sengerema na Taifa kwa ujumla, nasi hujatusahau, maelekezo yake yanaendelea kusimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri, Mheshimiwa Kakunda ufuatiliaji wa malipo ya fedha zile, ziara yake imezaa matunda, tumeshapata fedha kwa ajili ya Mkandarasi wa mradi wa maji Buyagu, Kangalala, Bichocho na utaratibu wa ukamilishaji unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy kwa msaada wake ambao ametupa. Nataja hawa wachache kwa niaba ya Serikali nzima kwa sababu muda hauruhusu kutaja wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizamia kwenye hotuba yetu iliyoko mbele yetu na hasa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Taarifa za Kiserikali pamoja na Kamati; naipongeza sana Serikali, lakini pia Kamati ya Bunge ya Bajeti pamoja na Kamati ya Uongozi kwa ujumla wake kwa maelekezo ya Mheshimiwa Spika, kwa namna ambavyo walizitumia zile siku sita kushauriana. Wameshauriana mambo mengi. Yale mazuri tumeshayasema sana na

yapo wazi, lakini katika Taarifa ya Kamati ya Bajeti, pia zipo changamoto ambazo ziliainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nizungumzie changamoto inayohusu sera za matumizi, kama ambavyo imeainishwa katika Taarifa ya Kamati ya Bajeti na hasa katika ukurasa wa 32, wakati nafanya mapitio na kupitia taarifa hiyo kuhusu Mpango wa Fedha na Matumizi kwa mwaka huu wa fedha mpya unaokuja mwaka 2018/2019. Moja ya jambo kubwa lililojitokeza ni kwamba kwa miaka kadhaa sasa kama nchi tumekuwa na changamoto ya kutokidhi matarajio ama maoteo ya bajeti tunazozipanga hapa, aidha kwa kutotimiza malengo kutokana na vyanzo vya ndani, lakini pia kwa kutopata misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameshauri hapa kwamba, kwa mujibu wa kanuni na ni jukumu la kikanuni, lakini pia inatokana na Katiba, kama Bunge tuna wajibu wa kuishauri Serikali; wameshauri kwamba suluhu ya kuwezesha utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo Serikali inafanya sasa hivi, natambua ujenzi wa reli ya kisasa, *Stiegler's Gorge,* lakini ununuzi wa ndege na miradi mikubwa kwa mfano kule Mkulazi pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iridhie ushauri wa Bunge lako kupitia Kamati ya Bajeti na michango ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa sasa kwa mazingira tuliyonayo na uwezekano wa kukusanya vyanzo vya mapato ambavyo tumeviainisha kwenye bajeti kwa asilimia 100 ni mdogo, tunaiomba Serikali na naamini kwamba Mheshimiwa Rais anafuatilia mjadala huu, tukakope kwa masharti nafuu. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri ametuthibitishia kwanza kukopa siyo dhambi, lakini sisi kama Taifa kwa mahesabu yetu bado tunakopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali itafakari jambo hili. Najua kuna kipindi fulani ilionekana kwamba pengine kukopa kungetuongezea madeni *(liability),*

Deni la Taifa, lakini kwa nchi kama yetu, kama nchi tajiri zinakopa kwa nini sisi tujivunge kukopa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali ikakope kwa mikopo yenye masharti nafuu ya muda mrefu, tujipe muda kwa vyanzo vyetu vya mapato vilivyopo ndani, tupumue, lakini tuweze kutekeleza miradi inayogusa wananchi moja kwa moja, miradi inayohusu Sekta za Kilimo, ambacho ndiyo kipaumbele, kinabeba wananchi zaidi ya asilimia 66, lakini mchango wake tunaona kwenye pato la Taifa ni 4% tu. Hili ni jambo ambalo tunahitaji kuliongezea muda wa kulifanyia kazi vizuri. Kwa hiyo, tukakope, lakini tuishirikishe sekta binafsi na pia tufanye miradi kupitia utaratibu wa ubia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo lake, nchi zote duniani zinapoelekea kwenye chaguzi na hasa miaka ya uchaguzi, bajeti zake huwa zinaathiriwa kwa sababu ya suala la uchaguzi. Sisi Tanzania mwaka kesho tuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mwaka 2020 tuna Uchaguzi Mkuu; vyovyote itakavyokuwa hatuwezi kukwepa kwamba kuna rasilimali fedha nyingi na hasa ya ndani itakwenda kwenye uchaguzi. Kwa sababu hiyo ndiyo msingi katika mustakabali wa Taifa letu. Tutafanyaje kama hatutakuwa na mikopo yenye masharti nafuu ya kutusaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunaomba sana Serikali izingatie ushauri huu, tufungue milango, tukakope kwa masharti nafuu, tuendeleze nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi, lipo jambo nimeliona nikasema niliseme tu niishauri Serikali. Kwa namna ambavyo lipo kwenye Taarifa ya Kamati ya Bajeti ni kama linaashiria hivi, kuna taratibu ambazo tumeziweka kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi yetu ni kama kuna viashiria hivi tunaelekea kuvikiuka. Hatujafikia hatua hiyo, kwa sababu Hotuba ya Bajeti na Mheshimiwa Spika, alielezea vizuri sana siku ile wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alivyowasilisha kwamba haya mapendekezo tunayoyajadili sasa hivi, sisi ndio tunatengeneza bajeti ya nchi. Nashauri kwa

yale maeneo ambayo Kamati yenu mliyabaini Serikali isikilize ushauri, kwa sababu viashiria vyake sio vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza inaonekana kuna viashiria vya kukiuka sheria kuhusu matumizi ya fedha ambazo zimetengwa kwa maeneo maalum na hasa Mifuko mbalimbali ambayo imeanzishwa kisheria. Halijafikia pabaya kwa sababu, sisi ndiyo tunaamua, hebu tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine inaonekana Kamati imebaini kwamba Wizara ya Fedha na Mipango inaanzisha utaratibu wa kubadili matumizi ya fedha zilizotengwa kisheria kwa ajili ya matumizi maalum. Sasa hili siyo jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili la kupendekeza kuanzisha Akaunti Maalum ama Akaunti Jumuifu ya Hazina. Sasa ukisoma ukurasa wa 40 mpaka wa 41 tumeelezwa kwamba hii imetokana na makubaliano ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki; lakini Kamati ya Bajeti ilipozamia kule imebaini kwamba kumbe sisi kama nchi tuna fursa ya kuliangalia jambo hili kwa namna yake; na madhara yake ni kwamba kama itaanzishwa hii *single account* maana yake ni kwamba hata ile Mifuko ambayo tumeanzisha kisheria tukatenga fedha, kama suala la umeme, masuala ya barabara, reli na masuala ya korosho na mengine, miradi ya maji, nazo zitahitajika kwenda kwanza Mfuko Mkuu wa Hazina halafu ndio zije. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa ushauri wangu ni kwamba jambo hili linahitaji mjadala mpana zaidi, ni zaidi ya kupitia kwenye bajeti hii, kwa sababu, tulianzisha sheria maalum na mpaka sasa ukiangalia ni kama hatujaathirika, matokeo yake naona mifuko ile imekuwa ikitekelezwa kwa utaratibu ambapo matokeo yake ukiyapima ni chanya zaidi kuliko hasi. Sasa labda tujipe muda zaidi tuangalie, tuendelee na utaratibu, twendenao kwa sasa, lakini kama kuna haja ya kufanya hivi, basi tufanye mjadala mpana zaidi kuliko ilivyo sasa kupitia utaratibu wa bajeti kwa sababu, tukifanya vile tunaweza kuathiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Taarifa ya Kamati ya Bajeti tumeyabaini kwa mfano, makusanyo ya Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, ziko fedha zaidi ya *1.5 trillion.* Sizungumzii lile suala la *CAG,* zimesemwa hapa kutokana na masuala ya kodi kulikuwa na mabishano na makampuni fulani, hazijakusanywa kwa sababu ambazo hazijaeleweka. Sasa kama Serikali yenyewe kuna mambo haijayaweka sawa, tunashauri kwamba tusiongeze tena mzigo wa fedha zote kwenda kule. Tujipe muda kidogo, nadhani tunaweza kufanikiwa, lakini wazo inawezekana limekuja kwa nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naona kama kiashiria chake siyo kizuri, tunasema tukisoma Katiba yetu ya nchi, Ibara ya 145 na Ibara ya 146, zimeanzisha utaratibu wa Serikali za Mitaa maalum kabisa na zikatambuliwa. Hili jambo nilivyokuwa nalisoma kwenye Taarifa ya Kamati ya Bajeti, ni kama vile Kamati inasema: "Kwa namna ambavyo baadhi ya hatua zinazochukuliwa za Serikali Kuu ni kama vile zinakwenda kuathiri uhalali na umuhimu wa kuwepo kwa hizi Mamlaka za Serikali za Mitaa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siyo jambo zuri sana, kwa sababu, ile *Decentralization By Devolution* tuliyoanzisha miaka ile kwa mujibu wa Katiba, lakini pia mwaka 1998 kulikuwa kuna Tamko la Kisera na tunafahamu manufaa ambayo tumeyapata; na kwa sababu, kuanzisha utaratibu ule ilitokana na uzoefu ambao tuliona kwamba kuendesha nchi kwa msingi wa kutoka Serikali Kuu peke yake ni mgumu sana duniani na utaratibu huo umekwaza baadhi ya nchi nyingi tu duniani na ndiyo maana sisi tuka-*opt* kwenda kwenye hiyo *route* ya kusema tuwe na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Mitaa ni Serikali kamili kabisa. Kwa hiyo, nashauri kwamba tupunguze uwezekano wa kiashiria hiki kushamiri kwa sababu bado tuna muda na jambo halijaharibika na Waheshimiwa Wabunge tulitazame Kitaifa zaidi, tusiangalie kwamba kwa kufanya hivi tutakuwa tunakwaza kitu gani,

hapana. Ni kwa faida yetu, nami naamini kwamba utaratibu ule haujatuathiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunafahamu kwenye ngazi ya Halmashauri, wapo Madiwani, zipo Halmashauri zimeshindwa kufanya vikao vyake kabisa na hawajalipwa stahiki zao kwa sababu hakuna fedha. Ni kwa sababu tunazi-*cripple.* Nashauri kwamba, hili jambo tuliangalie tena na naamini kwamba bado tuna fursa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Deni la Taifa, napendekeza *solution* tu. Mengi yamesemwa, lakini nataka nirejee miaka ya 1990 ilivyokuwa. Serikali ilikuwa na utaratibu wa kununua dhahabu, baadaye baadhi ya Watendaji hawakufanya vizuri sana, hatukufanikiwa, tukajiondoa, lakini wakati tunajiondoa wakati ule bei ya dhahabu kwa mfano kwa kigezo cha *ounce... (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya dhahabu haikuzidi dola 270, leo ni zaidi ya dola 1,400. Kilichotokea ni nini? Shilingi toka miaka ya 1990 Serikali tulivyojitoa kwenye kununua dhahabu, shilingi yetu imeporomoka kwa kiwango cha 80% na wataalam wa uchumi wako hapa wanaweza kurekebisha, lakini dhahabu imepanda ka zaidi ya 700%. Tungekuwa na dhahabu zetu ambacho tungekuwa tunafanya katika wakati wa mshtuko, unatoa dhahabu yako kutoka kwenye ghala lako, unaingiza sokoni unauza, unapunguza Deni la Taifa. Nikadhani kwamba Serikali itafasiri hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa gesi. Miaka ya 1992 tulipigwa na ukame ndiyo maana yakaja masuala ya *IPTL* ambayo yamekuja kuliyumbusha Taifa, ilitokana na ukame. Kutegemea chanzo kimoja kuna *risk* kubwa.

Ninashauri kwenye eneo ambalo nalifahamu kidogo. Suala la gesi tuliyonayo, leo tunajivunia trilioni 57 *cubic feet* za gesi ambazo tunasema ni *probable,* lakini ukizileta sasa kwenye uzalishaji *normaly* unazalisha 30% ya hiyo gesi uliyonayo. Asilimia hiyo 57 tunayoizungumzia, unaongelea trilioni 10 ziko nchi kavu, trilioni kama 40 na kitu ziko baharini kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ianze kuwekeza kwenye hii gesi iliyoko nchi kavu, kwa sababu, tusitegemee chanzo kimoja tu cha miradi ya maji, ni hatari kubwa kwa Serikali ya viwanda ambayo tunaitarajia kama tutakuwa na chanzo kimoja. Miaka ya 1990 tulikwama na ndiyo maana tukaenda kwenye mipango ya dharura, matokeo yake tukaja kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda huu tunaouzungumzia, hauwezi kuhimiliwa na Megawati 2,100 tu za *Stiegler's Gorge* ama za viwango vingine vilivyoko hapa, ni pamoja na miradi ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana. Serikali itafakari, twende kwa pamoja, uwekezaji wa *Stiegler's Gorge* ni mzuri, lakini tusipuuze pia suala la uwekezaji katika sekta ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Ngeleja. Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Omari Mgumba wajiandae.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nami sina budi kuungana na wachangiaji wa hapo awali kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mpango na Naibu, Mheshimiwa Dkt. Kijaji na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Fedha ambayo kwa kweli ndiyo inakutanisha Serikali yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kusema kwamba mpango ni mzuri na kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, naomba kusema kwamba, mapendekezo yangu yanaenda moja kwa moja na Kamati yetu ya Bajeti ambayo sina budi kumpongeza Mwenyekiti wetu mahiri na Makamu wake, Mama Hawa Ghasia na Mheshimiwa Jitu. Kwa kweli, wanatuongoza vizuri na andiko lenyewe mnaliona kwamba limekaa vizuri. Mheshimiwa Mwenyekiti, lililobaki ni Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Makamu wake ambao tunakutana nao mara kwa mara kutusaidia tu na sisi tuongeze zaidi yale tunayoyasema kwa namna ya ku-*amplify. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Mheshimiwa Waziri naunga mkono hoja iliyo mbele yetu, lakini nataka kufafanua mambo yafuatayo. Tuanze kabisa na Wizara yenyewe ya Fedha. Hii ni Wizara muhimu sana. Sina budi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuunganisha Fedha na Mipango, lakini naanza kuwa na wasiwasi nikiona mipango inafifia chini ya fedha. Nami kama mchumi, nakuwa na wasiwasi mkubwa sana nisipolisema hili kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie jinsi atakavyolinda *capacity* ya *National Plan. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa na naomba ieleweke kwamba bila kuwa na *Commission for National Economic Planning* itakuwa vigumu sana kujua tunakokwenda. Tunaweza tukajikuta katika mchezo wa juhudi bila maarifa na Mwalimu Nyerere alionya dhidi ya mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana suala hili la hatima ya *National Plan Commission,* sasa hivi ikiwa inafanya kazi vizuri ndani ya Wizara hiyo sio shida, lakini inakuwa na *enabling legal framework* ambayo inaruhusu mambo ya mipango kufanyika. Hili naomba liwe mezani na Mheshimiwa Waziri atufafanulie sasa kwamba anajipangaje? Dhana ya *Commission for National Economic Planning* tunailindaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; kwa kuwa tunangalia sasa bajeti ya Serikali, kuna suala zima la Mamlaka ya Waziri mwenyewe huyu. Nimefurahi sana; na kama Mwanakamati wa Bajeti tunaipongeza Serikali kwamba hatimaye wamekubaliana na mapendekezo ya siku nyingi ya Kamati kwamba, Waziri wa Fedha arejeshewe mamlaka yake ya uamuzi wa kusamehe kodi pale inapostahili, hususan katika mikataba ya wahisani au miradi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupendekeze kama Kamati ilivyopendekeza kwamba mamlaka yake yasikomee kwenye miradi ya Serikali, lazima pia na Serikali ielewe kwamba, Halmashauri nazo ziweze kupata msamaha huu. Kwa hiyo, nafikiri mamlaka haya pia yawe *total,* yasiishie tu miradi ya Serikali, lakini yaende hata kwenye Halmashauri na miradi mingine inayoweza kupatikana yenye *National interest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kinachogomba ni lazima tuaminiane. Ifike mahali kama mtu amepewa dhamana ya Waziri wa Fedha, afanye kazi hiyo, tumwamini kwa sababu, tunajua kwamba atafanya *in National interest.* Tukiondoa mamlaka yake kisheria, anakwama na sisi tunakwama. Hilo naomba niliweke wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna dhana nzima ya ukuaji wa uchumi. Tunapongezana kwamba Tanzania ni kati ya nchi zinazokua kwa haraka, lakini mwisho wa siku ukuaji huu ni lazima uonekane pia kwa sura ya fedha za wananchi mifukoni au siyo? Kwa hiyo, sasa hivi wananchi walio wengi nadhani ni halali kusema kwamba hali yao siyo nzuri. Kama yale ninayoyaona Muleba Kusini kule kwangu kwa wale walionituma hapa, kwa kweli hali ni ngumu. Sasa tunafanyaje kusaidia wananchi wetu na wenyewe kuwa na ukwasi wa kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi kusema uchumi unakua, lakini hauonekani mifukoni mwa watu. Kuna njia mbili za kuboresha vipato vya wananchi. Njia moja ni *direct income;* Mheshimiwa Waziri hili analijua, lakini nyingine ni *social income.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unapoleta dhana ya elimu bure, hiyo, ni njia moja ya kuboresha ukwasi wa wananchi, hawana haja tena ya kufanya michango. Sasa zile *direct income* zime-*shrink.* Mheshimiwa Waziri anajua, ni Mchumi, zime-*shrink* kiasi cha kwamba *social incomes* zinakuwa na *impact* kidogo. Kwa hiyo, sasa hivi tuko kwenye shule za msingi, kule kwangu Muleba Kusini watoto wamekuja, lakini hawajanywa uji, hawajapata chakula kwa sababu vipato vya wazazi havitoshi. Kwa hiyo, nataka kusema sasa suala la kuboresha ukwasi kwa kaya ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi zinakua. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri lazima pia ajue kuwa kuna *indirect taxes,* hasa tozo. Kwa mfano, kule kwangu Muleba sasa hivi bado naendelea kusema kwamba huwezi kuwasaidia wananchi kama hawauzi kahawa yao kwa haraka na kwa bei nzuri. Kwa hiyo, bado suala la kahawa ni kizungumkuti na unakuta kwamba sasa mwananchi anakwenda kubebeshwa mzigo wa kulipa madeni ya ushirika ambayo hakuhusika nayo. Hii ni njia moja ya kumdanganya mapato yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kahawa kwa mfano, Sh.400/= zitakwenda kulipia deni ambalo wananchi walikuwa hawahusiki nalo. Namna hiyo, unawanyima yale mapato yao ambayo wangeyapata kama *direct icome.* Kwa hiyo, suala hili la kuboresha ukwasi wa wananchi ni sehemu kubwa ambayo Mheshimiwa Waziri atakapokuja, atuambie mikakati yake na hapo anahitaji wapangaji wake, Wachumi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyo mbele yetu, Kamati imeichambua kwa kweli kwa ufanisi mkubwa, lakini ukiangalia Deni la Taifa lilipofika hapa, naomba niseme kabisa, hii dhana ya kwamba deni ni himilivu, Mheshimiwa Waziri aje atuambie uhimilivu wake wakati linaswaga 49% ya mapato ya ndani. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba fedha nyingi zinapokwenda ku-*service* deni, hapo uhimilivu unaanza kuwa wa mashaka. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri a tuletee mikakati mizuri au majibu

mazuri ya kutufanya *comfortable,* kutupa faraja kujua kwamba hili deni jamani tumejisahau wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaonesha kabisa kwamba uwezo; tunakopa zaidi, tunaendelea kutegemea kukopa, tunakusanya mapato ya ndani lakini yanaenda kwenye matumizi. Maendeleo yatakwama kwa sababu tunakopa na mikopo mingi ni mikopo ya kibiashara. Mheshimiwa Waziri ni lazima mkakati utafutwe kurudi kwenye mikopo ya bei nafuu ikiwemo kutafuta *guarantees* kutafuta ubia katika miradi mikubwa. Hata na Marekani mambo makubwa yamefanywa kwa ubia; *Equity financing* yamefanywa kwa *government guarantees.* Tukienda kichwa kichwa kwamba tunajitegemea, tunaweza kuja kuangukia pua. Nafikiri suala hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku nchi hii imesimama kwenye dhana ya Siasa ni Kilimo katika; katika nchi hii mtu ni afya; hiyo ndiyo miradi ambayo tumeiona. Sasa nimeshangaa sana kuona Mfuko wa Maji nao umepata hatima ya kutokupata fedha zote ambazo tunakusanya ambazo zimepangiwa. Tukisahau maji, tumesahau kila kitu. Maana yake kama nilivyosema, afya; maji ndiyo uhai na afya ni kitu muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyotangazwa hapo awali, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Hafla ya jioni ambapo tunakusanya fedha. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kuweka nguvu sasa katika kuboresha dhana ya usafi katika shule. Nataka niseme kwamba na mtoto wa kiume hatumsahau. Choo bora kinachojengwa kitajengwa pia na kwa watoto wa kiume na wenyewe watakuwa na sehemu yao na mtoto wa kike wana sehemu yao. Kwa hiyo, hili nalo nimeona nilifafanue. Tunamlenga mto wa kike lakini hatutaki kumwacha mwenzake nyuma. Kwa hiyo, tunakwenda pamoja kama tulivyo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekti, nataka kusema kwamba Kamati ya Bajeti imefafanua mambo vizuri na sisi

tunaongezea kama tulivyofanya, lakini hii dhana ya Mfuko Mkuu wa Serikali ni dhana nzuri, lakini kwani lazima imaanishe kwamba fedha zote hata zilizokusanywa na Halmashauri zije kwanza Hazina? Mfuko Mkuu wa Serikali kwangu mimi naona ni *concept.* Mheshimiwa Waziri nadhani anahitaji *concept,* wakati wote kweli Serikali Kuu tunakusanya nini? Siyo fedha zote zije pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwa mchango wako mzuri. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Almas Maige ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti yetu ya Serikali. Kwanza, naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia naomba nimpongeze Mheshimiwa Spika na niwapongeze Chama cha Wabunge Wanawake walioko hapa Bungeni kwa hafla hii ya leo ya kuhakikisha kwamba wanahamasisha wananchi kuchangia tukio hilo la kujenga vyoo vya watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu sasa kwa kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kijaji na Watendaji wote wa Wizara. Pia naipongeza Kamati ya Bajeti ambayo kwa kweli imekuwa ikifanya kazi nzuri sana kuhakikisha bajeti zetu zinakuwa rahisi hata kuzijadili hapa Bungeni. Vile vile bajeti hii ni nzuri sana. Bajeti ambayo ilisomwa tarehe 14 Juni, 2018 ni nzuri sana kwa sababu hata Mwenyekiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mbowe aliipongeza bajeti hii. Kwa hiyo, inaonesha jinsi gani ambavyo bajeti hii imekuwa nzuri. Hata Mbunge wetu wa Iringa alipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inatakiwa sasa Watendaji wajipange kuhakikisha yale mambo ambayo yako katika bajeti wanayafanya vizuri ili kusiwepo na malalamiko. Maana Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia, hasa kwenye bajeti ya Serikali kwa Wizara ya Fedha kulikuwa kuna malalamiko mengi sana hasa kwa upande wa kodi. Kwa hiyo, naomba kabisa Mheshimiwa Dkt. Mpango ahakikishe anasimamia bajeti ili wananchi wetu waweze kutendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naungana na Waheshimiwa Wabunge wote waliopongeza Serikali kwa kuondoa ushuru katika taulo za kike. Tatizo hili kwa kweli limekuwa likisumbua sana watoto wetu wa kike na nafikiri lilizungumziwa sana na Wabunge wengi wanawake na huu ulikuwa mshikamano halisi kwamba wanawake wote ni lazima tuhakikishe kwamba tunaipigania hii kodi. Serikali yetu kwa sababu ni sikivu, naona wameiondoa kodi. Kwa hiyo, nina imani kabisa bei zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niendelee kuipongeza Serikali kwa kuondoa kodi katika mikopo inayotolewa katika Halmashauri zetu, ile 5% ya wanawake na asilimia tano ya vijana. Najua kuondoa kodi kutasaidia sana kuwajengea uwezo hasa wa kifedha akinamama na vijana katika Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba kile kilio kwamba wanakosa mitaji sasa angalau kwa kuondoa ile kodi watakuwa na mitaji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba labda Serikali ingeweka wazi kuhusiana na watu wenye ulemavu, kwa sababu hii 5% ya wanawake na vijana bado haijatamka wazi kuhusiana na watu wenye ulemavu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Manispaa yetu ya Iringa, tayari imetenga 2% kwa kuwakopesha watu wenye ulemavu na vikundi vinne vimepata mikopo ya shilingi milioni tisa. Kwa hiyo, ni jambo zuri. Pengine nchi nzima kungekuwa kuna tengeo la 2% kwa watu wenye ulemavu. Kwa sababu watu wenye ulemavu wamekuwa wakifanya

biashara nzuri tu ambapo kwa kweli hawataki kuomba. Ni watu ambao wanaweza kufanya biashara nzuri kuliko hata watu ambao hawana ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee kuhusiana na kilimo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo. Uchumi wa Viwanda ambao ndio mwelekeo wa Serikali yetu hii ya Awamu ya Tano unategemea sana sana kilimo. Naipongeza Serikali sana kwa kuweka kilimo kama kipaumbele katika bajeti yetu. Pia Azimio la Maputo linasema asilimia 10 ya mapato ya bajeti ya Serikali ni kwa ajili ya kilimo, lakini karibu miaka mitatu sasa hivi, tunaona kilimo bado hakijapewa kipaumbele. Tunaona hata asilimia moja haitengwi kwa ajili ya kilimo. Kwa hiyo, naiomba Serikali yetu, ili sera yetu ya viwanda iweze kwenda vizuri, ni muhimu sana kutoa kipaumbele katika kilimo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali ihamasishe sana wakulima wakubwa waweze kuwekeza katika kilimo. Watakapowekeza katika kilimo maana yake hata ajira pia kwa vijana itapatikana kuhusiana na kilimo kwa wakulima wakubwa kama zilivyo nchi nyingine. Vile vile tuwajengee uwezo wakulima wadogo wadogo na kuwawezesha ili kilimo kiweze kuwasaidia, kwa sababu asilimia kubwa sana ya Watanzania ni wakulima wakiwepo watu wa Mkoa wangu wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali yetu ijitahidi sana kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji, kwa sababu programu zake nyingi sana za umwagiliaji hazijaweza kufanyika vizuri sana katika maeneo mengi. Unaona maeneo mengi yametengwa, lakini bado kilimo cha umwagiliaji hakifanyi vizuri sana. Ninao mfano halisi kabisa hata katika Mkoa wangu wa Iringa, miradi mingi ya umwagiliaji haijaweza kufanya vizuri kuwasaidia wananchi wanaofanya kilimo. Kwa hiyo, naiomba Serikali yetu ihakikishe kwamba programu za umwagiliaji zinapewa kipaumbe kwa sababu zenyewe hata bila mvua bado tutaendelea kupata mazao mazuri ambayo yatasaidia hata katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu Benki ya Kilimo. Nilitegemea Benki ya Kilimo ndiyo ingekuwa mkombozi kwa wakulima, lakini badala yake inafanya biashara ya kukopesha benki. Maneno haya hata siku ile Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli aliyazungumza wakati wa uzinduzi wa *ASDP II*. Sasa niombe Serikali isimamie kuhakikisha Benki ya Kilimo inawafikia wakulima na inawakopesha na wakulima waweze kukopesheka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya ziara kwenye Mkoa wa Iringa kwenye miradi hii ya *SAGCOT.* Tumeona miradi ya *SAGCOT* ni mizuri sana, lakini kuna changamoto nyingi sana katika baadhi ya viwanda tulivyovitembelea. Kwa mfano, kuna suala la vifungashio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda pale *Tanzanice Station* pale Njombe, vifungashio ni tatizo kubwa sana. Vifungashio vinanunuliwa kutoka Kenya, halafu sasa kuna walanguzi wanakuja hapa nchini wanachukua mazao, wanapeleka Kenya kwenda kufungasha. Inaonekana kama mazao ni ya Wakenya wakati ni ya Watanzania. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuwasaidia watu watakaofungua viwanda vya vifungashio ili kuondoa hii changamoto ambayo iko kwa wajasiriamali wetu na wafanyabiashara wengi waliopo nchini ili kusaidia kuongeza kipato kikubwa katika bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda katika kiwanda cha Asasi, tuliona kwamba kimeanza kuwekeza katika vifungashio. Sasa labda kiwezeshwe ili kisaidie kuondoa hii changamoto kubwa ambayo ipo. Kwa sababu pia kuna changamoto tuliona katika Kiwanda cha *Silverland* na hata Asasi kwamba kuna tozo nyingi sana zinatozwa katika viwanda vyetu, karibu tozo 12 na kusababisha sasa hata wenye viwanda wanakata tamaa. Kwa sababu naona kuna tozo nyingine zinafanana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kujumuisha hizi tozo iwe moja ili kusaidia watu wengi sana waweze kuwekeza katika viwanda, itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu miradi ya maji, bado mingi haijakamilika na miundombinu yake bado haifanyi kazi, hata iliyokamilika bado haifanyi vizuri. Sasa ile Sh.50/= naona kama Serikali ingeifanyia kazi. Tunategemea kama tutapitisha hiyo Sh.50/=, naona Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamechangia, ingeweza kusaidia sana katika kuhakikisha kwamba mwanamke tunamtua ndoo ya maji kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu kuhusu miradi ya *PPP.* Hii miradi ni muhimu sana. Tukichukulia tu mfano wa Daraja la Kigamboni; daraja hili sasa hivi tumeweza kujenga kwa kutumia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia mama.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali twende na mpango huu wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nizungumzie kuhusu…

**MWENYEKITI:** Aah, hapana.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *Electronic Tax Stamp*.

**MWENYEKITI:** Hapana, muda wako umekwisha. Kwa heri.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Naomba Watendaji wote waitendee haki bajeti yetu kwa sababu ni bajeti nzuri sana ambayo tunategemea kwamba itatendea haki hata Chama chetu cha Mapinduzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba, Almasi Maige, Mheshimiwa Anastazia James Wambura wajiandae.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyokuwa mbele yetu ya bajeti Kuu. Awali ya yote namshukuru Mwenyenzi Mungu aliyetupa afya na uzima, tumefika asubuhi hii ya leo. Nami pia naipongeza Serikali kupitia Wizara hii ya Fedha, Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mpango, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa utendaji wao nzuri na umakini na usimamizi mzuri katika taasisi hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nami nianze mchango wangu, kama muda utaniruhusu nitachangia mambo matatu. Jambo la kwanza, ni suala la *Export Levy,* kuvuja kwa mapato na lingine ni hili suala la *tax stamp.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa ajili ya *Export Levy* na ikiwezekana, naweza kutumia muda mwingi sana hapa kutokana na hali ninavyoiona na jambo hili tukiliachia liendelee kama hivi, linaweza kugawa Bunge letu, Serikali yetu, Taifa na upotoshaji ukikaa muda mrefu ambao siyo sahihi. Kuhusu *Export Levy* ina historia ndefu tofauti na hapa tunavyoanza kujadili. Sababu hizi ziko za kisheria. Kama unavyofahamu, kazi ya Bunge ni kutunga sheria; Serikali kazi yake ni kusimamia sheria na kutekeleza; na Mahakama ni kutafsiri sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hapa nina *Finance Bill* ya Mwaka 2010 ambayo ndiyo tunafanya *reference* Wabunge wengi, kwamba hizi pesa kama zinaonekana Serikali imeenda kuwapora watu wa Kusini ambao ni pesa zao, walikubali wakatwe kwenye korosho kwa ajili ya maendeleo yao, lakini Serikali hii bila huruma imeenda kuzichukua na kuzipangia matumizi bila kuwashirikisha wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niseme siyo kweli. Kwa mujibu wa *Finance Bill* ya Mwaka 2010 ambayo ninayo hapa, ilitunga Bunge hili. Naweza kununukuu, Sheria Na. 203 ilianza mwaka 1984 lakini marekebisho yake ya mwaka 2002, 2006 mpaka 2010. 17(a) inasema:

"*A person who export raw cashew nut shall pay an export levy to be computed and collected by Tanzania Revenue Authority (TRA) at the rate of fifteen percent of the FOB value.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesitisha. Twende Na. 2 kwenye mgawanyo wake ndiyo kwenye matatizo hapa. Kifungu cha 2 (a) kinasema:

"*Sixty five percent would be divided among district council which are cashew nut producer.*" Asilimia 65 inakwenda kwenye Wilaya zinazozalisha zao la korosho, lakini bado ni hela ya Serikali. Ukisema inakwenda Wilayani, Halmashauri bado ni Serikali. Siyo hela ambayo unasema kwamba imeporwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba (b), "*thirty five percent will be...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgumba, hebu ngoja kidogo. Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mgumba anajua namheshimu sana na ni mara chache sana mimi kusimama kutoa taarifa Mbunge anapozungumza, lakini Mheshimiwa Mgumba ama anazungumza jambo ambalo halifahamu au ameamua kupotosha makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha ambayo ilifanya Marekebisho ya Sheria ya Korosho mwaka 2010. Katika majadiliano yale na Wabunge

kadhaa wa kutoka mikoa ya korosho akiwemo Mzee Mkuchika walikuwepo. Pendekezo la kupeleka fedha asilimia 65 za *Export Levy* halikuwa pendekezo la Serikali, lilikuwa pendekezo la wakfu wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bill* iliyoletwa na Serikali haikuwa na hilo pendekezo. Kwa hiyo, tunaposema asilimia 65 ni fedha za korosho, ni kwa sababu kulikuwa kuna mkutano wa wadau wa korosho, wakapendekeza hivyo; na siyo hivyo tu, wao wenyewe wadau wa korosho...

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa.

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Kwa hiyo, maelezo Mheshimiwa Mgumba anayoyatoa ya *reference* ya *Finance Bill* siyo sahihi. Naomba Mheshimiwa Mgumba aende...

**MWENYEKITI:** Umeeleweka.

Mheshimiwa Mgumba unasemaje kuhusiana na hiyo taarifa?

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndugu yangu Mheshimiwa Zitto anavyoniheshimu, nami namheshimu sana, naye anafahamu hivyo, tunaheshimiana sana, nakubali sana maelezo yake, lakini sizungumzi maneno ya mtaani. Nimesema ninayo *Finance Bill* ya 2010 ndiyo naifanyia *reference* hapa. Hii hapa na nitai-*table* mezani ionekane nani anasema ukweli,. si ndiyo! *Cap. 203* sawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo taarifa yake siipokei kwa sababu mimi naongea mambo ya kisheria. Bahati nzuri, sasa ngoja nieleze kama anavyosema siijui, ni vizuri na Mheshimiwa anajua kabisa kwamba mimi nimeishi kwenye hii. Siongei jambo ambalo silijui siku zote. Nimekaa kwenye korosho miaka 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ilianza mwaka 1984 baada ya zao hili kudorora nchini. Tulifikia uzalishaji wa tani

zaidi ya 174,000, zilishuka mpaka tani 16,000 kwa mwaka. Ndiyo Serikali ya Awamu ya Kwanza ikaamua kuja na mkakati maalum ya kufufua zao hili mwa 1984. Mwaka 1985 ndiyo ikaanzishwa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Korosho *(CBT)* kwa ajili ya uendelezaji na kufufua zao hili. Mwaka 1990 tulianza kubinafsisha mashirika na kuwa-*invite* wafanyabiashara binafsi kutoka duniani kote kuja kushirikiana nao kulifufua na kuliendeleza zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994 Kampuni niliyokuwa nafanyia kazi, *Olam International* ilikuja hapa nchini na ikaanza kununua. Wakati huo *Export Levy* hii haipo, tulikuwa tuna-*export* korosho *zero rated.* Lengo la kufufua hili zao, tuviwezeshe viwanda vyetu 12 alivyojenga Baba wa Taifa mwaka 1978/1979 kwa ajili ya kubangua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikopa mkopo wa *World Bank,* hivyo viwanda 12 vyote vinajulikana, havikubangua hata korosho. Korosho yote ikawa inaenda nje. Ndiyo likaja wazo la kusema ili tu-*discourage* kwa ajili ya usafirishaji ya *raw nut* kwenda nje kufaidisha Mataifa mengine na kuhamishia ajira kule, tuweke *Export Levy*. Ndiyo ikaja *Finance Bill* na kubadilisha sheria mwaka 1996. Ndiyo tuliweka ushuru wa kwanza *Export Levy three percent.* Lengo lilikuwa ni ku-*discourage.*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mhshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa. Kaa kidogo.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ndio naongoza kikao. Nami *history* ya suala hili nalifahamu. Mheshimiwa taarifa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, kwa kweli anayoongea anaudhi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa kwamba kama hilo analolisema ni sahihi kwamba fedha hii inapaswa kuwa ya Serikali kwa asilimia mia moja, iweje leo Serikali wameleta *Finance Bill* kuja kufanya marekebisho ya Fedha ya Tasnia ya Korosho yote ichukuliwe na Serikali, kama Serikali haijui kwamba hiyo fedha inatakiwa iende kwenye zao la korosho kwa ajili ya uendelezaji wa zao la korosho? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgumba, unasemaje kuhusiana na taarifa hiyo?

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani amenipeleka nyumbani. Hili suala la kukusanya pesa zote kwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina haijaanza kwenye korosho. Tulianza *EWURA*, zote zinaenda Hazina, *TCCRA,* zote zinaenda Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala walileta *Finance Bill* hapa, kuondoa kipengele namba mbili (2) kwenye matumizi ya pesa zile, nilisema mwanzoni. Kwa mujibu wa Sheria, asilimia 65 ilipaswa iende kwenye Wilaya zinazozalisha korosho zote, zile za Mtwata na Kusini. *(Kelele)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Naomba nimpe...

**MWENYEKITI:** Hapana Waheshimiwa Wabunge. Hebu Mheshimiwa Cecil Mwambe, kaa.

Waheshimiwa Wabunge, nawasihi tu mwachane na kumpa taarifa hizo, kwa sababu, mbali na Serikali kupitisha mbali na mapendekezo ya Serikali, haya ya Bajeti Kuu, wiki ijayo si itapata uamuzi, tutakuja sasa kwenye Muswada wenyewe ambao mapendekezo haya yapo. Yeye ana haki ya kuelezea kama anavyoona, hata kama amejielekeza kusiko. Nanyi mtakuja kulinyoosha kwa maelezo mtakayoona kwamba ni sahihi.

Ndiyo maana mimi kama *moderator* nimesema nalifahamu sana suala hili, nami nitakuja kutoa mchango

wangu huko mbele ya safari. Kaa tu wewe, hakuna cha taarifa. Mheshimiwa Mgumba endelea, tumekutunzia muda wako.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ukizingatia, unitunzie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1996 ndiyo ikawekwa 3% kwa ajili ya *Export Levy Rate*, bado korosho ikawa inaenda *more than 90 percent* nje. Lengo halijafikia. Ilipofika 2002, Serikali ya Awamu ya Tatu ikaongeza kutoka 3% kwenda 5%, lakini bado korosho ikawa inaenda nje. Ndiyo hapo ulipoanza mgawo. Wakasema kwa sababu lengo kwa kuzuia korosho hizi zisiende nje ni kwa sababu korosho hizi ni chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa tutungie sheria tuzigawanye, sehemu ya asilimia 65, iende kwenye Wilaya zilizochangia zao hili kufika mapato yao, asilimia 35 ziende *CBT* wakati huo mfuko ulikuwa haupo kwa ajili ya kuendeleza zao hili ili tunyanyue uzalishaji. Baadaye uzalishaji ukiwa mkubwa, korosho zitaenda nje na viwanda vyetu vitapata. Bado pamoja na na juhudi zote za Serikali hizo, korosho ilikuwa inaenda zaidi ya asilimia 90 nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipofika mwaka 20…

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, umekiukwa sasa hivi.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68 na Kanuni ya 48 inazungumza kwamba Mbunge anayezungumza hatalizungumza jambo ambalo limeshakuwekewa utaratibu wa Kibunge. Hoja hii ya Korosho tayari kwenye *Finance Bill* inayokuja, hoja hii itajadiliwa. Sasa Mbunge huyu anavyoendelea kuzungumza jambo ambalo liko kwenye utaratibu wa kujadiliwa, anavunja utaratibu na hajatangaza maslahi ya jambo hili.

**MWENYEKITI:** Amesema yeye amewahi kufanya kazi, amesema, nimemsikiliza, Mheshimiwa endelea.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mchango mwingine mkubwa zaidi zaidi ya huu. Nimekuja kwa sababu lilianza kujadiliwa humu ndani kabla yangu. Sasa tukiacha jambo hilo likae kama lilivyo, umma kule wanaamini walichoongea ni sahihi. Ndiyo maana nimekuja na historia kwanza. Watu wanafikiria tu 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala lilianza 2002, ndiyo mgawo kwa mara ya kwanza ukaanza kuwekwa. Kabla ya hapo ilikuwa inakusanywa. Wakasema asilimia 65 iende kwenye Wilaya, asilimia 35 kwenye *CBT* kwa ajili ya kuendeleza. Tulipofika 2010, ikaonekana bado korosho zinaondoka nje. Ndiyo ikaja kuongezwa kutoka asilimia 10 iliyoongezwa 2006 kuja asilimia 15 ya sasa. Pamoja na hayo, kwa sababu lengo kubwa ilikuwa ni ku-*discourage exportation* ya *raw*, lakini bado korosho zinakwenda wakasema...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Nilikataa taarifa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Hiyo asilimia 65 katika Wilaya zilikwenda?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wako una dakika moja tu. Una dakika moja tu Mheshimiwa.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo mfuko ambao ulianzishwa kwa ajili ya 2009 na 2010 baada ya sheria kutungwa kwa ajili ya kusimamia *addition value* na ku-*procces* hizo korosho hapa nchini, ukafeli na ukawa na matumizi mabovu sana ya pesa. Sasa...

**MBUNGE FULANI:** *(Aliongea nje ya microphone)*

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Subiri. Huo ndiyo upotoshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa baada ya ...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgumba. Ahsante sana. Tunaendelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, naomba msitumie lugha ya mitaani. Mheshimiwa Bungara nakuheshimu sana. Nakuomba sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Ester Mahawe, ajiandae. Hapana, Mheshimiwa Oran Njeza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hamna haki ya kuniongoza mimi. *(Kicheko)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniruhusu nami nichangie hotuba hii ya Bajeti ya Mapendekezo ya Serikali kuhusu Mapato na Matumizi yake kwa mwaka huu wa 2018/2019. Kabla ya kuanza kuchangia, nami nina utangulizi kidogo. Kwa muda mrefu sana tumekuwa tunapata lawama upande huu. Wenzetu upande wa barabara ya pili kule, wanaongea na kutusema kila tunapomsifu Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli, kwa mambo mazuri anayoyafanya kwamba wamefanya nchi siyo yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote viongozi wote wa nchi na viongozi wa Taasisi wanapata sifa zinazofanya na Taasisi zao kwa niaba ya Taasisi hizo. Tumekuwa na Viongozi kama Mheshimiwa Baba wa Taifa, Mheshimiwa Kwame Nkhuruma, Mheshimiwa Mao wa Uchina na wengine wote wamekuwa wanapata sifa za nchi zao za matendo

yao kutokana na yale wanayoifanyia nchi. Pia kumekuwa na sifa mbaya, viongozi wanapata sifa mbaya ya matendo yao, kama vile sisi tulivyovamiwa na Iddi Amin. Yeye hakuchukua hata bunduki, waliotuvamia ni Askari wake, lakini lawama akapata yeye. Kwa hiyo, wenzetu upande wa pili wa barabara hii ya kuingilia Bungeni watuache tuendelee kumsifia Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa matendo yake, kwa sababu ndiyo sifa zake zilizomvaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya utangulizi huo, naomba niwashukuru sana na niwapongeze Mawaziri hawa wawili, Mdogo wangu Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mdogo wangu Mheshimiwa Dkt. Kijaji kwa kazi kubwa waliyoifanya kuandaa mpango huu wa Bajeti ya mwaka huu wa 2018/2019. Hawa ni Wachumi, wameonesha kwamba wamesomea kazi hii ya uchumi na ndiyo maana wanaitwa Madaktari wa Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti yako hii, yako mambo mengi kwa manufaa ya wananchi. Hii ni bajeti ya wananchi kwa mara ya kwanza. Serikali ya Awamu ya Tano imeleta Bajeti ambayo sisi Sekta Binafsi tunaiunga mkono; watu wote Viwandani, wanaiunga mkono. Tangu tumeanza kuleta Bajeti hapa Bungeni, tangu nimeingia Bungeni, hakuna Waziri yeyote aliyeleta Mpango wa kusamehe madeni yanayotokana na riba za madeni ya wanaodaiwa na *VAT*. Hawa wameleta mfano mzuri sana, kwamba sisi, wale ambao tunadaiwa; mimi pia nadaiwa na *VAT,* naomba ku-*declare interest.* Nimefurahi sana na sio mimi tu na wafanyabiashara wote, Mheshimiwa Dkt. Mpango, tutalipa madeni hayo kwa kipindi cha miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, bajeti hii imekuja na mapendekezo ya kusamehe ile kilichokuwa kinaitwa zamani kodi ya makampuni ya asilimia 30 na kwenda asilimia 20 kwa baadhi ya makampuni hasa yanayoanzishwa. Pia tumeona kwenye ngozi; na muhimu kabisa tumeona hata taulo za akinamama zimefikiriwa na ilikuwa adha kubwa sana na bei kubwa kwa watu kupata taulo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninayo machache ya kusemea kama changamoto. Jambo la kwanza ni elimu. Elimu tumeona hapa Mzaramo, rafiki yangu Waziri wa TAMISEMI, ameongelea kwamba wanafunzi waliochaguliwa kwenda sekondari ni asilimia 75,000, lakini bahati mbaya sana wanaopata nafasi, wanabakia wanafunzi wengine 25,000 hawana pa kwenda. Kwa hiyo, njia pekee aliyopendekeza, tujenge madarasa ili tuweze ku-*accommodate* wanafunzi hawa kwa mwezi wa Nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mie nakuja na pendekezo lingine na naomba lifanyiwe kazi, linaweza likasaidia. Kwa nini tusiingie *PPP* na shule za watu binafsi ambazo zina miundombinu tayari, lakini tutoe hela ile ile ambayo ni *unit cost ya* kila mwanafunzi kwa mwaka huu waende kwenye shule zile wakati tunaandaa shule zetu, ziwe tayari kwa ajili ya *intake* ya mwaka kesho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PPP* inawezekana tunaiongelea ipo kwenye sera yetu; tuitumie kwa mara ya kwanza kwenye elimu, tupeleke wanafunzi hao kwa kuwalipia *cost* ile ile. Bahati mbaya au nzuri nimefanya *research*. Ziko shule nyingine za binafsi, *cost unit* ya mwanafunzi mmoja ni rahisi kuliko *cost unit* ya wanafunzi wanaolipiwa katika Shule za Sekondari za Serikali au za Upili. Napendekeza basi, Serikali ifikirie *PPP* na shule binafsi ambazo zitafanyiwa uchunguzi kwamba zinafaa, zinatoa mafunzo sawasawa na za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la pili ambalo pia ni muhimu kuliongolea, nalo ni Elimu ya Ufundi. Nimekuwa nasimama hapa mara kwa mara kwa maana mimi ni zao la Shule za Ufundi, lakini bahati mbaya Serikali inaongolea Sera ya Viwanda, lakini mafundi sadifu, nina maana *technicians* wa kuendesha viwanda hivyo hawapo, kwa sababu Shule za Ufundi hazitoshi na Vyuo vya Ufundi kipo kimoja tu cha *DIT.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mingi imepita, Serikali sasa ione umuhimu wa kuandaa chuo kingine ili kuzalisha

mafundi sadifu *(technicians)* wengi badala ya kukazania *VETA* ambao wanatoa *Artisans,* ni kiwango cha chini cha Elimu ya Ufundi. Mafundi watakaoendesha mitambo hii viwandani wanatakiwa wawe na *level* ya *FTC (Full Technical Certificate)* au mafundi sadifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu atakapokuja ku-*wind-up* hii bajeti atuelezee mpango wa kuanzisha shule za ufundi; na ningependekeza shule za ufundi za Kata ili kwenye Kata kuanzishwe chimbuko la mafundi watakaoendesha ufundi wa viwanda vidogo vidogo huko kwenye kata na majimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la Kiswahili. Kiswahili chimbuko lake ni hapa Tanzania, lakini hakuna sheria yoyote inayosema Kiswahili ni Lugha ya Taifa wala hakuna *GN* yoyote inayosema Kiswahili ni Lugha ya Taifa. Wenzetu Kenya wameitia ndani ya Katiba ya Kenya, kwamba Kiswahili ni Lugha ya Taifa. Sisi tulikuwa tunaandika hapa Katiba, ile Katiba inayopendekezwa, tuliweka suala hilomle; lakini wakati huu wa ombwe la Katiba Mpya, kwa nini Serikali isije hata na *GN* tu ili watu waongee Kiswahili badala ya kuongea lugha ambayo haieleweki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa Kiswahili imekuwa kitendawili mashuleni. Watoto wanasoma Shule za Msingi, mpaka darasa la saba Kiswahili. Wakifika Shule ya Upili, wanaanza kufundishwa Kiingereza, hawaelewi masomo, hawaelewi lugha. Nchi zote ambazo zimeendelea; Ufaransa, Uingereza, Marekani, Ufilipino na China wote wanafundisha kwa lugha ya kwao ambayo inayoeleweka. Hivi mwanafunzi akifundishwa Kiswahili, Serikali inaona tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu inasema lugha ya kufundishia Shule za Upili na Shule za Utatu, ni Kiingereza, lakini huu ni Ukoloni. Nchi zote zote zilizojikomboa katika elimu zinafundisha kwa lugha zao. Naomba sana

Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind* hili ili suala la mambo yanayohusu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, aongelee Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala lingine ambalo linaleta gharama kubwa sana katika Bajeti ya Mambo ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Suala la nyumba za Mabalozi wetu; tumekuwa tunapanga nyumba kwa gharama; na asilimia 75 ya gharama zote za Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni pango za Balozi zetu; Ofisi na nyumba za wafanyakazi. Kwa nini tusiendeleze mpango uliokuwepo wa kujenga majengo ya Mabalozi wetu na nyumba za Makazi? Hata kama tutachukua miaka 10, lakini tutaweza kujenga nyumba hizo ili ziweze kuondoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Wambura, Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Mahawe wajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Bajeti ya Serikali. Nianze tu kwa kusema kwamba nami nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika Taifa letu; Watanzania wanajua na Mataifa mengi ya dunia hii yanajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hata sisi Waheshimiwa Wabunge, tunafanya kazi nyingi katika Majimbo yetu kwa kuhamasisha tu, kwa kuibana Serikali, lakini wakati mwingine kwa kuhamasisha wananchi, zinajengwa Hospitali, zinajengwa shule, lakini barabara pia

zinajengwa na pale wananchi wanatusifia na kutupongeza na kusema Mbunge fulani katujengea barabara, katujengea shule, katujengea hospitali; wakati huo huo pesa hizo zimetoka Serikalini. Sijawahi kusikia Mbunge hata mmoja akikataa wasimpongeze. Nadhani tunakubaliana na hilo. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango pamoja Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi Nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara yao. Vile vile nawapongeza kwa kutengeneza hotuba nzuri sana ya Bajeti ambayo inagusa maslahi ya Watanzania wote kwa ujumla. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, kuna baadhi yetu tunasema kwamba Bajeti hii ni hewa kutokana na kwamba tumeweka malengo makubwa na hatukuitekeleza kwa asilimia 100. Namwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake na timu yote nzima, wakaze buti, tusonge mbele. Kwa sababu wanafalsafa wanasema hivi: *"most people fail, not because they aim to high and miss, it is because they aim too low and heat."* Tusonge mbele Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ukienda ukurasa 23 hadi wa 25 wa kitabu cha Bajeti utaona mafanikio ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018 na mafanikio hayo yanatokana na matumizi ya kiasi cha fedha zaidi ya shilingi trilioni nne na zaidi na kati ya hizo, utakuta zaidi ya asilimia 25 yametumika kulipia malimbikizo ya madeni ya watumishi wa Umma, Wakandarasi, pamoja na Wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana kwa sababu hili tatizo lilikuwa limeendelea kwa miaka mingi na hii ni ishara nzuri na ni mwanzo mzuri sana kwamba sasa tutakuwa tunapambana na malimbikizo ya madeni. Naomba tuendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani zangu kwa Serikali kulipa fedha za Mkandarasi ambaye alikuwa anatekeleza Mradi wa *Mkwiti Group Water supply Scheme* alikuwa akidai *advance* ya shilingi bilioni 400 lakini amelipwa zaidi ya bilioni 300 na hivyo itamwezesha kuendelea na mradi wa maji katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba suala la kutatua tatizo la maji katika Halmashauri ya Tandahimba limepewa kipaumbele na kwa kweli wananchi wa Tandahimba wanashukuru sana, kwa sababu Wilaya hii ya Tandahimba ina watu zaidi ya laki 243 na tatizo la maji ni kwamba upatikanaji wa maji ni asilimia 24 tu katika vijiji, ambacho ni kiasi kidogo sana, iko chini sana na ile *average* ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Wizara ya Maji ielekeze nguvu zaidi katika eneo hili kwa sababu mwaka jana walikuwa wamepangiwa bajeti bilioni 2.3 na kwa sasa wanaomba Mkandarasi huyu apewe bilioni moja kwa ajili ya *certificate* ili kusudi aweze kumaliza ile *phase one (I)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri pia inaomba wapewe kibali cha kuendelea *phase II* na *phase III* ambayo inatarajiwa kutoa huduma kwa takribani wananchi elfu 36 ambao ni asilimia 14, kwa hiyo ukichanganya na zile 24 tutaweza kufikia asilimia 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana wadau wa sekta ya maji tusimamie vizuri miradi yetu ya maji kwa sababu Kamati ya *LAAC* tumetembelea katika maeneo mbalimbali. Katika Halmashauri mbili ambazo tumezitembelea na tulikuwa tumeambiwa kwamba miradi hii imekamika na inatumika, Halmashauri zote mbili miradi haitumiki. Kwa hiyo ni tatizo, tunaweza tukawa tunaitupia Serikali lawama lakini pia Watendaji wanaonesha kutukwamisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na nipongeze sana Serikali kuweka kipaumbele katika sekta ya

kilimo. Sekta ya Kilimo ni muhimu, lakini ndani ya sekta ya kilimo kuna suala la lishe na ukiangalia malengo la maendeleo endelevu *(SDG),* lengo namba mbili ni kipaumbele katika masuala ya lishe. Kwa hiyo, niombe Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ishirikiane na taasisi mbalimbali au Sekta mbalimbali sekta ya afya, uvuvi, kilimo yenyewe, fedha, elimu, viwanda ili kusudi tuweze kuipa kipaumbele sekta ya lishe au masuala ya lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo eneo la nishati, tumeona katika kurasa hizo za hotuba ya Mheshimiwa Waziri 23 – 25 kwamba kuna bilioni zaidi ya 400 zimeenda katika kuendeleza Sekta ya Nishati, lakini kuna tatizo moja ambalo naliona kwamba kiasi cha bilioni 400 haziakisi sana matatizo ya kukatikakatika kwa umeme. Tatizo hili ni kubwa na hasa tunapokwenda na sera yetu ya Tanzania ya viwanda tatizo hili linaweza likawa ni kikwazo kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana kwanza niwapongeze sana Waziri na Naibu wake wanafanya kazi nzuri sana katika sekta hii, wanajitahidi sana. Kila unapowaambia tatizo lolote wana-*respond* haraka na ni kwa dakika chache sana tatizo linakuwa limetatuliwa ila ninachoona *TANESCO* haina Watendaji wazuri. Baadhi ya Watendaji wa *TANESCO* kwa kweli wanatukwamisha. Kwa hiyo wapitie vizuri utendaji wa watumishi wa *TANESCO*. (*Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Wambura. Tunaendelea.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana. Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia katika hii Wizara yetu muhimu ya Fedha. Nianze kwa kuipongeza Wizara, Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, lakini pamoja na Wataalam wote, wanafanya kazi vizuri sana. Pia napenda niipongeze Serikali kwa ujumla kwa niaba ya wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambalo ndiyo Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kweli utekelezaji wa bajeti iliyopita ilikuwa nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya pamoja na kutengewa bilioni moja na nusu kwa ajili hospitali ya Wilaya lakini tuna vituo vya afya vitatu vinavyoendelea na tuko kwenye hatua ya umaliziaji sasa hili. Kuna Kituo cha Afya cha Ilembo, Santilia pamoja na Ikukwa. Tuko vizuri na tunaendelea vizuri tunategemea nafikiri kama kwa kazi hii Serikali itaendelea kutupa pesa zaidi kwa ajili ya kumalizia zaidi ya vituo 50 vya zahanati zetu ambazo ziko katika hatua nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye barabara nako Serikali kwa kweli imefanya vizuri kwenye Halmashauri yangu. Kuna barabara nyingi ambazo zimejengwa pamoja na jiografia yetu ambayo ina changamoto nyingi, lakini tunaishukuru Serikali kwa sababu mpaka sasa hivi kuna utekelezaji wa barabara za lami za kilomita 27 ambazo zimetoka kwenye barabara tulikuwa na barabara zenye kilomita mbili tu, sasa kuongezewa mpaka 27 kwa kweli inabidi tuishukuru Serikali. Pamoja na hiyo tuna kilomita kama 47 ambazo ni za barabara ya mchepuko. Tunaiomba sasa Serikali ikamilishe hizo barabara kwa haraka mno kwa sababu zinapita maeneo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye umeme Serikali imefanya vizuri kwenye Halmashauri yangu, kwenye elimu nayo tunashukuru sana tumepewa pesa kwa ajili ya miundombinu ya shule za msingi na shule za sekondari naishukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye maji napenda nimshukuru kwa kipekee Waziri wa Maji amefanya kazi kubwa sana. Tulikuwa na changamoto za utekelezaji lakini mpaka sasa hivi kuna miradi mingi ya maji ambayo inaendelea. Kwenye Mji Mdogo wa Mbalizi sasa hivi tumeunganishwa na Jiji, kwa hiyo tuna uhakika wa kupata maji namwomba Waziri ahakikishe kuwa asije akatuangusha. Sasa hivi tunaenda kiangazi tuhakikishe maji yanamwagika Mbalizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kwenye mradi wa Mbawi Jojo, mradi wa Haporoto Itimu, Haporoto Idimi, Izumbwe Iwindi, Horongo Itimu Mwampalala, Shongo, Igale, Swaya na Rupeta pamoja na Mshewe Muvwa, Njelenje Mapogoro na Mjele. Hii ni miradi muhimu namwomba sana Mheshimiwa Waziri aikamilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye bajeti ya mwaka huu, wenzangu wameongelea sana kipaumbele ukiangalia namba moja ni kilimo. Ukiangalia Serikali imetenga kiasi gani kwenye kilimo huwezi kuziona. Nilikuwa najaribu kuangalia bajeti ya Kenya kwa sababu katika vitu vingine hivi lazima tujilinganishe linganishe. Wenzetu wa Kenya wamefanya nini? Wana vipaumbele vinne katika kipaumbele kimojawapo ni hifadhi ya chakula hawajaita kilimo. Wametenga nini kwenye hifadhi ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *dash board* ya bajeti ya Kenya. Kwenye kilimo hifadhi ya chakula *(food reserve)* wametenga bilioni 32; kwenye nafaka wametenga bilioni 43; kwenye nafaka tena wametenga bilioni 20; kwenye umwagiliaji wametenga bilioni 192; na kwenye *subsidy* ya mbolea wametenga bilioni 97. Kwa jumla kwenye kilimo wametenga bilioni 409. Sasa hizo ukiangalia kwenye bajeti ya Waziri huwezi kuziona mara moja zimefichwa wapi. Tungeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ili wananchi wajue ni namna gani wakulima tunawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinaenda pamoja na miundombinu. Tuna tatizo sana la usafirishaji wa mbolea.

Leo hii kupeleka mbolea Mbeya kwa tani ni Sh.90,000 mpaka Sh.120,000. *TAZARA quotation* yao ni laki moja na ishirini kwa tani, lakini barabara ni elfu tisini kwa tani. Sasa unajaribu kuangalia kwa nini kuna tatizo hili. Ukija kwenye Reli ya Kati mpaka Tabora ni elfu sabini lakini kwa barabara ni zaidi ya laki moja na ishirini. Ningeomba sana Serikali ingechukua jukumu ni namna gani tuiboreshe *TAZARA* ili tuweze kuwakomboa wakulima. Tukipunguza bei ya mbolea tutakuwa tunamsaidia mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nafikiri limeongelewa kwa kiasi kikubwa na wenzangu waliotangulia ni suala la hii akaunti ya *Treasury Single Account*. Ningependa kupendekeza kwa Serikali ingeangalia kwa uangalifu sana, hizi hatua inazozichukua wakati mwingine zinaweza kutupeleka mahali pabaya. Kwa sababu ukichukua pesa zote za Halmashauri benki ambazo zimefungua matawi zitabakiwa na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iangalie *NMB*, *CRDB*, na *NBC*, pesa nyingi ambazo wanazo kwenye Halmashauri zetu kule, kwenye Wilaya zetu ni pesa za Serikali. Ukizikusanya zote hizi unazipeleka Benki Kuu na Benki Kuu ni kwa ajili shughuli za benki siyo *retail banking*. Shughuli za Benki Kuu ni Benki kwa Serikali na Benki wa Mabenki, hata wenzetu waliochukua hatua za kufungua hii *Treasury Single Account* hawakwenda kwenye Halmashauri, kwa sababu imegundulika kuwa katika hizo nchi kulikuwa na *abuse* kubwa sana, kulikuwa na ubadhirifu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na madhumuni ya hii *Tresuary Single Account* ni kwa ajili ya ukwasi *liquidity, cash management* siyo kwa ajili ya *financial control,* kwa sababu huwezi ukahamisha *responsibility* za Maafisa Masuuli kuzipeleka kwa Waziri wa Fedha. Hii Wizara watashindwa kui-*manage*. Waziri ali-*make reference* nyingi tu, ningependa vilevile aende kumsoma mtu mmoja anaitwa ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Utapata nafasi tu ya kuyaeleza vizuri hayo. Tunaendelea Mheshimiwa Ester Mahawe, atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi ninapenda kukushukuru kwa ajili ya kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya bajeti. Pia napenda kupongeza juhudi zinazoendelea kufanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli pamoja na Wizara hii ya Fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu Waziri wake wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua tumesikia sana humu ndani watu wakisema bajeti hii ni hewa ama bajeti ya tangu mwaka 2016 ni hewa. Sasa nashangaa sijui hawa ndugu zetu wanaishi nchi gani ambako hawaoni maendeleo makubwa anayoendelea kufanyika ndani ya nchi hii. Wenzangu wamesema tumeona mengi bajeti ya Wizara ya Afya imekwenda juu sasa hivi mpaka madawa yana-*expire* hayana watumiaji kule kwenye hospitali zetu, lakini bado watu wanasema bajeti ni hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kupongeza sana Wizara ya Fedha kwa kuweza kuondoa tozo ya *VAT* katika taulo za watoto wetu wa kike. Kimekuwa ni kilio cha Wabunge wanawake na Wabunge wanaume ndani ya Bunge hili kwa ajili ya watoto wetu ambao mara nyingi wamekuwa wakikosa shule kwa takribani siku 70 ndani siku zile zote za kusoma. Hili siyo jambo dogo, tunaishukuru sana Wizara hii na Serikali kwa ujumla, Mungu awabariki sana kwa jambo hili jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka kwa mtoto wa kike naomba nielekee kwa akinamama ambao muda mwingi wamekuwa wakitafuta maji na muda wao mwingi ukiwa

umepotelea kwenye suala zima la kusaka maji vijijini. Wabunge wenzangu wamezungumza suala la tozo ya Sh.50 kwenye mafuta, nami naomba niungane nao ya kwamba tuweze kutoza hiyo Sh.50 na kuweza kuongeza kwenye bajeti ya maji ili kuweza kumtua mwanamke ndoo kama ambavyo Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya 2015/2020 inasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba jambo lingine lolote katika maisha kwa mfano hata umeme unaweza ukawa ni *option,* lakini maji hayana mbadala. Kwa hiyo niiombe sana Wizara hii ya Maji iweze kupatiwa fedha na zaidi sana ipate hii Sh.50 ili kwamba akinamama waweze kuondokana na adha kubwa ya utafutaji wa maji na huku muda wao mwingi ukipotelea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumze suala la kutokupelekwa kwa fedha kwenye Halmashauri zetu mbalimbali nchini kwa wakati, pia fedha hizo zimekuwa hazipelekwi tu kwamba kwa wakati. Hii imekuwa ikiathiri hata ile asilimia 10 ya wanawake na vijana kwa kiwango kikubwa kwa sababu yale makusanyo ya ndani ambayo ndiyo yanapaswa kutoa asilimia 10 yamekuwa hayafanikiwi kwa kiwango kikubwa kwa sababu Wakurugenzi wetu wanaishia kutumia hizo fedha kwa ajili ya kukidhi matakwa na mahitaji mbalimbali katika Halmashauri zao kwa sababu ya kukosa fedha zile ambazo zinatakiwa kutoka Serikali Kuu kurudi kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali itazame hili kwa jicho pana kidogo ili kwamba fedha hizo kama ambavyo tulizungumza huku nyuma kwamba siyo ni za kihuruma huruma bali zipo kisheria ziweze kuwafikia wanawake na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hapa tumekuwa tukipendekeza katika Bunge hili kwamba kuna kundi maalum la walemavu. Hili kundi limesahaulika. Bado imeonekana asilimia tano vijana, asilimia tano akinamama, lakini bado naendelewa kushauri kama ambavyo iliwahi kushauriwa

hapa tutenge asilimia mbili katika hizo 10 ziende kwa walemavu. Hili ni kundi maalum. Mtu anaweza akawa na ulemavu wa kiungo kimojawapo lakini akawezeshwa na bado akaweza kufanya biashara ama kazi ambayo inaweza ikamfanya yeye na familia yake wakapata maisha. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kundi hili lizingatiwe la walemavu katika zile asilimia tano za vijana itolewe hapo asilimia moja na kwa akinamama itolewe asilimia moja zipelekwe kwa kundi hili rasmi la walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Waziri tumeona jinsi ambavyo amekuja na miradi ya kielelezo kama *Stiegler's Gorge* mradi ambao kwa sehemu kubwa pia umekuwa ukibezwa. Niseme kama tulivyosema tunaelekea kwenye Serikali ya viwanda ama uchumi wa viwanda hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda pasipokuwa na umeme toshelevu. Kwa hiyo, naunga mkono hoja suala zima la huu umeme wa *Stiegler's* ili kwamba tuweze kupata viwanda vya kutosha na hatimaye tuondoke katika umaskini na kuingia katika uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Waziri amekuja na *Tax Amnesty* kwa maana ya kwamba zimeondolewa riba katika madeni ya wafanyabiashara wengi wanaodaiwa, lakini muda uliotolewa nina wasiwasi kwamba hautoshi. Huu muda wa miezi sita kwa vile hawa watu wako hapa hapa nchini na hawaendi mahali popote na hawatoroki na Wazungu wanasema *the payment delayed is interest saved,* kwa nini basi Waziri asitazame namna gani wanaweza haidhuru hata miezi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wamepewa muda mfupi wa miezi sita hii inaweza ikasababisha hawa wafanyabishara wakakimbia tena benki kwenda kukopa kwa riba ya juu ili kuweza kulipa haya madeni waliyopewa muda wa miezi sita. Hii inaweza ikaathiri *working capital* yao. Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Waziri atazame namna gani anaweza akaangalia tena kwa mara nyingine, namna gani anaweza akaongeza huu muda kwani madeni haya yatakapolipwa bado uchumi wetu utaendelea kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote niwaombe tena wafanyakazi wa *TRA* wanapodai kodi waweze kuwa *friendly* na wale watu wanaowadai kodi. Tunajua kodi ni jukumu la kila Mtanzania na bila kodi nchi yetu haiwezi kwenda lakini haidhuru waweze kuwa na lugha rafiki na nina hakika Watanzania ni watu waungwana na waelewa watalipa tu hizo kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kumekuwa pia na changamoto kubwa kwenye suala zima la kilimo. Tumeona bajeti ya kilimo ya mwaka 2017/2018, ilikuwa imetengewa takribani bilioni 150, lakini sana kwa mwaka huu tumeona imeshushwa kwa asilimia 34.7 nini kimetokea. Huku tunazungumza uchumi wa viwanda. Viwanda vyetu vinategemea *raw material* kutoka sehemu kubwa ya wakulima kwa maana ya kwamba nchi hii ina wakulima asilimia zaidi ya 65 ama asilimia 66. Sasa kama bajeti hii imeshuka kwa kiwango hiki kama hatutaweka nguvu kubwa kwenye suala zima la kilimo tunatoa wapi malighafi ya kupeleka katika viwanda vyetu? Kwa hiyo, naomba sana Wizara itazame namna gani itaondoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Mahawe.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwami Zitto Kabwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Suleiman Yussuf na Mheshimiwa Cecil Mwambe ajiandae.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti hii ya Serikali, hii ni mara yangu ya kwanza nachangia mjadala wa bajeti toka mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningependa kushauri kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni kwamba mfumo wetu wa Bunge ni mfumo wa Kamati. Kamati za Bunge zinafanya kazi kwa niaba ya Wabunge wote. Kwa hiyo taarifa ambayo Kamati za Bunge zinaleta ndani ya Bunge, ndiyo taarifa ambazo zimefanyiwa kazi na kwa niaba ya Wabunge na Kamati husika. Kwa hiyo ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge kuwashauri tu kwamba turejee sana kazi ambazo wenzetu wamefanya kwa niaba yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kwamba panapokuwa na jambo ambalo unaona kundi la Wabunge wenzako wana mashaka nalo, jitahidi sana kuwaelewa kwa sababu humu Bungeni tunategemeana. Leo hii ukija humu Bungeni ukaanza kuwa-*counter* Wabunge wa kutoka mikoa inayolima korosho, kesho utakuwa na jambo lako hutapata mtu wa kukuunga mkono, hiyo ndiyo *Parliamentary Politics*. *Parliamentary Politics* ni Wabunge kushirikiana. Kama unaona mwenzako ana jambo hulipendi, busara inakwambia kaa kimya usiwapinge wenzako, kwa sababu wao ndiyo ambao wana-*feel the pinch* ya jambo ambalo linakuwa limetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo naenda kwenye korosho moja kwa moja. Ukurasa wa 43 wa Kitabu cha Kamati ya Bajeti, kimeeleza wasiwasi wake kutokana na mapendekezo ambayo Serikali inaleta kuhusu kuweka fedha za kutoka kwenye mazao kuziingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilikumbushe Bunge mwaka huu 2017/2018, kama siyo korosho na *transit goods* kwenye *forex* tungekuwa na dola inakwenda mpaka kwa Sh.4,000. Korosho na *transit goods* ndiyo zimetusaidia kuingiza mapato ya fedha za kigeni, kwa sababu mazao mengine yote mapato yameporomoka. Pamba mapato yameporomoka ya fedha za kigeni, kahawa mapato yameporomoka na mazao mengine kama jinsi ambavyo Kamati ya Bajeti imeweza kueleza. Kwa hiyo, korosho ni zao

ambalo limetuokoa, limeingiza dola za Kimarekani milioni 514 mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana tutazame nini kimesaidia korosho kuongeza uzalishaji na mauzo nje. Ni maamuzi tuliyoyafanya mwaka 2010 ya *export levy* asilimia 65 kwenda kuendeleza zao la korosho. Sasa hivi Serikali inataka kuchukua fedha hizo, itakuwa ni makosa makubwa sana kwa sababu unaenda kumshughulikia mtu anayefanya vizuri. Katika hali ya kawaida ilitakiwa Serikali ilete pendekezo asilimia 100 ya *export levy* iende kwenye korosho kwa sababu Mikoa inayolima korosho imeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi la kuzingatia hapa na ambalo Wabunge wa Mikoa ya Kusini wamelieleza vizuri sana ni kwamba fedha ambayo imetengwa kisheria wameichukua hawajairudisha, hawajaitekeleza sheria inavyotaka, halafu badala ya kulipa kwanza hizo fedha ndiyo waje na mapendekezo mapya, wanakuja na mapendekezo ya kuchukua na zingine zitakazokuja *forever*, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi hapa. Shilingi Bilioni 755 fedha ambazo ziko *ring fenced,* ambazo zina matumizi maalum ya kisheria, Wizara ya Fedha haijazipeleka kule ambako kunatakiwa. Kawaida hapa tayari sheria imevunjwa! Sasa Serikali inapata wapi *moral authority* ya kuja na hoja ya kwamba sasa hizi hela zote sasa ziende Mfuko Mkuu wa Hazina, ni makosa makubwa sana ambayo tunakwenda kuyafanya, nami naungana mkono na taarifa ya Kamati ya Bajeti kwamba suala hili lisitekelezwe kama jinsi ambavyo linapendekezwa na Serikali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni *Treasury Single Account*. Kwanza niseme kwamba wazo lenyewe siyo baya. Ni vizuri tuelewane hapo, wazo la *Treasury Single Account* si wazo baya, kwa sababu nimeenda kusoma kwenye taarifa za *IMF* na nitampatia nakala Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kuna *working paper No*. 10/143 iliyoandikwa na Sailendra

Pattanayak nzuri sana inaeleza hili, lakini haielezi namna ambavyo Serikali yetu inataka kulifanya. Serikali yetu inataka fedha yote iingie Mfuko Mkuu wa Hazina na Serikali yetu inatuambia jambo hili ni la Jumuiya ya Afrika Mashariki, siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetazama *protocol* zote ambazo tumesaini za Jumuiya ya Afrika Mashariki hakuna jambo hilo. Jambo hili ungeliona Afrika Mashariki kama tungekuwa tunaanza kutekeleza *monetary union*. Hatujaletewa hapa Bungeni *protocol* ya *monetary union*. Kwa hiyo, hoja ambayo Serikali iliileta kwamba hili jambo ni la Afrika Mashariki ilikuwa ni hoja ya kutushawishi tu, lakini siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo hoja ni kweli Serikali ituletee hapa ni *protocol* ipi hiyo ya Afrika Mashariki ambayo inasema jambo hilo, siyo kweli! *East Africa* imetoa vigezo vya namna ya kuingia kwenye *monetary union,* ikiwemo nakisi ya bajeti na kadhalika, haijasema mtunzeje fedha zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zingine wanachokifanya hawasemi hela zote ziingie kwenye akaunti moja ya Benki Kuu au ya *reserve bank* na kadhalika. Wanachokifanya wanajenga *system* ambayo Hazina na Benki Kuu watajua pale Bariadi kuna *balance cash* kiasi gani siku ile wakati *business day* imefungwa. Kwa hiyo Serikali itajua kama ni *cash management* Serikali itajua Bariadi Halmashauri ina hiki, sijui Itilima Halmashauri ina hiki, Misungwi ina hiki, Kigoma ina hiki, lakini kilicholetwa na Serikali ni kwamba Kigoma tukikusanya tupeleke Benki Kuu, siyo sahihi! Kwa hiyo, nadhani Wizara ya Fedha ilitazame hili. Siyo jambo baya, hatuwapingi, liandaliwe vizuri na tulifanye kwa mazingira yetu ya Tanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hili jambo la *stamp* za *electronic*, msingi wa hoja siyo mbaya kwa sababu unaenda kudhibiti mapato, lakini tunatekeleza namna gani, lazima tulitekeleze kwa namna ambayo hatupeleki ushuru

kwa wananchi kinyemela. Kwa sababu kwa mazingira ambavyo lipo sasa hivi gharama kwa wananchi zitaongezeka. Waziri Mpango ametusomea hapa kwamba bidhaa za ndani soda, bia nini hazijaongezewa kodi, lakini ukitekeleza tu hii *electronic stamp* zinaongezeka kodi na baadhi ya bidhaa zitaongezeka kodi mpaka Sh.90 kama maji, soda na kadhalika. Kwa hiyo hatusemi kwamba ni jambo baya, liandaliwe utaratibu ambao likitekelezwa wananchi hawatapata madhara ambayo wanakwenda kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine mawili ya mwisho ambayo nitaenda kuchangia, Kamati ya Bajeti imezungumza kuhusu kodi, ushuru wa mafuta kwa ajili ya maji. Waheshimiwa Wabunge tulizungumza hapa wakati wa Wizara ya Maji na kuna *consensus* ya ndani ya Bunge kwamba tuongeze fedha kwenye ushuru, fedha Sh.50 ili tupate fedha za kutatua kero za maji kwa wananchi wetu, hakuna Mbunge ambaye hakuliunga mkono hili. Serikali haijaja na hilo wazo. Kamati ya Bajeti imependekeza kwamba Sheria ya *Road and Fuel Tolls Act* ibadilishwe tulete fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha namwelewa ana wasiwasi wa masuala ya mfumuko wa bei na kadhalika, lakini namshauri Waziri wa Fedha akaangalie takwimu zake vizuri Dkt. Mpango. Ukiangalia mara ya mwisho tumepandisha ushuru huu kisawasawa ni mwaka 2007. Ushuru huu mwaka 2007 kwa dola *(in dollar terms)* ilikuwa ni senti za dola 0.42, leo ushuru huu kwa senti za dola leo 2018 ni senti za dola 0.34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hali ya kawaida *in real terms* utakuwa umefanya marekebisho ya ushuru na katika hali ya kawaida Mheshimiwa Waziri wa Fedha ushuru ungepaswa kupanda kwa Sh.160. Kamati ya Bajeti inaomba Sh.50 tu lakini ushuru unaweza ukapanda mpaka Sh.160 bila kuathiri mfumuko wa bei, kwa sababu tutakuwa tunafanya *rationalization* na *exchange rate* kwa sababu hayo mafuta tunayanunua kwa

dola. Kwa hiyo ni sahihi kabisa kuhakikisha ya kwamba tuna-*relate* huo ushuru kutokana na *dollar terms*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu, Waziri ametueleza hapa kwamba kipaumbele ni kilimo. Kilimo hakijatengewa fedha za kutosha, umwagiliaji haujatengewa fedha za kutosha. Ukifanya 160 Mheshimiwa Dkt. Mpango, akisema Sh.60 ziende kwenye umwagiliaji unapata shilingi bilioni 190 ambazo hata kwa ambao tunataka michikichi watu wanaoleta mafuta ghafi wameongeza kodi ili tuweze kuzalisha hayo mawese kwa ndani, si tunahitaji uwezekezaji, hela hii hapa kwa ajili ya kuja kuwekeza. Watu wa alizeti hela hiyo hapo kwa ajili ya kuja kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza katika *Road and Fuel Act* tufanye marekebisho hayo tuendane na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti na tunaweza tukaenda mpaka Sh.160 tukapata fedha za umwagiliaji, nchi ikajitegemea kwa mafuta ya kula ya kutosha ndani ya muda mfupi ambao unatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa, kuna makosa tuliyafanya mwaka 2016/2017, lazima tukiri. Matatizo ya kibajeti tuliyonayo sasa hivi, matatizo ya ukwasi wa fedha tuliyonayo sasa hivi ni *measures* tulizozifanya kwenye bajeti ya kwanza ya mwaka 2016/2017. Lazima tuanze kurekebisha, tulipandisha bajeti kwa *thirty one percent (31%)* ndiyo maana leo bajeti hii tunaijadili hapa ukilinganisha na mwaka jana imepanda kwa asilimia mbili tu ili kurekebisha makosa ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kosa tulilofanya mwaka ule ni kodi kwenye huduma za utalii. Kasi yetu ya kuongeza wageni wa utalii ilikuwa *twelve percent (12%)* kabla ya kuongeza hii kodi. Leo hii kasi yetu ni asilimia tatu. Nataka niwaambie jamani sasa hivi ukicheza na utalii, ukicheza na *transit goods,* Bandari ya Dar es Salaam na ukicheza na korosho ya kina Mzee Mkuchika shilingi itafika Sh.5000 au Sh.6000 kwa dola, sababu haya ndiyo maeneo yanayotupa *forex* sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba ile kodi ya ile *VAT* kwenye *tourism services* iondolewe. Pili sasa hivi kwenye mapendekezo haya kwenye kukodisha ndege pia tumeweka *VAT* tena. Tumeleta mapendekezo kwenye *Finance Bill* ya sasa hivi, namwomba Mheshimiwa Waziri aitazame. Kwa kweli kama tukisimamia vizuri na ikiboreshwa iwe *electronic stamp* tutapata fedha za kuziba haya maeneo. Napendekeza maeneo hayo yaweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango kuhusu mambo mengine nimepeleka kwa maandishi na tutajadiliana zaidi kwenye *Finance Bill* wakati wa mjadala kuweza kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwami Zitto Kabwe kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhannahu Wataalah* aliyeniweka hai mpaka leo nimefunga Ramadhani, nimemaliza sita, kwa hivyo leo ni sikukuu kwangu *Alhamdulillah*. Pili namswalia *Mtume Muhammad (Swalallah alayh wasalaam).*

**MWENYEKITI:** Hongera sana.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sana nitakuwa ni mtu mwenye kushangaa shangaa lakini wewe usishangae. Jambo la kwanza ambalo linanishangaza sana ni kuangalia pande mbili za Muungano baina ya Zanzibar na Tanganyika kwa upande mmoja, lakini upande wa pili tuangalie Zanzibar na nchi zote za Afrika Mashariki huo ni upande wa pili. Kipi cha kuangalia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tumeshuhudia kwamba bajeti za nchi za Afrika Mashariki zimesomwa siku ya Alhamis tarehe 14 Juni, 2018, lakini Bajeti ya Zanzibar imesomwa juzi tarehe 20/6/2018 hii ni kwa sababu gani? Je, Zanzibar haimo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki au vipi? Kwa nini Zanzibar inabaguliwa kiasi chote hiki. Sababu tunaijua, sababu ni kwamba kwanza ni lazima Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa upande wake awasilishe Wizara yake ijulikane marekebisho ya kikodi ndiyo baada ya hapo Zanzibar nayo waige, wafuate mfumo ule. Kwa hivyo, haiwezekani kabisa kabisa kwa Zanzibar kusoma bajeti siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi ni kwamba kwa kawaida Bara huwa wanaunda vikosi kazi vya kushughulikia mambo ya kikodi na mambo ya kibajeti. Wakishamaliza wenyewe kwa wenyewe ndiyo wanaalika wadau kwa jumla waje na wao watoe maoni yao ikiwemo Zanzibar inaalikwa kama mwalikwa wa kawaida tu na siyo kama mshiriki wa Muungano. Ni kwa nini Zanzibar inafanyiwa hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka atakapokuja Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini Zanzibar isishirikishwe katika vikosi kazi badala yake ibaguliwe kiasi kikubwa namna hiyo. Kwa sababu kama tunakumbuka mwaka 1985, Zanzibar na Bara walipitisha bajeti siku moja. Bara wakashusha kodi, Zanzibar wakapandisha ikalazimu Zanzibar iitake Bara ilipe tofauti na ikalipa tofauti. Je, wanataka tuendelee na hali hiyo? Hakuna haja, tushirikiane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Serikali iliunda Akaunti ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa Ibara ya 133 ya Katiba kupitia Sheria Na. 15 ya mwaka 1984 ili kila upande usimamie uchumi wake na masuala ya Muungano pia yasimamiwe na shughuli za Muungano. Ni miaka 34 tokea Tume hii ilipoundwa mpaka leo hii nilijibiwa wiki mbili zilizopita na Waziri wa Fedha kwamba akaunti hii haijafunguliwa miaka 34. Waziri atakapokuja jambo la kwanza atuambie hii akaunti itafunguliwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linatuonesha ni vipi Serikali ya Muungano ilivyokuwa haina nia njema kwa Zanzibar, kabisa. Serikali ya Muungano haina nia njema kwa Zanzibar kwa sababu kwa kuunda Tume hii au kwa kuunda akaunti hii matatizo mengi sana ya kifedha, ya kikodi yangelikuwa yametatuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uwoga huo wa Serikali tumeshindwa kuelewa mambo mengi sana kwa mfano, hivi sasa hatujui mahitaji halisi ya Muungano ni kiasi gani, matumizi ya Muungano hatujui ni kiasi gani, hatujui mchango wa kila upande katika Muungano ni kiasi gani, pia hatujui hata kodi zipi ni za Muungano, kodi zipi siyo za Muungano, nia njema haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *study* iliyofanywa na *PriceWaterHouseCoopers* imeonesha kuwa vyanzo vya mapato vyenye vinasaba vya Muungano kwamba vyanzo hivyo vinatosha kabisa kuendesha Muungano kwa mambo ambayo ni ya Muungano. Pia pande mbili za muungano zikabakiwa na vyanzo vya kutosha kwa ajili ya kujiendesha kila upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya mfuko huo mpaka leo hii haujaanzishwa na wala nia haipo, tunaambiwa tu kwamba majadiliano yanaendelea. Miaka 34 majadiliano hayajakamilika, hebu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango atuambie tumpe miaka hamsini na ngapi tena ili akaunti hii ya pamoja ianzishwe. Nataka kusema kwamba kama wanataka kujua kero za Muungano, basi hii ni kero mama katika kero za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa kweli nashangaa tena na napata mashaka makubwa sana juu ya nia ya Tanganyika kwa Zanzibar. Najiuliza ni faida zipi hasa za kiuchumi ambazo Zanzibar zinapata kutokana na Muungano huu kwa sababu jambo lolote ambalo ni la Zanzibar, Bara halitakiwi. Sukari ya Zanzibar imekataliwa, ukileta bidhaa kutoka Zanzibar tunaambiwa kwamba tulipie

kama vile bidhaa inatoka Dubai. Jamani huu Muungano uko wapi? Muungano uko wapi ndugu zangu nataka kulijua hilo mnieleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha sana hata lile ambalo ni haki ya Zanzibar, hatupewi, kwa mfano katika suala la uajiri ni asilimia 79 Bara, asilimia 21 Zanzibar, hata hili halijatekelezwa mpaka leo hii, lini tuambie litatekelezwa suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote yenye maslahi na Zanzibar basi tunanyang'anywa. Leo hii tumeambiwa kwamba usajili wa meli tunataka kunyang'anywa, jamani! Mnatutakia nini Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumze kidogo tu Kisiwa cha Fungu Mbaraka au kinaitwa *Latham Island*. *Latham Island* imepandishwa bendera ya Zanzibar pale tarehe 19 Oktoba, 1898, tokea wakati huo kisiwa hiki ni milki ya Zanzibar na hata siku moja bara haijawahi kusema kwamba ni chao, lakini waliposikia pale kwamba kuna *block* ya mafuta wamekuja mbio kwamba hiki kisiwa ni chetu. Nawa-*challenge* Mawaziri wote waliopo hapa waje hapa watuambie ni lini Bara imemiliki Kisiwa cha *Latham Island,* wote nawa-challenge waje hapa waniambie, lini wamekimiliki kisiwa hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bara zipo fursa nyingi sana. Tanzania Bara kuna madini, mbuga za wanyama, kilimo, mifugo na gesi, Zanzibar hakuna chochote lakini inapotokea tundu moja tu kidogo kwamba kuna heri inataka kuja haraka wanakwenda kuiziba, tukiuliza jamani kulikoni, wanatuambia atakayeuchezea Muungano tutapambana naye kwa thamani yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako, hiyo ya *Latham Island* tutakuja kuonana nje hapo baadaye.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe kulingana na muda Mheshimiwa Kanyasu ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze na kuwakumbusha Watanzania wote Waislam kwa Wakristo tusome Luka 8:18. Luka 8:18 inaelezea juu ya mambo ya mali, aliyenacho ataongezewa na yule asiyekuwa nacho hata kile kidogo ambacho anahisi anacho na chenyewe atanyang'anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maana sana kusema maneno haya ya utangulizi wa kwenye Biblia kwa sababu ni wazi kabisa sasa hivi Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo inaongoza nchi hii imeamua kusimama kwenye huu mstari Luka 8:18 na nina mifano ya kuhalalisha kwa nini nimeamua kusema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti ya Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mpango kule ndani hakuna sehemu ambako amekwenda kuonesha kwamba watumishi wote wa kada zote watakwenda kuongezewa mishahara yao. Pamoja na kukamilisha masuala ya uhakiki na walisema kwamba baada ya uhakiki mara moja watakwenda kuboresha mishahara. Juzi hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu amesimama anasema suala la nyongeza ya mishahara itabaki kuwa siri, itafanywa kimya kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize bei za mazao na bidhaa nyingine zinapanda, tumeona kabisa kwamba hata kwenye shule ada zinapanda, lakini watumishi wao hawaongezewi mishahara wakiwemo na watumishi wa Bunge wanaotusaidia hapa ndani mishahara yao haipandishwi sasa hivi kwa mwaka wa pili au wa tatu kwa kisingizo cha uhakiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya kabisa wale wachache ambao walikuwa wanatakiwa kupandishiwa mishahara yao walipewa barua za kupandishiwa madaraja wakiwemo Polisi na Wanajeshi. Ukienda Jeshi la Zima Moto ni kilio, wamenyanga'anywa ile mikataba yao ya mwanzo, wiki mbili tatu zilizopita wakati tunakuja kwenye Bunge la Bajeti wamepewa barua nyingine wanaambiwa vile vyeo vyao vya awali vimesahaulika wanaanza kuhesabiwa toka juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Rais anashangaa, anamwambia hapa Mama Jenista Mhagama kwamba eti anahisi anaajiri vilaza ndiyo maana watu hawafanyi kazi vizuri huko mtaani, hapana na sidhani kama alimjibu. Nataka leo nimwelekeze amwambie Rais hawa watu wamekuwa *demotivated* kwa sababu hawapati stahiki na mishahara yao, hawafanyi kazi kwa moyo kama ambavyo ikuwa zamani, hili ndiyo tatizo pekee lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa mama Jenista kama inawezekana awasiliane na Rais amweleze kwamba hawa watu wamekuwa *demotivated* wanataka wapandishwe vyeo na mishahara ili waweze kufanya vizuri. Kuna watumishi wa umma wengi wamebaki kwenye vilio sasa, Walimu na wengi waliobakia wanasikiliza Bunge ili tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu yetu ya awali kama Wabunge yalikuwa ni kuisimamia, kuielekeza na kuishauri Serikali, lakini hapa tumeona sasa hivi mtindo huku ndani na hasa zaidi ndugu zetu wa Chama cha Mapinduzi wanavunja sana Kanuni ya 154. Hii kanuni ya 154 inaruhusu kabisa kutoa pongezi za aina yoyote, anayetakiwa kufanya jambo hili kwa niaba ya wote Wabunge ni Mheshimiwa anayekuwepo kwenye Kiti siku hiyo pale. Sasa imekuwa kama utamaduni ili uweze kuonekana utaanza kumsifia Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani wakati sijawa Mbunge nilifikiri hili jambo linakwendaje; unanisifia wee halafu mwishoni unaanza kumwambia lakini hata hivyo rekebisha hii. Twendeni kwenye *point* tuisimamie na tuishauri Serikali na ndiyo liwe lengo letu wote. Wote tunatamani kupongeza lakini wasiopongeza wanaonekana wabaya kwa sababu wengine wanapongeza na ndiyo tumefikia hapo, hii ni *double standard. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa pia niongee leo ni masuala machache kwa ajili tu ya kuishauri kama ambavyo nimeanza toka mwanzo. Nimenukuu hapa Luka 8:18 na ndiko walikosimama Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Twende kwenye gesi Mtwara, mpaka sasa hivi gesi ya Mtwara inatumika kwa asilimia saba tu, wale Wawekezaji wa *Maurel and Prom* wamekuja kulalamika kwamba wao wanashindwa hata kurudisha mtaji wao kwa sababu gesi ile haitumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeruka imeachana na gesi ambayo ingekwenda kuwanufaisha watu wa Mtwara, wamekimbilia kufanya mradi wa *Stiegler's Gorge* ambao thamani yake halisi mpaka utakapokuja kukamilika haifahamiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna nia ya kupinga huu mradi lakini kwa nini tusikamilishe miradi iliyopo mwanzoni ya kimaendeleo inayoweza kusaidia ili mambo mengine yafanyike. Hiyo pesa inayokwenda *Stiegler's Gorge* ingekwenda kutumika kusaidia kwenye miradi ya maji, kujenga zahanati na kufanya shughuli zingine tukaokoa maisha ya watu wetu tukaongeza *life span*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la reli *(Standard Gauge).* Reli ya Tanzania kulikuwa kuna reli inaitwa Reli ya Kusini ilikuwa inaanzia Mtwara inapita Newala, inakwenda Masasi inanyooka kwenda kule chini. Hii reli ingekuwepo mpaka sasa hivi ingetusaidia kudumisha au

kupata chuma cha kujenga hiyo reli ya *standard gauge* hapo katikati, kwa sababu Mchuchuma na Liganga uwekezaji wake sasa hivi ungekuwa umeshakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeachana na hiyo, tunatumia *forex* nyingi kununua chuma kwa ajili ya kutengeneza reli na tunasema hapo tuna miradi mingine ya kimkakati, huko *Stiegler's Gorge* tunakoongelea inatakiwa na kwenyewe ipelekwe chuma, kwa nini Serikali isifikirie kutengeneza Mchuchuma kwanza kwa hizo pesa zote tena kwa haraka tupate chuma yetu wenyewe, nyingine tuiuze nje na nyingine tutumie kwenye miradi yetu ya kipaumbele. Matokeo yake wao wanaamua kuingiza tu *(import)* ndiyo maana shilingi inashuka kila siku, hii ni biashara ya kawaida kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hapa ambalo kwa kweli hili kwetu ndiyo lenyewe. Hapa nina makaratasi mengi tu na Mheshimiwa Omary Mgumba nimwombe kabisa atuombe radhi watu wa Mtwara kwa sababu Mgumba kilichomleta Mtwara ilikuwa ni biashara ya korosho, walikuwa wanafanya kazi na kampuni moja inaitwa *Olam* Tanzania *Limited*, hawa ndiyo walikuwa watu wanaowafanya watu wa Mtwara waendelee kubaki vile wanavyobaki kwenye korosho kwa sababu walikuwa wanajua wananufaika na nini. Ndiyo maana anakuja kutetea, anawatetea ambao walikuwa waajiri wake na hao ndiyo waliotufikisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya *export levy* ipo hapa ndani, karatasi hizi ninazo na hizi karatasi nitaku... *(Makofi)*

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe hebu kaa, naona taarifa huko.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa kwanza nilitangaza mwanzoni nilisema nimefanya kazi kwenye kampuni ya *Olam* Tanzania *Limited* miaka 19. Sasa hivi hicho kiwanda kilikuwa kinabangua korosho zaidi ya tani 30,000, kimeshahama kipo Mozambique. Kwa hiyo, sina maslahi yoyote tangu nimeingia Ubunge siyo mfanyakazi wa *Olam,* mimi ni Mwakilishi wa wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini muda wangu umeutunza. Nataka tu nikwambie wakati tukiwa Wabunge wageni kabisa mwaka juzi, Mheshimiwa alinikutanisha na Meneja Mkuu wa *Olam* duniani, sijui alimtoa wapi tukakutana hapo nje, sasa ndiyo anaoendelea kuwatetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya *export levy* ninayo hapa na nitampa pale Waziri, nataka nisome tu mistari michache nikueleze. Wanasema hivi changamoto hii ilipata utatuzi kupitia maazimio yaliyofikiwa katika mkutano wa wadau wa korosho uliofanyika tarehe 12 mpaka 14 Aprili, 1994, Mkoani Mtwara katika Wilaya ya Masasi. Mkutano huu pamoja na mambo mengine uliazimia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa walisema kuweka mikakati ya kuwa na utafiti endelevu wa zao la korosho. Pia kuwa na usimamizi wa uratibu mzuri wa tasnia ya korosho nchini; kuongeza uzalishaji wa zao la korosho kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora na kuendeleza ubanguaji wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Serikali inakuja hapa pesa zetu sisi tunadai ili tukafanye mambo haya... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwaka gani huo?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mwaka ambao?

**MWENYEKITI:** Mwaka gani?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unajua mimi nilikuwa nani kipindi hicho?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** *Attorney General*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwa *Attorney General,* kwa hiyo naamini kabisa unafahamu na ndiyo maana ulisema historia hii unaifahamu. Ahsante sana Mheshimiwa Chenge kwa kunisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya tafiti ambazo zipo, nilimshauri mwaka jana hapa Waziri wa Viwanda kwamba tunaomba tufanye utafiti na jana tumekaa hapa na wadau wanaozalisha pombe na vitu vingine wanalalamika upatikanaji wa *alcohol*. Nilikwambia mabaki yanayobaki kwenye korosho na ndiyo maazimio yao pale ikiwemo pamoja na zile kitu kwetu tunaita *kochoko* inapatikana kule ndani *nipah*, ukiamua kuitengeneza vizuri unapata *ethanol, methanol* na vitu vingine mle ndani ili kuwaongezea wakulima wale kipato. Huu utafiti ulikuwa unafanyika Naliendele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za kuondoa hiyo *export levy* ya kwanza kabisa inasema upotevu mkubwa wa idadi ya mikorosho nchini Tanzania. Hapa karibuni tumeona Serikali inawasisitiza mikoa mingine waanze kulima korosho wakimemo Tumbi, Mkuranga Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Dodoma Mpwapwa, Tabora, Singida na mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niwaambie Watanzania hawa ambao wanaingizwa huu mkenge, zao la korosho sisi ndiyo limetufanya wakazi wa Mikoa ya Kusini tuwe maskini, lakini tulikuwa tunavumilia, tukagundua kwamba tunahitaji pesa ili tuweze kuliendeleza. Serikali ya

Chama cha Mapinduzi inakwenda kutoa mtaji wetu wa kuendeleza zao hili, sasa wanataka kuingiza mkenge Watanzania wasiohusika na jambo hili. Hili jambo ni la Wamakonde watuachie wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hili tunalosema, wazee wetu akina Mzee Nandonde wakati huo walikuwa wanaomba Kusini basi tutengwe na Tanzania iliyobaki ambayo tunafikiri maendeleo yao yanakwenda kwa kasi, tuishie kuna sehemu moja hapo panaitwa Kinyonga, Kilwa. Kule tunajitosheleza, tuna gesi na korosho zetu tutajua wenyewe namna ya kujiendesha pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pesa ya *export levy* ilikuwa na mgawanyo wake maalum ambao upo kisheria, asilimia 35 inakwenda Serikalini na asilimia 65 ilikuwa na matumizi yake, karatasi hii hapa inayoonesha matumizi mbalimbali ya pesa hiyo asilimia 65, mpaka sasa hivi Serikali wametoa bilioni 10 katika bilioni 211 tunazoidai Serikali hii. Tunataka Mheshimiwa Dkt. Mpango akija pale atueleze hiyo *balance* inayobakia yote wamepeleka wapi na kufanyia nini wakati wenyewe tunaumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tunakoelekea sasa ni kubaya na ndiyo maana hapa juzi Mheshimiwa Bwege alisema tunakwenda kuandamana na tunakwenda kuandamana kweli. Nitaongoza maandamano Jimbo la Ndanda la kudai haki na stahiki yetu kwa sababu tunadhulumiwa na tunaonewa. Kila kidogo tunachojaribu kukikusanya kwa nguvu zetu Serikali inakwenda inapora, wanaleta sheria hapa wanataka watudhulumu. Basi kwanza walete pesa tuliyonayo, halafu baada ya hapo wao walete huo utaratibu wao wa kutaka kubadilisha hii sheria ili tuone mwisho wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *document* nitaipa hapo Kamati yako. Kati ya mambo ambayo yatakwenda kufeli huko mbele ni pamoja na taasisi itapoteza wafanyakazi Watafiti waliobobea kwenye utafiti wa zao la korosho.

Tanzania ambako tunazalisha maeneo mengi, kati ya hao watafiti pale Naliendele Chuoni wameajiriwa wafanyakazi 126 kati ya hao wafanyakazi 71 wameajiriwa kwenye programu ya utafiti wa korosho ambapo mishahara yao inatokana na *cashewnut levy. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu hapa Mheshimiwa Mgumba anakuja anasimama anataka kutetea wanaomtuma anataka kutuaminisha kwamba... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe. Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba pia nitumie nafasi hii ingawa Mheshimiwa Mwambe amesema tusipongeze lakini niipongeze sana Serikali yangu kwa kuendelea kutekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ili uvuke uende Geita lazima upite Busisi na juzi tumeona uzinduzi wa kivuko kipya ambacho kitakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuchukua abiria wengi na magari na ni njia hiyo pekee ambayo kwa kutokea Mwanza naweza kufika Jimboni. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kutimiza ahadi yake hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niiombe Serikali walikuwa wanafanya *feasibility study* nadhani kwa ajili ya kujenga daraja kwenye eneo lile ambalo litapunguza sana vifo visivyo vya lazima ambavyo vinatokea wakati unasubiri *ferry* kwenda Bugando kwa sababu ndiyo hospitali pekee ya rufaa, kama upembuzi yakinifu ule umekamilika basi nimwombe sana Waziri wa Fedha kwamba wananchi wa Kanda ya Ziwa hasa wananchi wa Geita na Mikoa mingine wanasubiri kwa hamu kuona ujenzi wa daraja lile unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri juzi amesema ameondoa kodi ya *VAT* kwenye taulo za kike, nampongeza sana kwa sababu ilikuwa ni ombi la kwetu wenyewe Wabunge. Wasiwasi wangu tu nataka aje anisaidie punguzo hili la *VAT* wamefanya utafiti litapunguza bei kwa kiwango gani kwa watumiaji. Nafahamu kwamba hizi *exemptions* mara nyingi mwisho wa siku zinawafaidisha zaidi wafanyabiashara na siyo watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Kamati kwenye suala la maji, mwaka jana na mwaka juzi tulipendekeza kwamba iongezeke Sh.50 ili tutunishe Mfuko huu wa Maji na hatimaye tuongeze uwezo wa Serikali kwenye kuhudumia miradi ya maji. Kwa hiyo, nimwombe mwaka ule alikataa lakini mwaka huu na dalili ilivyo na kwa sababu tumemaliza mwaka mmoja na nusu kwenda kwenye uchaguzi nadhani sasa anafahamu kwamba bila kufanya hivyo suala hilo litakuwa gumu sana kutekeleza na kwa sababu ni Ilani yetu wenyewe ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye suala lenyewe la hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Hapa karibuni baadhi ya wachangiaji wameonesha sana wasiwasi wa kwamba bajeti yetu Tanzania ni ndogo kulingana na nchi ya jirani kwa mfano Kenya ambao bajeti yao ni dola bilioni 30 na nimeona Uganda wenyewe wana kama dola bilioni 8.5 lakini imeongezeka kwa asilimia 15, Tanzania imeongezeka kwa asilimia mbili. Nadhani sababu ya Waziri kutokuongeza bajeti kama alivyokuwa anafanya miaka ya nyuma ni kutokana na *tax base* yetu kuwa ndogo na *tax base* yetu imekuwa ndogo siyo kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana nami kwamba Waziri wa Biashara anahangaika sana kuvutia wawekezaji waje, lengo lake ni kuongeza *tax base* ili Waziri Mpango aweze kukusanya kodi. Waziri wa Madini anahangaika kutengeneza sheria ili kuwarasimisha wachimbaji wadogo wadogo lakini kuhakikisha kwamba migodi yote inaweza sasa kulipa kodi ili kuongeza *tax base*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata tabu sana kama Serikali inakwenda kwa kufikiri pamoja. Wakati Wizara hii inahangaika sana kuboresha *tax base* unashangaa kuona Wizara nyingine inatumia sheria na kanuni kuhakikisha kwamba wafanyabiashara ambao wapo wanaendelea kulipa kodi wanafilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mfano kwenye uvuvi, nimeangalia hapa kwenye taarifa ya Kamati, uvuvi umetengewa 0.06. Hivi ninavyozungumza tumepata taarifa hapa kutoka kwa Mheshimiwa anayeshughulika na uvuvi na mifugo kwamba amekusanya takribani bilioni nane kwenye faini na kodi mbalimbali kwa wavuvi haramu, lakini anasema amekuja kugundua asilimia 98 ya wavuvi wote Tanzania ni wavuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba ameondoa walipa kodi asilimia 98 kwenye mfumo wa kulipa kodi ambao Mheshimiwa Dkt. Mpango alikuwa anakusanya kodi wote ni wavuvi haramu, amewaondoa kwenye mfumo bila kuja na mpango wowote wa kuhakikisha kwamba hiyo *tax base* anairudishia. Madhara yake ni kwamba tunaotoka kwenye maeneo ya uvuvi kabla ya Watanzania wengi kuingia ziwani kuvua samaki, wavuvi pekee walikuwa ni wale wenye viwanda na wenye viwanda walipewa kazi na Serikali ya kuwawezesha Watanzania kununua nyavu hizi ambazo ziliruhusiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waletaji wa nyavu wakalipa kodi, wakawakopesha Watanzania na wale Watanzania wakanunua wakaweka dhamana nyumba zao, nyavu ambazo zote ni haramu, zimekamatwa zote zimechomwa moto. Hawa wenye viwanda ambao leo hawawezi kuwakopesha tena Watanzania waliokuwa wanavua samaki na wale wote waliokuwa wanavua samaki hawana mitaji, maana yake ni kwamba hatuwezi tena kukusanya kodi lakini tumeua hiyo *industry* ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sishangai ninapomwona Waziri anaposema samaki wamekuwa wengi ziwani, ni kwa

sababu anasahau *there is no more industrial fishing* tena kwa sababu asilimia 98 ya wavuvi waliokuwa mle ziwani ni wavuvi haramu kwa tafsiri yake, kwa nyavu alizopokea na alizoziruhusu yeye kuingia ziwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni mmoja, tunalalamika kwamba bajeti yetu ni ndogo lakini ukiangalia *system* nzima haifanyi kazi pamoja. Nilitarajia kwa kuwa kanuni hizi ni za Waziri na kanuni zinazomwongoza kufanya kazi hii amezitunga yeye, Sheria ya Uvuvi iko vizuri sana. Kwa kuwa nyavu hizi zililipiwa kodi na kwa kuwa tunahitaji *industry* ya uvuvi iendelee kuwepo ili tupate kodi, nimeangalia kwenye kwenye kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango makusanyo yote haya kwa miezi minne sasa ukienda Mwanza hayapo, angefanya mpango maalum wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na *transition period* kabla ya kuanza kuchukua hatua ambazo zinaondoa walipa kodi, karibu asilimia 30 ya walipa kodi wa Kanda ya Ziwa ni Wavuvi wote wanaondoka kwenye mfumo na wakirudi kukopa wataanza kulipa *interest* na *interest* ina gharama kwenye kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba tunapotengeneza *tax base,* ukiangalia sasa hivi mwaka huu tumeshindwa kuongeza kwenye *projection* yetu ni kwa sababu *tax base* yetu ni ndogo. Tulikurupuka miaka fulani tukawa tunaongeza kila mwaka matokeo yake hatujawahi kukusanya kwa asilimia 100. Sasa kama tunatengeneza *tax base* leo kesho tunaibomoa, unaitengeneza kesho, kesho unaibomoa maana yake ni kwamba tunarudi nyuma badala ya kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona juzi kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi amegundua kwamba operesheni ili iweze kufanikiwa sasa ni lazima twende kwa walaji na walaji ni kwenye hoteli na anatumia *regulations* hizo ambazo ni za uvuvi. Tatizo kubwa ambalo naliona, mimi nadhani Watanzania wengi hawajui kwamba *source* ya samaki siyo Ziwa Victoria peke yake, *regulation* iliyopo inazungumzia samaki wa Ziwa Victoria, sato na sangara lakini kuna watu wanafuga samaki, ambao

hawafugi kwa masharti kwamba ili awavune lazima wafikie sentimita ambazo yeye anazitaka. *Cost* yake ya ku-*run* lile bwawa huwezi kusubiri mpaka samaki akae miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki wa Mtera na Nyumba ya Mungu hawafanani na sato walioko Ziwa Victoria. Kwa nini Waziri akili yake anafikiri tu kwamba lazima hawa watakuwa ni kutoka Ziwa Victoria halafu ukikutana na sato *species* 50...

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukisema hapa ni kwamba unaweza ukaletewa sampuli ya sato 10 lakini wale sato 10 ni *species* tofauti, hawafanani na kadri wanavyotofautiana hawakui kwa kufanana. Kwa nini Waziri anakimbilia kwenda... kwa sababu kadri unavyochukua hatua una-*demoralize* watu wote wanaoshughulika na ile biashara una *erode tax base*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kanyasu kwa mchango na ushauri wako kwa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, tumejitahidi kuvuta mpaka hapo kwa asubuhi ya leo, bado tuna wachangiaji tutapata tu nafasi. Kwa vile wachangiaji wa leo mnajifahamu sihitaji nitaje majina nani ataanza, nini ndiyo...

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wataje.

**MWENYEKITI:** Wewe wahi tu ndiyo haki yangu. Waheshimiwa Wabunge tunaenda kwa uwiano na ndiyo maana...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Basi siwataji. Waheshimiwa Wabunge sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi alasiri. *(Kicheko)*

*(Saa 7. 00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Wakati tunasitisha Bunge sikutaja tutakaoanza nao, kwa hiyo naanza na Mheshimiwa Pascal Haonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Kiza Mayeye ajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba sasa nami niweze kuchangia Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja ya kwanza ambayo wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameigusia kidogo nami naomba nianze nayo hiyo, kuhusu hii bajeti ya mwaka 2018/2019 ambayo naona kwangu imepuuza sana maslahi ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa umma katika Taifa hili tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano imeingia madarakani bajeti zake zote, kuanzia bajeti ya mwaka 2015/2016 ambayo ilikuwa bajeti ya kwanza, bajeti ya 2016/2017, bajeti ya 2017/2018 ambayo ndiyo inaisha siku chache zijazo, imepuuza maslahi ya watumishi wa umma. Hakuna nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma. Mishahara ambayo watumishi wa umma wanapokea kwa mara ya mwisho iliongezwa mwaka 2014, ni mishahara ambayo Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliiacha hadi

watumishi wa umma wanapokea mishahara hiyo, hapajawahi kuwa na nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba gharama za maisha zinazidi kupanda, zinazidi kuongezeka. Mwaka 2015 ukiuliza bei ya sukari ilikuwa shilingi ngapi ilikuwa bei ya chini Sh.2,000, lakini leo maeneo mengine hadi zaidi ya shilingi elfu tatu na kitu. Huku ni kuwakosea sana watumishi wa umma kwa sababu gharama za maisha zinaongezeka lakini mishahara yao ni ileile ambayo Awamu ya Nne iliiacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti haijapunguza kodi kwa watumishi wa umma. Tulitegemea kwamba bajeti hii ingekuwa ni msaada kwa watumishi wa umma ingeweza kupunguza kodi, haijazungumza lolote lile, huku ni kuwapuuza watumishi wa umma. Ikumbukwe kwamba wakati wa kampeni viongozi mbalimbali walikuwa wanaomba kura na Viongozi wa Serikali hii ya Awamu ya Tano na wengine walikuwa wanapiga *push up* majukwaani wakiomba kura, leo watumishi wa umma wamepuuzwa, wamesahaulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nasikia ilipokuwa siku ya Mei Mosi pale Iringa, Mheshimiwa Rais anasema hajawahi kuzungumzia popote pale kuhusu kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma wakati mwaka jana Mei Mosi kule Moshi - Kilimanjaro alisema mwaka unaofuata kwa maana ya mwaka huu, angeweza kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma lakini mwaka huu akiwa Mei Mosi amesema kwamba hakuwahi kuzungumza popote pale kuhusu kuongeza mishahara. Hii siyo sahihi, huku ni kuwapuuza watumishi wa umma...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga, unakwenda kwa kasi sana, hebu ngoja upewe taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Haonga kwamba, jambo hili kwanza lilishaamuliwa na Kiti chako kwa sababu mara tu baada ya sherehe za Mei Mosi, tayari kuna Wabunge walitaka kulipotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais mwaka 2017 hakutoa ahadi hiyo, lakini alitoa maelezo fasaha ya utaratibu ambao utatumika pale ambapo Serikali itakuwa tayari kufanya hicho anachokizungumza. Jambo hili limerudiwa tena na Mheshimiwa Rais katika sherehe za Mei Mosi mwaka huu wa 2018. Hata hivyo, pamoja na Kanuni ya taarifa, ninaomba nirejee kwenye Kanuni ya Utaratibu, jambo ambalo limekwisha kuamuliwa na Bunge hili halipaswi kurudishwa tena ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakumbuka, nami nina kumbukumbu sahihi kwamba siku ambayo ulikuwa umekaa kwenye Kiti hiki ulishalifanyia maamuzi jambo hili na siyo tena vema likaendelea kurejewa na kupotoshwa ndani ya Bunge lako. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana MheshimiwaWaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Haonga, karibu uchangie lakini usiende kwenye *danger zone.*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Tuelewane kwanza. Suala la mishahara ya watumishi wa umma lilizungumzwa, nikaombwa mwongozo, nikalitolea maamuzi na siku ile nilikuwa mwenyewe hapa. Kwa hiyo, tuchangie kwa kadri utakavyoona inafaa lakini siyo kupotosha kwamba Rais alitoa ahadi. Tuendelee.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki nibishane sana na Kiti chako, lakini ukweli unajulikana, Watanzania wanajua ukweli jinsi ulivyo au uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe Mosi Februari, 2016, watumishi waliandikiwa barua za kupandishwa vyeo au kupandishwa madaraja, tarehe Mosi Februari, 2016. Tarehe Mosi Novemba, 2017 barua hizi zikafutwa, yaani mwaka moja baadaye barua za watumishi kupandishwa madaraja au vyeo zikafutwa. Hili jambo ni kuwaumiza watumishi kweli, hili jambo halikubaliki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi ameandikiwa barua ya kupandishwa cheo au kupandishwa daraja, mwaka mmoja baadaye barua inaandikwa nyingine ya kufuta cheo chake. Mwaka huo 2016 kuna watumishi walistaafu na waliondoka na barua ambayo imeshaandikwa mwaka huo na tunajua kabisa kwamba pensheni ya mtumishi wa umma wanai-*calculate* kulingana na mshahara wake wa mwisho au daraja lake la mwisho, leo huyo mtumishi ameshastaafu yuko nyumbani inakuja kuandikwa barua nyuma kwamba tumeshafuta. Hii siyo sahihi kabisa na haikubaliki kabisa kuwafanyia Watanzania ambao ni wazalendo katika Taifa hili na wanaofanya kazi ngumu sana katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watumishi ambao wamestaafu tangu mwaka 2015 hawajalipwa mafao yao hadi leo tunavyozungumza. Mwaka 2015 hawajalipwa pensheni yao, mwaka 2016 hawajalipwa, mwaka 2017 hawajalipwa, hii ni 2018 bado sioni kwenye bajeti hii kama kuna matumaini kwa watumishi hawa ambao wamelitumikia Taifa hili kwa uzalendo na kwa uadilifu wa hali ya juu sana. Namshauri Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango, Watumishi wa Umma ni vizuri wale waliostaafu walipwe sasa mafao yao, walipwe fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu kilimo. Bajeti hii ni ndogo, lakini bajeti ya Wizara ya Kilimo imetengewa asilimia 0.52 ya bajeti yote. Tukumbuke Maputo *Declaration* na baadaye Malabo *Declaration,* viongozi wa Afrika wote walishauriwa kwamba angalau

bajeti zao asilimia 10 iende kwenye bajeti ya kilimo, leo Bunge letu hili Serikali imekuja na 0.52 tunakwenda kwenye nchi ya viwanda ambayo naona haitawezekana kwa sababu bajeti ya kilimo imekuwa ni ndogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira haya hata kufikia nchi ya uchumi wa kati na nchi ya viwanda naona ni ndoto za Alinacha, ni ndoto za mchana kweupe. Hatutaweza kufikia kwa sababu siku njema inaonekana tangu asubuhi. Kama tumetenga asilimia 0.52 maana yake viwanda itakuwa ni ndoto, tunazungumza tusiyoweza kuyatenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la masoko ya mazao, juzi nimesikia Serikali inasema sasa tumesharuhusu mazao yauzwe popote pale. Ukweli ni kwamba wananchi wetu wengi wanaolima mazao mbalimbali, kwa mfano wakulima wanaolima mahindi, Mkoa wa Songwe wananchi waliuza debe la mahindi mwaka mmoja na nusu Sh.20,000 kwa debe moja, leo wanauza Sh.3,500 na maeneo mengine na mikoa inayolima mahindi ni mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata soko la mahindi nchini Kenya, baada ya kufunga mipaka kuzia mahindi yasipelekwe nje, Kenya wakaenda kununua mahindi Zambia, wameenda kununua Uganda, wananchi wetu wakakosa masoko ya mahindi. Wamenunua pembejeo kwa bei kubwa sana, hali ni mbaya kwelikweli, Serikali lazima ioneshe *commitment* kwamba masoko ya mazao *trip* hii hawatazuia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la Serikali ya Awamu hii ya Tano imetia fora kwa kuleta Bungeni bajeti isiyotekelezeka. Mwaka 2016/2017, Bunge hili tuliidhinisha trilioni 31.7....

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haonga, unga mkono sasa. Sasa namwita Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nipate kutoa mchango wangu na naomba Serikali haya nitakayoyasema pia wayachukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuna vitu ambavyo hatuangalii. Ulinzi ni jambo muhimu sana katika Taifa hili, lakini tumekuwa tunatenga bajeti hewa, kwa nini nasema hivyo? Mwaka wa fedha 2016/2017 zilitengwa bilioni nane na pesa hizi zilitengwa kwa ajili ya uwanja wa ndege, kukarabati maghala ya silaha, lakini fedha hizi hazikuenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gongo la Mboto paliwahi kutokea maafa makubwa tu. Ndani ya vyombo hivi vya ulinzi na usalama, hasa Jeshi la Wananchi kuna vitu ambavyo ni nyeti ambavyo vinatakiwa Bajeti ya Serikali ipelekwe kwa wakati muafaka. Sasa vitu kama hivi tunapitisha ndani ya Bajeti ya Serikali halafu havitekelezeki tunasema ni bajeti hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la wastaafu, Wanajeshi wastaafu siyo watu wazima sana, ustaafu unajua kuna wastaafu wengine ambao pia wameshafika umri wa kustaafu lakini mpaka sasa hivi wengine wako kazini, lakini hawa walishastaafu. Ni kwa nini hawataki kuwapa stahiki zao Wanajeshi wastaafu? Wanajeshi Wastaafu sasa watajisikia unyonge na ni watu na taaluma yao, wamekusudia vipi kujenga mioyo yao au wanataka ibadilike. Kwa sababu ni watu wenye fani mbalimbali lakini Serikali haitaki kutoa mafao yao kwa wakati. Siyo Wanajeshi tu, wapo wastaafu wengi ambao wanaidai Serikali, je, mpaka sasa hivi Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wastaafu wote inawalipa kwa wakati muafaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Wajane. Hawa Wanajeshi ambao wanakwenda kupigana huko nchi za wenzetu wanakwenda kulinda amani, lakini wengine wanapata maafa, wengine wanakufa, hata hapa kwenye

nchi yetu, lakini hawa Wanajeshi wakishakufa hawa wajane hawaangaliwi, wala zile stahiki zao hawapewi kwa wakati muafaka. Ni lini Serikali watatoa hizi stahiki za hawa Wajane wa Wanajeshi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la vijana. Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya 'Hapa Kazi Tu'. Tumeona kuna ongezeko kubwa sana la vijana, ukianza na vijana ambao wanamaliza vyuo hawapati ajira kuna vijana wa kati, hawa vijana wengine wa mitaani ambao wanaishia *form four,* wanamaliza darasa la saba hawana ajira, hata wale ambao wanajiajiri wenyewe, basi bado Serikali hawajatazama kundi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye kundi hilo kuna kundi la wanawake sasa hivi linaongezeka kwa kasi, linakuja kwa *speed*, waangalie ni namna gani sasa hawa wanawake hawana kazi, hawana vyanzo vya miradi, maendeleo madogo madogo ya kujiendeleza kwa kujikimu na walisema watatoa kila kijiji milioni 50, zile milioni 50 kwa kila kijiji zimekwenda wapi? Hakuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija huku kwenye Halmashauri, vyanzo vya mapato pia wamechukua kupeleka Mfuko Mkuu. Sasa waangalie namna gani vijana wanaingia kwenye mambo yasiyokuwa na maana, akinamama nao wanaingia kwenye janga la mambo ya kujiuza huko, hakuna maana, matokeo yake mnasema tupime UKIMWI, huu UKIMWI utaendelea na utazidi kuendelea kwa sababu sasa kipato hakuna, mtu anatafuta namna ya kujikimu hakuna, Serikali hawaangalii haya makundi ya wapiga kura, vijana, akinamama, wazee, hawawaangalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango sasa tuangalie huu mpango wa mwaka huu unatekelezeka? Tukiangalia huku nyuma yale aliyosema watapeleka milioni 50 kwa kila kijiji hakuna, watawezesha vijana hakuna, watawezesha akinamama hakuna. Sasa nimesoma Gazeti la Nipashe leo Mheshimiwa Rais amesema kuna mikopo

ambayo inatoka, kwa kweli kama hii mikopo ipo basi itoke kwa wakati muafaka ili angalau wananchi wapate ahueni, hasa hili kundi ambalo nimelitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Zanzibar. Zanzibar ni nchi na imeshasoma bajeti yake, lakini Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Naibu Waziri ni lazima kuna masuala wananchi wa Zanzibar nao wanataka wayapate, wapate ufumbuzi wa mambo haya kwa sababu haya mambo yanakuwa yanaenda hayapati muafaka. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atoe kama ni kwenye Gazeti la Serikali au kuwe na kipindi maalum cha kufahamisha wananchi kuhusu hii Akaunti ya Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Akaunti ya Pamoja imekuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu kwa sababu kule Zanzibar wanasema, sisi tunachangia kiasi gani na Muungano nao huku Tanzania Bara wanachangia kiasi gani, hawajui. Kwa sababu nao kule kuna *percent* ambazo zinatoka kwenye mambo ya ushuru ziende kule, kuna pesa zinazotoka kwenye Akaunti ya Pamoja ziende kule ili zichochee miradi ya maendeleo, zichochee mambo ya barabara na mambo mengine. Sasa kunakuwa na kizungumkuti, wanasema pesa haziendi kwa wakati muafaka, kinachochangiwa kwa pande hizi mbili hakijulikani, kwa hiyo naomba hili somo walitoe na waangalie ni namna gani ya kufahamisha hawa wananchi wapate kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mambo ya ushuru. Bandari ndiyo kitega uchumi cha Tanzania, lakini sasa hivi kwa ukiritimba wa *TRA* mizigo ya bandari imeshahamishwa, imehamia kwenye bandari za wenzetu. Tunusuru, kuna watu wanatumia mwavuli wa Rais, kumsingizia Rais Mheshimia Dkt. Magufuli kwamba yeye ndiye anawatuma kwenye mambo ya kukusanya kodi, lakini wengine wanaenda kwa utashi wao kwa kutumia mwavuli wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wale waende kwa mujibu wa sheria na kile ambacho kinatakiwa wakidai kwa wakati muafaka, siyo kwenda kubambikiza wananchi kodi

kwa kutumia mwavuli wa Rais. Taaluma zao wazitumie kwa sheria na kanuni na siyo kusema Rais kasema, maagizo yametoka juu, hakuna maagizo yaliyotoka juu, wao wana taaluma zao za kukusanya ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara hawa wadogowadogo wanalalamika. Hebu wapite huko Kariakoo, watu wanafungua maduka kwa kuvizia, leo Zanzibar waweke pia ni kitu gani ambacho kinatakiwa kikishalipiwa ushuru kwa Zanzibar, Tanzania Bara kisilipiwe ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukiangalia mizigo bandari imepungua, watu wanatafuta njia tu, hata mtu anakwenda *South Africa,* anakwenda wapi, lakini ilimradi mzigo wake anahakikisha haujapita Bandari ya Tanzania, sasa mapato tutayapata wapi? Serikali itapata wapi pesa kama hawajaboresha utaratibu mzuri wa kukusanya mapato ya Serikali na kuwashirikisha wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi iliyoendelea bila wafanyabiashara, hakuna nchi iliyoendelea bila matajiri. Kwa hiyo waangalie, waweke urafiki wa kukusanya kodi na hawa matajiri wasiwe maadui wao, wawe marafiki zao kwa sababu tukiweka mfumo mzuri kwa wafanyabiashara na Serikali nayo itapata Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili tatizo la vijana wanaomaliza vyuo nimerudia tena mara ya pili, ajira hizi mpya zitatoka mwaka gani, wakija hapa waseme kabisa ajira katika sekta hii zitakuwa hivi na katika zile pande za Muungano hizi ajira zitatoka hivi na zile pande za Muungano ambazo pia zinakaimiwa ajira zake zitakuwa lini kamili na zile Taasisi za Muungano nazo ambazo zinadaiwa wachanganue tusije tukaonekana kama Zanzibar labda hawalipi umeme, Zanzibar hawalipi nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sekta za Muungano wanatakiwa waje wazichambue. Hii Taasisi inadaiwa inatakiwa ilipe, hii Taasisi ni Taasisi hii ilitakiwa itoe *percent*

hii iingize Serikali haijalipa, kwa sababu sijui kama mwananchi wa kawaida kwa uhakika hakuna mwananchi wa kawaida Zanzibar ambaye anadaiwa kuhusu hata hili suala la ... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, unaunga mkono eeh nimekusikia. Mheshimiwa Mayeye.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia jioni ya leo, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kusimama hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kabisa na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt, Philip Mpango pamoja na Naibu Waziri nimeipitia bajeti, niwapongeze sana kwa kuweza kupunguza kodi katika hizi taulo za kike. Naamini kwamba wamemfikiria binti wa Kitanzania ambaye yupo kijijini ambaye alishindwa kujiifadhi na wapo wengine mpaka kutumia majani kwa sababu ya kushindwa kupata hizi *pads*. Kwa hiyo, niwapongeze sana kwa kumfikiria binti huyu wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu suala zima la kilimo, wote tunafahamu kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Wote tumefika hapa tulipo, wazazi wetu wamekuwa ni wakulima wamelima na leo Mheshimiwa Waziri wa Fedha umefika hapo naamini hata kule Buhigwe babu yangu alikuwa akilima na akamsomesha na amefika hapo. Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii tuzingatie sana suala la kilimo, kwa sababu naamni kilimo ni uti wa mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri bado kuna mazao ambayo sijaona wakiyapa kipaumbele kwa mfano zao la mawese ndani ya Mkoa wangu wa Kigoma. Zao hili la michikichi, mbali na kwamba linatoa mafuta, pia linatoa bidhaa nyingi, tunaweza kutengeneza sabuni kwa kutumia michikichi, bado

tunaweza kupata mafuta ambayo yanaweza yakalainisha ngozi na muonekano mzuri kwa akinamama, ningeomba sana tuweze kujali suala hili la michikichi na tutenge bajeti kwa wananchi wa Kigoma na maeneo mengine, tulifanye zao hili kwamba ni la biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika michikichi, leo michikichi iliyopo katika Mkoa wa Kigoma tayari imeanza kuzeeka, lakini wananchi wa Kigoma wako tayari kulifanya zao hili la biashara, naomba sana Mheshimiwa Waziri kuna mbegu bora ambazo sasa zinapatikana za michikichi waweze kuwagawia wananchi wazipate bure, mashamba yapo, maeneo yapo, waweze kulima na wapate mbegu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mche mmoja leo unauzwa kwa Sh.5,700, katika maisha ya kawaida mtu hawezi kulima heka moja na akaweza kupata michikichi hii. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie zao la michikichi Kigoma, Serikali iwagawie wananchi michikichi na tuko tayari kuweza kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tena zao la alizeti. Alizeti inalimwa katika maeneo ya Singida na maeneo mbalimbali. Ningeomba sana Serikali tulifanye hili kama zao la biashara, mikoa yote tuweze kulima alizeti tuweze kupata mafuta na tuweze kuondokana na uhaba wa mafuta katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie tena katika suala zima la afya, maeneo mengi ndani ya nchi yetu ya Tanzania bado kuna changamoto ya Wauguzi, hospitali nyingi hazina Wauguzi na hata nikitoa mfano katika Mkoa wangu wa Kigoma nimekuwa nikilisemea sana na kuuliza, kwamba hatuna Madaktari katika hospitali ya Mkoa, hata baadhi ya vituo havina Wauguzi. Unakuta kituo cha hospitali au zahanati kina Muuguzi mmoja katika hali ya kawaida bado tutaendelea kuwa na vifo vya mama na mtoto kwa sababu hatuna Wauguzi wa kutosha wa kutoa huduma kwa haraka na wakati unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii wanapokwenda kutenga fedha wahakikishe kwamba ajira hizi 8,000 wanazozitoa basi waweze kutusaidia ndani ya Mkoa wa Kigoma tupate Wauguzi wa kutosha na maeneo yote yenye changamoto hizi yaweze kupata Wauguzi. Wauguzi watakapokwenda katika maeneo husika basi waweze kulipwa pesa zao kwa haraka na kwa muda ambao unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie katika suala zima la ajira. Ajira imekuwa ni changamoto kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania hasa kwetu vijana. Vijana wengi wamekuwa wakimaliza vyuo; lakini wanakaa mtaani. Wao wanasema kwamba tujiajiri, kijana huyu wa Kitanzania anaweza kujiajiri vipi kama hata mtaji hana? Kwa hiyo, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika kuhakikisha kwamba wanaleta ajira kwa vijana hata kama wao wanajiajiri basi waweke mikakati ya kumwezesha kijana kujiajiri na biashara mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha kwamba sasa Afrika tunakabiliwa na tatizo la ajira, vijana wengi wamekuwa wakikimbilia nchi za ughaibuni kutafuta ajira, lakini katika bajeti hii sijaona Mheshimiwa Waziri ameelezea suala la ajira kwa vijana kwamba kama Waziri, kama Serikali wana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanawasaidia vijana wa Kitanzania na je, tupo katika hatari gani kama vijana wa Kitanzania kukimbilia katika nchi zingine kutafuta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisikia watu wakiangukia katika bahari wanatokea Ethiopia, lakini hata Tanzania kuna vijana ambao wanakimbilia South Africa, wanaishi maisha magumu South Africa, wanateseka wanauawa, yote hiyo ni kwa sababu hakuna ajira, wanaona bora wakimbie nchi zingine kutafuta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha baba yangu Dkt. Mpango waweke mikakati ya kumsaidia kijana wa Kitanzania

kuondokana na changamoto ya ajira. Hii itasaidia vijana kujiepusha na vitendo vya wizi, lakini itawasaidia vijana hasa kina dada kuepukana na tabia hii ya kujiuza ili waweze kupata kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie tena katika suala la *TRA*. Tunasema kwamba ‘Hapa Ni Kazi Tu’ na kweli wananchi wanajituma kufanya kazi. Imekuwa inasikitisha hata Mama Lishe ambaye anajitahidi kuchuuza ili aweze kumsomesha mtoto na kuondokana na umaskini bado *TRA* wanamsumbua. Hata kijana huyu wa Kitanzania ambaye ametoka shule anasema ngoja nijiajiri nifungue kibanda changu niweze kupata riziki, bado *TRA* wanakimbizana nae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli hii inakatisha tamaa na kwa stahili hii tutaendelea kuwa na vibaka na wezi ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, ningeomba sana *TRA* Mheshimiwa Waziri ukae nao uongee nao, imekuwa ni changamoto kubwa, imekuwa ni kero kubwa watu wanafunga maduka, imefikia hatua sasa mtu anaona nina milioni tatu siwezi kufanya biashara, kwa sababu milioni tatu hata dada akisema afungue kisaruni chake kidogo bado hataweza kufanikiwa kwa sababu *TRA* nao wako nyuma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri suala zima la *TRA* kiukweli wakae nao chini waangalie ni jinsi gani wanaweza kutusaidia wananchi, isifike mahali sasa mtu unaogopa hata kufungua biashara yoyote kwa sababu unaamini *TRA* wanakwenda kunisumbua. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Aisee waambie tena! *(Kicheko)*

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie tena katika suala la nishati. Nipongeze sana Wizara ya Nishati kiukweli wanafanya kazi nzuri katika miradi hii ya *REA* maeneo mengi yamepata umeme na naamini hata yale ambayo hayajapata umeme yanakwenda kupata umeme katika *REA* III. Pia nipongeze mradi huu wa Mto Rufiji, binafsi naona ni

mradi mzuri na naupongeza sana, lakini naomba kutia msisitizo kwamba tuhakikishe fedha zinakwenda kwa wakati, pia nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba tutenge bajeti ya kutosha katika suala zima la nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi huu pamoja na kwamba tunaenda kupata megawati nyingi za umeme lakini kwa sababu tunakwenda katika nchi ya viwanda bado naamini kwamba yawezekana ule umeme usitoshe na tukahitaji umeme mwingine, tuweze kuwa *encourage* hawa *private sector investors* waweze kuja kuwekeza na wenyewe katika nishati hii ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nishauri jambo moja, kwamba ingekuwa ni vizuri.....

**MWENYEKITI:** Ahsante. Unga mkono tu nitakuruhusu.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimalizie kwamba ingekua ni vizuri ikatengwa bajeti kwa sababu ya watu wa *TANESCO* wakafanya *feasibility study and then* ikaelezea kwamba hapa tunazalisha megawati kadhaa, tumetumia kiasi kadhaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante haya.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hamidu Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuweza kutimiza mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani pamoja na *Sunnah* ya sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze suala la korosho. Nimefuatilia mjadala wa asubuhi ulivyokuwa unaendelea na namna watu walivyokuwa wanataka kulipotosha jambo hili.

Mimi nilikuwa Lindi nimerudi jana, athari za pesa za *export levy* kutopeleka Bodi ya Korosho wataziona mwaka huu kwenye mapato ya korosho. Kwa sababu naamini labda Mheshimiwa Dkt. Mpango anachotaka ni asikie kwamba korosho zimeshuka uzalishaji atafurahi labla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango kwamba Bodi ya Korosho mwaka huu imeshindwa kutoa *sulphur* yenye ruzuku, hawajatoa hata mfuko mmoja. Mpaka sasa, nainapozungumza humu ndani ya Bunge sasa hivi mfuko mmoja wa *sulphur* unauzwa Sh.70,000 kutoka Sh.30,000 ya mwaka jana. Hivi ninavyoongea ndani ya Bunge chupa ya dawa ya viuatilifu ambayo ilikuwa inanunuliwa Sh.15,000 sasa hivi inauzwa Sh.51,000 wakulima wanakopeshwa kwa riba kubwa, yako makampuni nimeyakuta yako Jimboni yanakopesha wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango anachokitaka ni kwamba mazao yote yafe na korosho ife jibu litapatikana mwezi wa Kumi wala siyo mbali, korosho itakufa ili afurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu walitaka kutupotosha hapa kwamba *export levy* siyo fedha wakulima. Tunasema fedha ya wakulima kwa sababu korosho zimelimwa na wakulima, fedha ile kwa mujibu wa sheria asilimia 65 inakwenda kwenye maeneo yaliyolima korosho. Maana yake ni kwamba ile fedha ndiyo iliyokuwa inatumika kutengeneza ama kuandaa miche. Wataalam wa Hazina wapo pale wananisikia wamekwenda kule wamezunguka Lindi na Mtwara kwenda kuangalia wale watu waliokuwa wanaandaa miche na walikuwa wanasema wanakwenda kufanya tathmini, wamefanya tathmini wamemaliza wanawalipa lini, wale watu wanalipwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongea hapa kuna watu leo nyumba zao zimewekwa *bond* na benki, Bodi ya Korosho iliingia mikataba na wazalisha miche, mpaka sasa

hakuna. Nimezungumza na wale watu ambao walichukua *tender* Jimboni kwangu, nilikutana nao juzi, nikazungumza nao wanalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango anatakaje, tuache kulima korosho, atuambie? Anayesema kwamba asilimia 65 siyo fedha ya wakulima maana yake ni nini? Fedha hii ndiyo ilikuwa inafanya utafiti, wakumbuke kwamba Kituo cha Utafiti cha Naliendele ndiyo miongoni mwa vituo bora vya utafiti vya korosho Barani Afrika, imepata na tuzo, wao ndiyo wamefanya utafiti wa korosho wamepeleka korosho Nigeria, wamefanya utafiti wa korosho wamepeleka korosho Gambia, wamepeleka korosho Ivory Coast, jana nimewaona watu wa Naliendelea wanalalamika hawajapata fedha ya maendeleo hata shilingi kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umezuka ugonjwa wa mikorosho, wote wameona Waziri wa Kilimo alikuwa anahangaika hapa na Naibu wake, umezuka ugonjwa mikorosho inakauka kule Liwale, wanashindwa kufanya utafiti hawa hawana fedha hata shilingi tano, sasa kuna mtu anasisima anasema fedha za *export levy* siyo za wakulima ili iweje, mikorosho ife?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango nimemsikia Mwenyekiti wangu wa Wabunge wa Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Bwege ametangaza maandamano waandae Magereza watatufunga. Kama wameandaa Askari kuja kutukamata kutupiga watatupiga ikitokea mpaka tarehe Mosi tunatoka hapa fedha bilioni 200 hawajapeleka, tunakwenda kuandamana tunadai fedha zetu tutafunga barabara, hatutakubali kwa sababu ni fedha zetu, ni fedha za wananchi, wanataka kuua zao la korosho tubaki kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango ni Mchumi, Mchumi wa aina gani ambaye hafanyi *affirmative action* kwa watu maskini. Ninachojua Serikali kunapokuwa na *gap* kubwa la maendeleo baina ya

walionacho na wasionacho, hawa wasionacho wanafanyiwa *affirmative action.* Watu wa Mikao ya Lindi na Mtwara mara nyingi tumekuwa maskini, kiwango cha umaskini Lindi na Mtwara ni kikubwa, kitu pekee kingeweza kutusaidia ni zao la korosho, leo wanataka kuliua! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili hatukubali kabisa*, it is nosense to remain here* wakati korosho wanataka kuiua, hatutakubali kubaki Bungeni wakati korosho wanataka kuiua hatukubali, kwa sababu ndiyo njia pekee ya kutokea wananchi wa Lindi na Mtwara. Huu mjadala ulioletwa wa kutaka kuja kubadilisha sheria, wanataka kuja kubadilisha sheria ili pesa hizo wazichukue, wakae nazo, wapange lini tuwapelekee na lini tusiwapeleke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongea kama labla hawajui sasa hivi kuna maeneo korosho zimeanza kuokotwa. Mimi mwenyewe ni mkulima wa korosho ninasema hilo, nimekwenda shambani kwangu nimekuta korosho zimeanza, tayari, mpaka leo Bodi hawana hata mfuko mmoja wa *sulphur* hizi korosho watazipata wapi, shilingi trilioni 1.3 ya fedha ya korosho kama ya mwaka jana wataipata wapi? Mheshimiwa Dkt. Mpango huu ni uchumi wa aina gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuseme labda watatuelewa, kwamba katika suala la korosho fedha shilingi bilioni 210 ambazo zimebaki zilikuwa bilioni 210, shilingi bilioni kumi mmepeleka, bado bilioni 200 fedha hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango apeleke. Apeleka kabisa wakulima wa korosho hatumwelewi na hatutamwelewa maisha yote. Hii habari tunaongea mchana wengine mpaka usiku tukilala tunaota kwenye ndoto, hii habari siyo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wangekuwa wanajua huko wakulima wanasemaje wala wasingekaa hapa wakasema, kwa sababu ninachokiona kama wakishindwa kabisa wajue kwamba hicho Chama chenu ndiyo kinakufa Kusini na *we*

*are very serious!* Watu wa Lindi tuna historia ya kufanya hivyo. Nawaomba sana hili jambo wali-*take very serious*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimesikia suala la *Gaming Board,* hii Bodi ya Michezo ya kubahatisha pia nimeona namna wanavyotaka kuongeza *tax.* Ukiwasikiliza wadau wa michezo ya kubahatisha wanasema wanachokipata wao ni 1.4 *percent*. Sasa hivi wanataka kuwaongezea kodi ya mashine kutoka Sh.32,000 mpaka kufika Sh.100,000 kwa mashine moja. Nimekutana na Taasisi moja wanasema wao wana mashine 1,550 kwa mwezi wanalipa kodi shilingi milioni 49. Leo wakiwaongezea kodi ya Sh.100,000 maana yake michezo yenyewe itakwisha watashindwa kabisa hata kupata hiyo kodi yenyewe. Sasa hivi kupata kidogo ambacho wanakipata kila mwezi, *TRA* wanakusanya na kukosa kabisa lipi ni jema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii kama hawajui sasa hivi wamebatizwa jina badala ya kuwa 'Hapa Kazi Tu' wameitwa 'Hapa Kodi Tu'. Wamekuwa ni watu wa kodi tu!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji amesema anashukuru Mwenyezi Mungu amefunga siku 30 salama na sita kamili salama. Namshangaa Muislam mzima anatetea kamali! Nampa taarifa hiyo akumbuke. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Taarifa hiyo unasemaje Mheshimiwa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa, sijatetea kamali. Maana yake ukisema hivyo unasema kwamba watendaji wote kila mtu ana dini yake hapa ndani, maana yake tusifanye shughuli za Kiserikali hilo jambo halipo. Ninachokisema kwamba kama tunaamua

ku-*discourage,* tu-*discourage totally* kwamba Tanzania hatutaki michezo ya kubahatisha. Kama tunaamua iwepo kwa ajili ya kutengeneza ajira za vijana, basi tuamue kwamba iwepo na itozwe kodi inayostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho najua muda umekimbia sana, bajeti *discipline.* Mheshimiwa Dkt. Mpango tunaweza tukapanga fedha nyingi sana hapa, je, nidhamu ya utoaji wa fedha iko wapi? Changamoto ya Serikali tangia Mheshimiwa Dkt. Mpango umekuwa Waziri ni nidhamu ya bajeti. Bajeti *discipline* ni ndogo, kinachopangwa na Bunge sicho kinachoenda kufanyika. Leo wanaweza wakapanga shilingi fulani ziende huku hata fedha ambazo zimekuwa *ring fenced* wanazitumia kwenye matumizi mengine. Nidhamu ya kibajeti haipo na hili ndiyo tatizo kubwa ambalo linawapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hii bajeti wanaosema inawezekana ikawa bajeti hewa ni kweli. Ukisoma kitabu cha bajeti inaonesha mapato ya ndani yatakuwa trilioni 18, maana yake ni kwamba kila mwezi watakuwa mnakusanya 1.5 trilioni, ukipiga mahesabu matumizi ya kulipa deni pamoja na watumishi wa umma ndo hiyo 1.5 trilioni, fedha za maendeleo ziko wapi au ndiyo wanakwenda kukopa kwenye hiyo mikopo ya kibiashara ambayo inasababisha riba kubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *discipline* ya kibajeti lakini changamoto nyingine walionayo ni kwamba namna ya matumizi ya fedha, sioni kama kuna dalili ya fedha za ndani zitatumika kwenye miradi ya maendeleo na kusipokuwa na fedha za ndani kwenye miradi ya maendeleo tukategemea wahisani na mikopo tu, mpaka Mheshimiwa Magufuli anatoka nchi hii ataacha deni kubwa kabisa ambalo litakuwa siyo himilivu na halitalipika na Rais ajae atakuta mzigo mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa James Millya, hayupo, Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae. Mheshimiwa Tunza Malapo

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Naomba nipate majibu ya haya mambo ambayo nitayaongea na sidhani kama nitatumia dakika zote kwa sababu mengi yameongelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasikia hapa wanasema kwamba kuzalisha umeme kwa njia ya gesi ni gharama kuliko kwa njia ya maji ndiyo maana wanakwenda kwenye *Stiegler's*. Swali langu; wakati wanakwenda kukopa pesa nyingi, mabilioni kwenda kuwekeza kwenye bomba la gesi, wananchi wetu wa Mkoa wa Mtwara wamepigwa, wanawake wajawazito walijifungua kabla ya siku zao, walikwenda kukopa na kuwekeza wakati hawajafanya utafiti wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate majibu ya swali hilo kwa sababu hiyo *Stiegler's* ipo kabla hata hiyo ya gesi, ama vyote vilikuwa pamoja wakaenda kuwekeza kwenye gesi kwa pesa nyingi ambayo kama nchi tutatakiwa kulipa. Sasa hivi tunatumia kati ya asilimia sita mpaka saba, leo wanahamia kwenye *Stiegler's* kwa mbwembwe nyingi wakisema huu huku ni gharama kuliko huu, waliingia bila utafiti? Tukiwaambia kwamba tunakwenda kwa mizuka wanakasirika, huu haukuwa mzuka? Naomba nipatemajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho, lazima tu niiseme yaani hakuna namna. Unapozungumzia uchumi wa Mikoa ya Kusini, Mkoa ninaotoka mimi Mtwara huwezi kuzungumza bila ya kutaja korosho, yaani *no way out.* Sasa kama kuna mtu anafikiria hizo pesa tunazozizungumzia zaidi ya bilioni mia mbili si za wakulima, hivi kama wakulima wale wasingenyeshewa na mvua, wasingeng'atwa na nyoka, jua lisingewawakia, hizo trilioni moja nukta ngapi ambayo

ilipatikana kwenye *export levy* ingepatikana kutoka wapi? Kwa hiyo hatuwezi kuona kwamba hizo pesa siyo za wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimezaliwa Mtwara mpaka leo ninavyokwambia naishi Mtwara, mimi si Mbunge wa Mjini, kwetu ni huko huko Mtwara. Wakati huo sisi tunakua, Bandari ya Mtwara ilikuwa inafanya kazi kutokana na korosho zikaanza hujuma. Mara meli haiwezi kufika hapo, mizigo hakuna na vitu hivi, Bandari ile ikaanza kudorora. Mama lishe, vijana ambao walikuwa wanafanya kazi pale wakawa hawafanyi kazi kwa sababu ya kutokuijali bandari ile na kuiendeleza kutokana na zao la korosho. Sasa tumeanza kurudi kidogo tunaonekana Wamakonde wale wanapeleka watoto wao shule ili waondokane na ile dhana ya watu wa Kusini hawakusoma kwa ajili ya kilimo cha korosho, leo hawataki kupeleka hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kusikitisha kabisa, kama mnakumbuka, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu ambaye namheshimu sana; mnakumbuka mwaka jana alipita kuzindua miche kupanda, kuwahamasisha watu, ile miche mpaka leo haijalipwa, wale watu ambao wameotesha hawajalipwa, *is it fair?* Wanawatakia nini Waziri Mkuu na watu wake wa Kusini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate majibu na pia naomba nipate majibu ni nini mkakati wa Serikali, tuna kiwanda kinachozalisha *cement* pale cha Dangote, lakini kwa kiasi kikubwa *cement* ile inasafirishwa kwa barabara, hatujaona meli ya mizigo na barabara ile kila siku ukipita kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam kila siku ina viraka kwa sababu inabeba mzigo mkubwa. Maendeleo yoyote ni gharama. Sasa nataka nijue kama Serikali ina mkakati wowote wa kuleta meli ya mizigo ili kusudi bandari yetu itumike kusafirisha mizigo ikiwemo na ile *cement.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia madhumuni ya hiyo pesa ya wakulima, mimi sina namna nyingine ya kuiita hiyo pesa ya korosho, kuna madhumuni mengi kwa nini

ikaanzishwa, wadau wa korosho wakafikiria ili tuliendeleze hili zao, tutenge pesa ambayo itasaidia. Dhumuni mojawapo tumesema ni kuwa na mikakati endelevu kuhusu zao la korosho ambapo mikakati hiyo inafanyika kwenye utafiti katika Chuo cha Naliendele ambapo *90 percent* ya matumizi ya pale yanategemea hiyo *export levy.* Kwa hiyo kama hatupeleki tujue tumeua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kitu kingine, zao la korosho ukiliangalia, yaani wale Watafiti ukienda pale Naliendele wana mashamba ya mikorosho ambapo ile mikorosho inatunzwa vizuri ili iweze kutoa mbegu bora, hivi wanataka wale watafiti wetu waende wenyewe shambani wakalime ili watunze mikorosho wapate mbegu bora za kuendeleza hili zao ambao wanasema kwamba liende kwenye mikoa mingine ambapo sasa limesambaa katika mikoa 17?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu za korosho ni tofauti na mbegu zingine, kwamba unachukua shambani unaleta, hizi ni lazima kwanza uanze kutunza ile mikorosho iwe katika *standard,* unavuna *then* unakuja kuotesha, watu wanapata miche, wanakwenda kuiotesha kwa ajili ya kuendeleza zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhumuni lingine ni kufanya usimamizi na uratibu mzuri wa stakabadhi ghalani. Hawataki watu wauze *Kangomba* wanataka watu wauze korosho zao ghalani, hivi wale watu wote ambao watakuwa wanafanya hizo shughuli wanazifanya kwa kupata pesa kutoka wapi kama hawataki kutoa pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango ameitwa kwenye kikao si mara moja wala mara mbili, alikataa kuja. Angekuja, akatoa majibu watu wangemwelewa kwa nini alikataa kuja, pesa wamezipeleka wapi? Hilo ndilo swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapoongea ni mwezi wa Sita, msimu kule umeshaanza hakuna *sulphur,*

hakuna madawa, hakuna nini, hivi anategemea mwakani hata kama hiyo sheria yake ikapita na naamini itapita kwa sababu ni tumezoea, hakuna kitu kinachoingia humu ndani kikashindwa kupita. Hiyo Sheria yake imepita, anataka pesa zote zikusanywe ziwekwe kwenye huo Mfuko wa pamoja, atakusanya kitu gani kama korosho hakuna?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni suala tu la kujiongeza, kwamba, tunahitaji tuhudumie vizuri ili mazao yawe mengi, aidha atakusanya yeye, atakusanya nani kwa sababu yote ni Serikali, hapa *issue* siyo kukusanya, *issue* pesa ikusanywe lakini pia itumike kwa matumizi yaliyokusudiwa. Atakusanya nini kama hakuna korosho? Atakusanya nini kama *sulphur* haijakwenda? Atakusanya nini kama madawa hakuna? Atakusanya nini kama kwenye taasisi ya utafiti hakufanyiki utafiti? Nafikiri hilo jambo wala halihitaji akili kubwa sana, ni jambo tu la kawaida, kwamba unahitaji uwekeze ili upate mavuno, sisi hatutaki kuwekeza, tunataka tupate mavuno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhumuni la tatu, tunasema kuendeleza ubanguaji wa korosho nchini, sasa hapo ndiyo majanga. Viwanda havieleweki, mashine hakuna, matatizo chungu mzima, Waziri wa Viwanda ukimuuliza kwamba kuna kiwanda gani kimetengewa eneo Mtwara Mjini? Anakwambia eti Chikongola kuna eneo, Chikongola hapo mnapopasikia ni katikati sokoni. Sasa sijui ametenga sehemu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya nimeuliza hili swali mwenyewe sikuwepo, nikajibiwa kwamba eti Chikongola sokoni wametenga eneo sijui sehemu gani. Kwa hiyo, yaani kuna vitu ambavyo ukikaa, ukivitafakari yaani ni lazima ushangae kwamba uelekeo wetu uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimalize; tunachotaka watu wa Kusini ni pesa siyo maneno kama maneno tumeyasikia mengi tu. Hayo maneno aliyoyasema Mwenyekiti, Mheshimiwa Bwege wa Lindi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Hebu lisaidie Bunge umesema *Kangomba*, *Kangomba* ni nini?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kangomba yaani kule kwetu kuna bakuli kubwa hivi ambalo lile wanapima kwa ujazo siyo uzito.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo ni Kimakonde?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Kibantu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Kishimba Jumanne ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mpango pamoja na Naibu wake Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. Hali kadhalika shukurani hizi pia zifike Mamlaka ya Mapato *(TRA)* kwa kazi nzuri ya ukusanyaji ambayo inaendelea na watendaji wote walioko katika Wizara hii. Mwisho, lakini si kwa umuhimu bali kwa kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwen yekiti, mimi ningetaka kuanza na hili hili la korosho ambalo naona kama linataka kuligawa Taifa. Sisi ni watunga sheria, sisi tunasimamia maslahi ya wananchi, hivyo ni lazima wakati tunafanya wajibu huo tuhakikishe kwamba ndimi zetu tunazielekeza katika kujenga Taifa na si katika kulipasua. Tutajadiliana kwa hoja, tutabishana kwa hoja mbalimbali lakini msingi wetu mkubwa uwe katika namna bora ya kujenga, siyo namna ya kuanza kugawana mbao za Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tukianza kuzungumza kanda, kanda, kanda naamini hatutabaki kuwa na Taifa linaloitwa Tanzania. Kwa hiyo nitoe rai sana kwa Waheshimiwa Wabunge tujadili mambo haya kwa hoja, kwa *fact*, kwa *data* lakini tusiingize haya mambo ya kuanza kuvutana kwa misngi ya Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili suala la korosho ambalo kwa Sheria hii ya Mwaka 2010, nataka nianzie hapo hapo kwamba, lazima kwanza pia tutafakari kwamba kwa hiyo miaka mitano, hizi pesa zilivyokuwa zinakwenda zimefanya kazi ya kuongeza uzalishaji kwa kiasi gani? Sasa hapa ni lazima Wizara ikiwezekana ifanye uhakiki wa namna bodi ilivyoweza kusimamia hizi hela tangu hiyo mwaka 2010 hadi sasa; je, ni kwa kiasi gani imeongeza tija si tu katika uzalishaji lakini kwa yale makusudio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu mojawapo ya kuanzisha hii *export levy* ilikuwa ni ku-*discourage* kusafirisha korosho ghafi kwenda nje ili ikiwezekana sasa tuwe na viwanda vya kubangua korosho. Hata hivyo tunachoshangaa ni kwamba viwanda vingi vya kubangua vimezidi kufungwa. Wameanza Feeder Hussein na kiwanda chao cha *Premier cash* wamefunga, *Olam* wamefunga kiwanda wamepelela Msumbiji, *Mohamed Enterprises* nae amefunga kiwanda; kwa hiyo lazima tuone...

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** ...huu mchakato mzima...

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anayechangia nataka nimpe taarifa kwamba, viwanda vyote vilivyofungwa ni viwanda binafsi na fedha ya *export levy* ilikuwa inakusudia ku-*empower* viwanda vya Serikali; na ndiyo maana kuna viwanda vimefufuliwa ukienda Tandahimba leo kuna viwanda, ukienda Nachingwea kuna

kiwanda, ukienda Mtama kimefufuliwa kiwanda na kitaanza ubanguaji muda wowote. Kwa hiyo kama wamefunga watu binafsi siyo hoja kwamba viwanda...

**MWENYEKITI:** Ahsante, usichangie; Mheshimiwa Shangazi unasemaje kuhusiana na taarifa hiyo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anachofanya yeye ni kuwahisha shughuli. Nilikuwa nataka nije kwenye sababu, sababu mojawapo ambayo viwanda hivi vimeshindwa ni kwamba wenzetu India kule wao korosho ghafi wanaipa *incentive.* Kwa hiyo maana yake ni kwamba huku wakati tunaweka *export levy* ku-*ban export* wenzetu kule wanatoa *incentive* ku-*encourage* watu wasafishe korosho ghafi. Kwa hiyo kama viwanda binafsi vimeshindwa hata vya Serikali pia haviwezi vika-*compete* kwenye hilo soko. Kwa hiyo lengo hapa ni kwamba, tutafute mjadala wa pamoja siyo huu wa kutishana. Tukianza kutishana na wengine tunazalisha *carrot,* tunazalisha viazi tutaanza kusema na vyenyewe...

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilindwe, niendelee na kuchangia hapa hilo la mjadala...

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo Mheshimiwa, ngoja kidogo. Tunalinda muda wako. Mheshimiwa Bungara nataka kama unatoa taarifa, toa taarifa tu siyo kutuhutubia hapa. Umeona *trend* yake anavyochangia vizuri tu.

**MHE. SELEMAN S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumzia hapa ni fedha asilimia 65 kwenda kwa wakulima wa korosho, hiyo ni sheria. Sasa akituambia tunatisha, sisi hatutishi. Sisi tunadai haki kwamba asilimia 65 ya korosho iende katika sehemu ambayo inalimwa korosho na...

**MWENYEKITI:** Ahsante umeeleweka, umeeleweka. Mheshimiwa, Mheshimiwa…

*(Hapa Mheshimiwa Selemani Bungara aliongea bila kipaza sauti)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa…

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** …asilimia 65 tunaitaka iende kwa wakulima…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Mheshimiwa…

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Hii iko kwa mujibu wa Sheria…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara!!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Na hatumtishi mtu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara!!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** *Inshallah*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nitakutoa nje sasa hivi. Mheshimiwa Shangazi endelea.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni hoja yake yeye, sasa hiyo atabaki nayo yeye, mimi ya kwangu ni hayo ambayo nimeyaeleza kwa maana kwamba tujadili mambo haya kwa mapana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la *transit goods*; *TRA* hapa lazima tuangalie, tuongeze wigo wa hizi siku, siku 30 ku-*clear* mizigo ni siku chache sana. Kwa nini nasema chache? Katika siku 30 utoe *weekend,* wiki nne ukitoa siku mbili mbili ni siku nane, kama itaangukia nayo kuna sikukuu nayo uitoe. Pia tunajua utendaji katika nchi yetu, kuna siku utaambiwa leo *system* haiko vizuri siku zinazidi kushuka.

Kwa hiyo unaweza ukakuta kwamba utendaji kamili wa hizi siku 30 za ku-*clear* mizigo ni kama siku 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili jambo kwa mapana. Ili bandari yetu iweze kushindana na bandari nyinginezo kama Beira, *South Africa* na kule Angola, ni lazima tuhakikishe kwamba tunaongeza wigo wa siku angalau zifike 60 hadi hata 90 kwa sababu hili ni eneo ambalo tunaweza tukalitumia vizuri sana kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mzigo unaotoka labda Burundi au Rwanda ukifika pale unatakiwa ndani ya siku 30 uwe umeondoka. Kwanza utakapobaki tunapata *storage,* tunapata *wharfage,* kwa hiyo ni lazima suala hili tuliangalie kwa kina; lakini sambamba na mafuta ambayo yanasafirishwa kwenda katika nchi ambazo zinatuzunguka, yakifika siku 30 wanatakiwa waya-*localise* kama bado yamebaki. Kwa hiyo namshauri sana Mheshimiwa Waziri jambo hili aliangalie kwa kina, linaweza likatusaidia sana kuongeza mapato na pia likaweza kuifanya bandari yetu iweze kushindana. Hii itatusaidia pia kuboresha Bandari hizi za Mtwara na Tanga na hata Bandari mpya hii ya Bagamoyo kwamba zitakuwa za kibiashara zaidi kuliko hivi zilivyo sasa, inakuwa kama ukiritimba umekuwa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningelizungumza ni suala la kilimo hasa tunapoanza na Benki hii ya Kilimo. Benki ya Kilimo walitakiwa waanze katika mikoa mitano Tanga ikiwemo lakini mpaka sasa bado hawajaanza shughuli zote katika Mkoa wa Tanga. Nadhani kuja kwa Benki ya Kilimo ilikuwa ni mahususi kwa ajili ya kuja kufufua zao la mkonge ambalo zao hili sasa limeanza tena kupanda soko huko ulimwenguni. Kwa hiyo nimsihi sana asimamie katika eneo hili ili Benki hii ya Kilimo iweze kwenda kwenye ile mikoa mitano ambayo inatakiwa ikafungue matawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna suala la kuangalia ushuru katika bidhaa za ambazo zinaingia

kama vifungashio*;* hivi vinaingia kwa *zero tax* kiasi kwamba sasa vinaathiri uzalishaji wa magunia. Viwanda ambavyo vinazalisha magunia kwa kutumia bidhaa ya mkonge kwanza vinashindwa kupata soko kwa sababu mkonge kidogo upo ghali na hata hii korosho tunayoizungumza ingekuwa ina maana sana kama tungeisafirisha katika magunia yaliyotengenezwa kwa mkonge, maana yake tungeongeza uzalishaji zaidi. Kinachotokea sasa hivi kwamba, tunaingiza vifungashio vinaingia bila ya kodi, vinasafirisha korosho na mazao mengine; kwa hiyo matokeo yake ni kwamba viwanda vinavyozalisha bidhaa za mkonge vinakosa kuzalisha, vinakosa kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nizungumzie suala la chikichi kule Kigoma. Mheshimiwa Dkt. Mpango anaona wenzetu wanaanza kugawana mbao za Taifa naye anatoka Kigoma. Nadhani uwe ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba zao la chikichi kule Kigoma nalo linapewa umuhimu wa kipekee. Tukishakuwa na uzalishaji mkubwa wa michikichi; na nadhani kuna maandiko kadhaa kwenye *RCC* yao kule Kigoma wameshayapitisha, itaweza kusaidia uzalishaji wa mafuta tukichanganya na mafuta haya ya alizeti. Matokeo yake ni kwamba tutaweza kuondokana na hii adha ya kuagiza mafuta kutoka nje na ambayo wakati mwingine yanatuletea shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimsihi sana, michikichi iliyopo kule imeshazeeka sana, haiwezi tena kuzalisha mafuta haya. Kwa hiyo lazima tuanzishe utafiti mpya kwa ajili ya kuweza kuangalia hali ya hewa lakini pia tupate mbegu bora zaidi ambazo zitakuja kuwa na tija katika uzalishaji wa hili ambalo tunalikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ambalo ningependa kuzungumzia suala hili la *electronic stamp* naye jana alilizungumzia vizuri. Nakubaliana naye kabisa kwamba hili suala ni vizuri tukaenda kwa hatua; tukaanza katika haya maeneo ambayo tayari wameshaanza *stamps* hizi kawaida, kwenye maeneo ya mvinyo, vinywaji, sigara na vinywaji vikali, kwamba tungeanza huku kabla hatujaingia kwenye hizi *daily*

*consumable goods* hizi soda, maji na juisi, kwanza tuziache tuanze na hizi hizi ambazo wameanza nazo ili tuone *performance* iko namna gani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri Ahsante.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Dkt.Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Stanslau Shing'oma Mabula.

**MHE.DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Nianze kwa kuunga mkono hoja. Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii ya Fedha kwa bajeti nzuri yenye mwelekeo wa kuipeleka nchi yetu Tanzania katika hadhi ya uchumi wa kati mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa mkakati wa ujenzi wa viwanda ili nchi yetu iweze kujikomboa kutoka kuwa nchi tegemezi kwa karibu kila kitu na kuelekea katika hadhi ya uchumi wa kati nchi yenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza mpango wa kutenga maeneo maalum ya uwekezaji *EPZ* na *SEZ*. Uwekezaji katika maeneo haya utachochea sana maendeleo ya viwanda katika nchi yetu hususani maendeleo ya viwanda ambayo yana mpangilio mzuri na yanawezesha kulinda mazingira na kusaidia ukuaji wa miji yetu katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Bagamoyo Serikali imetenga hekta jumla ya 9,080 kwa ajili ya viwanda,

eneo maalum la *EPZ* katika jimbo la Bagamoyo. Awamu mbili zilifanya hivyo, awamu ya kwanza jumla ya hekta 5742 na *EPZ* awamu ya pili jumla ya hekta 3388. Katika *EPZ* awamu ya kwanza ilitathiminiwa mwaka 2008, wafidiwa 2,180 kwa thamani ya shilingi bilioni 60, lakini mpaka hii leo mwaka 2018 kwa maana baada ya miaka 10 baadaye, wafidiwa 1,025 bado hawajalipwa fidia yao, jumla ya shilingi bilioni hamsini na moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, fidia ni mazingira wezeshi ya viwanda, kwa maana unapolipa fidia ardhi ile sasa inakuwa huru ili mwekezaji aweze kuwekeza viwanda. Kabla hujafanya hivyo maana yake mazingira yale si wezeshi tena. Pia inamuwezesha mwananchi wa kawaida kuweza kujenga upya maisha yake, kumudu kukimu familia na kuweza kuhakikisha kwamba anafaidika na eneo lile ambalo ameliacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu Tukufu iwalipe fidia wananchi hawa ili ardhi ile iwe huru, pia wananchi waweze sasa kuendeleza maisha yao vizuri na wawekezaji waweze kuwekeza viwanda. Muda si rafiki, miaka imepita mingi na wananchi wa Tanzania wanakiu ya maendeleo wamechoka na umaskini, sasa tufanye kazi tu kama ambavyo Mheshimiwa Rais anasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya *EPZ* Bagamoyo ilihusisha maeneo ya makazi ya watu wengi, naiomba Serikali kwamba iondoshe maeneo ya makazi ya watu wengi katika mpango wa *EPZ*, wananchi hawalikubali hili, hawana mahali pengine pa kwenda. Tuache katika hiyo awamu ya kwanza ya hekta 5,742 iwe sehemu ya *EPZ* kwa ajili ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua ya kijasiri ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge,* hili ni jambo kubwa sana. Reli ni kichocheo cha maendeleo ya viwanda na kichocheo cha maendeleo ya uchumi katika nchi yetu. Ila reli hii ya kisasa yenye uwezo

mkubwa italipwa na sehena za mizigo kutoka nchi yetu na nchi jirani ambazo zinatuzunguka kama Rwanda, Burundi, DRC-Mashariki, Zambia na Malawi, ni shehena hizi za mizigo ambazo zitalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya abiria ni nyongeza tu na ni faida ambayo itawezesha watani wangu Tabora na Mwanza kuweza kusafiri lakini siyo nauli za abiria hazitoweza kulipa. Kwa maana kwamba bila shenena ya mizigo itakuwa vigumu sana reli hii kubwa kuleta manufaa katika nchi yetu, haitoweza kujilipa. Sasa mwenzie reli yenye uwezo kama huu ni nini? Mwenzie ni bandari, bandari kubwa, yenye uwezo mkubwa wa kuweza kuleta shenena ya mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 Mamlaka ya Bandari iliweza kufanya *study* na ika-*establish* kwamba itahitaji kujenga bandari Bagamoyo, bandari kubwa ya kisasa, miundombinu mipya ambayo inaendana na Tanzania ya kesho. Sasa Mheshimiwa Waziri ili reli hii iwe na tija maana yake ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ni bora uanze mapema na uanze kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi na mkakati wa ujenzi wa Bandari Bagamoyo, kwa sababu Rais wa China na Rais Mstaafu Jakaya Kikwete tarehe 24 Machi, 2013 walishuhudia utiaji saini wa *implementation agreement* kuhusu ujenzi wa Bandari Bagamoyo, leo ni miaka mitano baadaye bado tunazungumza. Katika kipindi hiki cha miaka mitano wabia wetu wa *China Merchant* wamekamilisha mazungumzo na wamejenga bandari katika maeneo yafuatayo; Djibouti, Abuja, Ivory Coast, Colombo-Sirlanka, wamejenga pia *Tin-Can City* Nigeria na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa wenzetu hawa wanawezaje kukamilisha maongezi na kuanza kujenga ndani ya miaka mitano hii wakati sisi tunaongea. Wao wana nini na sisi tuna nini? Tuna watalaam wa kutosha wa kuweza kukamilisha maongezi na kuweza kuhakikisha kwamba ujenzi unaanza mapema iwezekanavyo. Wananchi wa Tanzania wana kiu ya maendeleo na ni muhimu tuhakikishie kwamba

tunaondoa umaskini wa wananchi hawa mapema iwezekanavyo. Hatuwezi kuendelea kusubiri kila siku wakati, wakati tuna watu ambao wanaweza kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha atuambie ni lini tunaanza ujenzi wa Bandari Bagamoyo ili bandari hii iweze sasa kuungana na reli mpya ya *SGR* na barabara zetu kuu za usafirishaji ili kuweza kuchochea maendeleo ya uchumi katika nchi yetu, tunahitaji tuondokane na umaskini. Mwaka 2025 Tanzania kuwa na uchumi wa kati ni miaka sita tu usoni yaani muda hatuna. Muda umekwisha ama sivyo tutafika mwaka 2025 tunajitathmini ni kwamba hakuna ambacho tumeweza kukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali kubwa kabisa namba moja kwa maendeleo ya nchi yetu ni watu wetu, wakiwemo vijana wetu wa kike na vijana wa kiume. Kuna mahitaji makubwa sana ya mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana wetu wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne ambao wanakosa nafasi ya kuendelea katika elimu ijayo. Jambo ambalo linanisikitisha ni kwamba, Serikali imekuwa na mtindo wa kutokupeleka *VETA* fedha za *SDL* na hili ni jambo la kisheria. Kwa taarifa nilizonazo takribani shilingi bilioni 65 hadi mwezi Aprili mwaka huu zilikuwa hazijapelekwa katika Wizara ya Elimu kama fedha za SDL kwa ajili ya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha za malimbikizo karibu miaka mitatu, sasa *VETA* wanahitaji hizi hela za *SDL* ili waweze kupanua nafasi za mafunzo kwa ajili ya vijana wetu. Kupanua nafasi za mafunzo kwa kutujengea *VETA* katika Wilaya zetu, kununua vifaa vya mafunzo na kununua vifaa vingine ambavyo vinawezesha mafunzo mazuri kwa ajili ya watoto wa kitanzania yaweze kutekelezwa. Vijana hawa wawe na *skills* mikono mwao, waweze kuingia katika soko la ajira wakiwa na *skills* katika mikono yao, wawe watu ambao wataisaidia nchi hii kufika katika uchumi wa kati mwaka 2025. Naiomba Wizara ya Fedha wahakikishe kwamba hizi pesa zinapelekwa....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kawambwa. Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Shing'oma, Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. JUMMANE J. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye bajeti yetu hii ya 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili au matatu kama muda utaniruhusu. Suala langu la kwanza alijaribu kuliongelea hapa Mheshimiwa Ngeleja. Suala hili la dhahabu tumekuwa tukiliongea leo mwaka wa tatu toka tumeingia hapa Bungeni, sijaelewa ni kwa nini Waziri Mpango hataki kulielewa. Mara ya kwanza mimi nilikuja na hoja ya *one percent* kwa dhahabu kwa watu wanaofanya *export*. Tuliongea na Mheshimiwa Mpango lakini baadaye sikupata jibu kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhahabu ni sawasawa na dola, sijaelewi kwa nini tunapuuza dhahabu ya wachimbaji wadogo ambayo ni karibu ya asilimia 70 ya dhahabu yote ya Tanzania na leo migodi yetu mikubwa imefungwa. Sisi tunaotoka maeneo hayo ya dhahabu tunaifahamu dhahabu vizuri sana. Benki Kuu ya Tanzania ilianza kununua, kama alivyosema mwaka 1991/1992, baadaye ilisimama baada ya matatizo yaliyotokea pale kwamba uaminifu uliokuwepo haukuwa mzuri kati ya wafanyakazi wa Benki Kuu na wafanyabiashara waliokuwa wanapeleka dhahabu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukiangalia *trend* ya dhahabu duniani, kama alivyosema Mheshimiwa Ngeleja, kwamba tangu mwaka 1999 kwa mfano dhahabu imekuwa ikipanda kwa *speed* nzuri sana. Serikali ingekubali kununua

dhahabu kwa ushindani kwa bei ya soko la dunia kwa shilingi za Tanzania ingeweza kupata faida kubwa na ingeweza kuifanya pesa yetu kuwa imara. Sasa hivi kinachofanyika ni kwamba, Serikali inapotaka kulipa madeni lazima ichukue pesa za shilingi ika-*source* dola, lakini ingekuwa inanunua dhahabu ingeuza kipande cha dhahabu wakati inapotaka kulipa deni. Hii ingesaidia shilingi yetu vile vile isiweze kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nafikiri kinachotusumbua hapa huenda hii dhahabu ya *local* kwa kuwa haimo kwenye mitaala ya shule, labda kwa kuwa haiko shuleni kwa watalaam wa uchumi inawapa kigugumizi; kwa sababu Waamerica na Waingereza wanaotoa elimu hawana hiyo dhahabu ya kuokota mitaani. Kwa hiyo kuna uwezekano mkubwa kwamba, kila ukimwambia mtu ambaye hafahamu anaona unaongea kitu ambacho si sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka 1999 kweli dhahabu ilikuwa dola 270 kwa *Ounce,* ambayo ni kama dola nane ama tisa; leo iko dola 1400 ambayo ni takriban dola 50. Kwa hiyo imepanda kwa asilimia 800. Pesa ya Tanzania mwaka 1999 ilikuwa 1,300 leo ni 2,300, pesa ya Tanzania ime-*depreciate* kwa asilimia 80. Kwa hiyo kama tungekuwa na *stock* ya dhahabu deni la Taifa tungelifuta lote mara moja na tusingekuwa na deni lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Mpango ajaribu aidha atuite watu tunaotoka maeneo ya madini, tujaribu kuongea na watalaam wake kama kuna sababu hasa, kwa maana hatupi jibu ni kwa sababu gani. Leo dhahabu yetu Uganda wana-*charge 1.5 percent* kwa *export levy*, Burundi *1.0 percent,* Rwanda *1.0 percent;* na watu hawa hawana mgodi hata mmoja na wote tuko Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sisi tunaletewa *plastic* na Wachina, sasa itawezekanaje? Sisi tuna kiwanda cha kuchapa dola, dhahabu ni dola, ni kama una kiwanda cha kuchapa dola, hutakiwi hata kufikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo *indication* ya bei ya dhahabu duniani inaonekana kwamba itaendelea kupanda; nitatoa sababu tatu ambazo zinaonesha itaendelea kupanda. Sababu ya kwanza, ni kuwepo kwa sarafu mpya duniani; kuna sarafu ya Euro, kuna sarafu mpya ya China ambayo imekuwa imara, kuna sarafu mpya ambayo inatarajiwa ya nchi za Brazil, South Afrika na nchi za Asia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile dhahabu sasa hivi imeanza kutumika kutengeneza kwenye komputa na *laptop*, kiasi ambacho sisi ambao tunayo dhahabu, tunayo *chance* nzuri zaidi ya kupata faida kutokana na dhahabu. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Madini wajaribu, kama watalaam wao wanakuwa na kigugumizi kwa ajili ya matatizo yaliyotokea mwaka 1992, teknoloji ilikuwa bado, leo teknoloji ya dhahabu ni ya kugusa simu unajua ina *percent* ngapi ya dhahabu ndani yake; tunaomba wasiwasi huo uondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajenga reli kwenda Mikoa ya Mwanza na kwenda Mikoa ya Kigoma. Wajerumani wakati wanajenga walikuwa wakati huo huo wanaandaa na mazao ya kwenda kubebwa na treni ile. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mpango awekeze kwenye mazao ambayo treni *standard gauge* itakapokuwa imefika kule Kigoma na kule Mwanza licha ya abiria kuwe na mazao ya kuweza kubeba kurudi nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa *idea* ndogo tu, kwamba Malaysia kilichofanya wakafanikiwa kwenye michikichi ni kwamba walikuwa wanampa mtu mche wa mchikichi halafu kila mwezi wanamlipa pesa yule mtu. Baada ya miaka mitatu mchikichi ilivyoanza kutoa matunda yule mtu analipa. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aweke pesa pale, awapatie wananchi wetu michikichi na mikorosho awape Sh.1000 kila mche, gharama yake itakuwa Sh.40,000 peke yake kwa mche mmoja, lakini baada ya miaka mitatu atakuwa na miche mingi ya

korosho nyingi na michikichi mingi. Kwa hiyo treni yake itakapofika Kigoma atakuwa na mizigo ya kurudi nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tu, ningemalizia kwenye kodi ya viwanja na majengo. Tanzania ni nchi pekee ambayo ina-*charge* kodi ya viwanja na majengo kwa kumfata mtu. Nchi zote duniani zinatumia kwenye *bill* ya maji au umeme. Mimi kama kodi ya kiwanja ni Sh.24,000 au kodi ya jengo ni Sh.24,000 tunagawa kwa 12. Kwenye *bill* yangu ya maji unaleta elfu mbili ambayo inakuwa *indicated* pale kwenye *bill* ya maji au ya umeme. Nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaweza akalichukua hili litamsaidia zaidi na hatakuwa na sababu yoyote ya kushinda kutwa nzima na majembe *Auction Mart*, kamata huyu, funga huyu, inaweza ikatusaidia sana sana, Mheshimiwa Waziri wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naomba nihitimishe mchango wangu kwa kuongelea suala la bandari. Bandari yetu ya Dar es Salaam inafanya kazi vizuri. Hata hivyo namwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango aangalie zile bidhaa ambazo zinakwenda nchi za jirani, aongee na wafanyabiashara wa Kariakoo kwamba kwa nini bidhaa hizi haziuzwi hapa, ili aone ufumbuzi. Kama zinaweza kuteremshwa bei na hazina madhara kwa viwanda vya Tanzania ni vizuri ikafikia upya suala la kupunguza kodi juu ya bidhaa ambazo zinaweza kulipishwa ushuru hapa na wewe ukapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kishimba, kwa mchango wako mzuri

**MHE. JUMMANE J. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio Mheshimiwa Kishimba anaongelea kutokana na uzoefu wake kwenye biashara. (*Makofi*)

Kwa hiyo tunakushukuru sana kwa ushauri huo, nadhani Serikali nzima wamekusikia. Tunaendelea Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma, Mheshimiwa Kafumu na Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. STANSLAU S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushuru kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo kuchangia kwenye bajeti hii muhimu kabisa kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. Pia niungane na Waheshimiwa wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia lakini ambao wameona umuhimu wa kuendelea kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa kazi kubwa ambayo imeendelea kuifanya katika kuhakikisha inatatua changamoto za Watanzania. *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yetu ni kwamba bajeti hii ya mwaka 2018/2019, pamoja na muonekano wake wa kwamba inakwenda kujibu changamoto nyingi ambazo tumekuwa tukizijadili kwenye miaka mingi iliyopita, lakini yako mambo ambayo ni lazima sasa tuendelee kuyazingatia. Kwa sababu tumeamua kuyaleta sasa ni lazima tuyasimamie ili utekelezaji wake ukaonekane moja kwa moja kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameongelea suala la uimarishaji wa viwanda vidogo kwa maana ya SIDO lengo lake likiwa ni moja tu kubwa kuendelea kutoa ujuzi na taaluma mbalimbali kwa vijana ambao hawajafikia kiwango kikubwa cha elimu ili wawe na ujuzi ambao utawasaidia katika soko la ajira hasa tunapokuja kuzungumza habari tarajiwa ya viwanda vingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la viwanda vya *SIDO* au wazo la hivi viwanda vidogo vidogo lazima liwe na mipaka. Inawezekana sana tunakosea; leo unakwenda kule kwa kina Mzee Lubeleje kijijini kabisa kule au kwa kina Mzee Mwamoto kule nako unataka kuweka kiwanda cha *SIDO* watu wengine wamezoea shughuli tu za kulima wanataka walime tu. Kwa hiyo nimwombe sana tuangalie, tuwe na malengo. Inawezekana tukachukua manispaa, halmashauri za miji na majiji tukaimarisha shughuli za viwanda vidogo

vya *SIDO* kwa kuanzia ili tuzalishe wataalam wengi zaidi na kuzalisha vifaa vingi zaidi ambavyo vitasaidia kuvipeleka ma mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie juu ya habari ya wazabuni. Mheshimiwa Waziri ni shahidi wamekusanya fedha nyingi sana na Serikali imefanya kazi kubwa sana. Wazabuni waliofanya kazi na taasisi za elimu, shule, hospitali na maeneo ya taasisi za Jeshi la Polisi na wananchi wanapata tabu sana ya malipo yao kwa muda mrefu sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwaomba sana tujitahidi kwa namna yoyote ile tuhakikishe tunalipa madeni haya, kwa sababu kwa kuwalipa hawa tunaongeza mzunguko wa fedha. Naamini Mheshimiwa Waziri fedha tunazo nyingi sana za kutosha na baadaye nitamwambia kwa nini fedha hizi naamini anazo kwa sababu ya mambo makubwa ambayo Serikali hii imeyasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kodi ya ardhi; Mheshimiwa Kishimba hapa amelizungumza na mimi niliseme kwa namna ya tofauti kidogo. Niwashukuru sana Wizara ya ardhi kwa kuamua kuanzisha urasimishaji wa makazi kwenye miji yote mikubwa. Maana yake ni nini, kodi tunayokusanya sasa naamini kodi ya ardhi haijafikia hata asilimia 30. Tukiweka mfumo mzuri majengo yote ambayo tunataka yapimwe yakapimwa sawasawa, naamini Serikali hii kupitia kodi ya majengo peke yake Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango anaweza akakusanya fedha nyingi sana na zikaendelea kutusaidia katika kutatua changamoto tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivi hatutakuwa leo tunahangaika kuwa na bajeti ambayo mwisho wa siku hatufikii malengo ya ukusanyaji wa fedha. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, naamini, leo kila mtu anashangaa kwa nini Serikali inafanya miradi mikubwa, lakini ukiangalia fedha peke yake tunayokusanya kwa mwezi mmoja na matumizi tulioyonayo hayalingani na kiasi tunachokusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mheshimiwa Mpango anasahau naye kwenye hotuba yake amemsifu sana Mheshimiwa Rais, lakini naona amemsifu kwa vitu vidogo vidogo sana. Nimkumbushe Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango, wakati najaribu kusoma kuangalia, miaka ya nyuma huko wakati sisi tuko nje tunatamani kuja kwenye Bunge hili tulikuwa tunaona Bunge likisimamia na kulalamikia mambo makubwa. Leo tumekuja humu mambo haya yote yamefanyiwa kazi na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango hajatuambia kwa mfano wako Wabunge humu mwaka 2012/2013 alikuwa Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Ndugulile na wengine wengi walifika hatua ya kugomea bajeti hii kama hii tunayoijadili leo wakitaka mambo ya msingi ambayo Serikali iilkuwa inashindwa kuyasimamia wakiamini yangeweza kuleta mapato mengi kwenye Serikali lakini yalishindikana. Leo Mheshimiwa Dkt. Mpango tunazungumza hapa, nimpe mfano wa mambo matatu tu kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi si Mhasibu lakini nilikuwa nasoma naona, wanazungumzia habari ya *illicit financial flows;* yeye anafahamu kwa kiasi gani Serikali ya Awamu ya Tano imezuia masuala yote yanayotokana na mfumo huu. Haya ni pamoja na mikataba ya kampuni nyingi ambapo mikataba ya kampuni zinazoshughulika na rasilimali za Taifa zilikuwa zinasimamiwa na zilikuwa zimeachwa wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango ni shahidi, hapa wamesimamia masuala ya mikataba, masuala ya usafirishaji wa mizigo. Kwa mfano mdogo alikuwa akija hapa tunasikia tunauza nguzo nje ya nchi, lakini zinauzwa hapa nchini zinapelekwa Kenya au *south Africa* halafu zinarudishwa hapa zinanunuliwa kwa gharama kubwa zaidi. Hili limekoma na limekwisha, leo ni kiasi gani cha fedha kimeokolewa hapa? Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri kuna kitu kinaitwa *dollarization,* matumizi ya dola

nchini. Mtu alikuwa anaweza kuja na begi zake za dola akaondoka na begi zake za dola hapa hakuna mtu anauliza. Leo kwa kiasi gani Serikali yake imefaidika na kuzuia utaratibu wa matumizi ya dola yasiyokuwa na mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge hili mwaka 1992 Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi kwa kiasi kikubwa sana leo nchi yetu haiko kwenye mfumo wa matumizi ya moja kwa moja kwa dola kama Zimbabwe na nchi zingine. Sisi dola ni matumizi ambayo si ya lazima, lakini sheria iliyoruhusu kufunguliwa *account* za dola na matumizi ya dola imeweka mipaka ambayo ilikuwa wazi, leo wamedhibiti maeneo hayo na fedha zinapatikana kwa wingi; hii ni sambasamba na *transfer pricing.*

Mhehimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mambo haya makubwa ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imeyafanya yametuongezea fedha kiasi gani, yameiongezea Serikali nguvu ya kiasi gani, aje hapa awaambie Watanzania wajue mabadiliko ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana tukisimama hapa tunaongelea Mheshimiwa Magufuli kafanya mambo makubwa watu hawatuelewi na ndiyo maana wanasema msisifie tu. Yako mazingira yanatulazimisha tusifie na Mheshimiwa Waziri anapokuja atuambie kwa kiasi gani Serikali imeokoa fedha nyingi kwenye maeneo hayo matatu na ambayo leo tunazungumza Serikali hii tunaweza kuwa na miradi mikubwa ambayo inafikirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye kila halmashauri tunazungumzia kujenga vituo vya afya, hospitali za Wilaya 60, tunazungumzia kujenga vituo vya afya kila kata, fedha zinatoka wapi? Tulizonazo ukipiga hesabu hazitoshi, lakini kwa sababu kuna mifumo wamesimamia, wamezuia fedha nyingi zaidi zimepatikana, ndio maana Serikali ya Awamu ya Tano ina fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie jambo moja dogo sana, tunazungumza habari ya mjadala hapa namna gani Serikali inataka kuanzisha Mfuko mmoja *(Treasury Single Account);* wala si jambo jipya. Tukifuatilia kwenye hotuba na mijadala ya Bunge la mwaka 2014 suala hili limepitishwa na maazimio ya Bunge hili bada ya umoja wa nchi za Afrika Mashariki na Kati kuamua kuwa na mfumo huo. Sasa leo hapa tunataka kulifanya kama jambo jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ukichukulia kwenye halmashauri zetu, mwaka mzima uliopita leo kati ya halmashauri 151 tulikuwa na zaidi ya *account* 1,500, leo tuna *account* zisizopungua chache 150 na kitu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. STANSLAU S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa kwenye *pick* sasa, naunga mkono hoja kidumu Chama cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naelewa treni la kasi hilo. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Yahya Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti hii Kuu ya Serikali kwa mwaka huu 2018/2019. Nitangulie kwa kuunga mkono hoja, lakini pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mawaziri, Waziri wa Fedha na Naibu wake, kwa hotuba yao nzuri, yenye nia njema kwa nchi hii na kuifanya nchi hii ijitegemee kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia juhudi kubwa za Serikali katika kujitegemea katika umeme kwa kujenga sasa *Stiegler's Gorge*. Vile vile nipongeze juhudi za Serikali za kujenga Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mawazo yangu kidogo ya kuishauri Serikali, kwamba sasa ione sekta ya kilimo inaweza ikawa na mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi hii, lakini ni sekta iliyoajiri zaidi ya asilimia 66 ya Watanzania lakini haija-*reflect* vizuri katika bajeti hii ni namna gani tunawabeba wakulima wetu ambao baadaye tunatarajia kwamba sasa sekta hii iendelee kuajiri hata wasomi ambao wanatoka katika vyuo vikuu ambao ajira katika sekta iliyo rasmi imekuwa hamna kama inavyoonekana. Sasa nia yangu ni kuishauri Serikali tuone namna gani sasa tutawezesha kilimo hiki. Tukiendelea kutegemea kilimo hiki cha mvua bado hatutaweza kufika popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa Serikali ikatoa mwelekeo wa namna gani tutaweza kuwa na kilimo cha umwagiliaji maeneo mengi, ni namna gani tutawezesha miundombinu ya kufanya kilimo cha umwagiliaji kiwezekane hususani katika mikoa kame Mikoa ya Kanda ya kati ya Dodoma na Singida. Katika mpango wake kuna bwawa hili la hapa Farkwa ambalo kama litajengwa kwa wakati lina msaada mkubwa sana kwa wakulima wa Kanda ya Kati, Skimu za umwagiliaji ambayo ipo ya Bahi na maeneo mengine ya mkoa wa Singida yatanufaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali ione ni namna bora ya kufanya sasa hata *deep well* za kutosha ambazo zitafanya maeneo mengi ya umwagiliaji. Tukitegemea kilimo hiki cha mvua ambacho tumekizoea mwaka ambao mvua itakuwa kidogo itakuwa ni namna ngumu sana ya kujitegemea hata kwa chakula ambacho kwa miaka hii mingi sasa tumeanza kujitegemea. Ni vizuri sasa Serikali ikawekeza pahali hapo ili wananchi wetu na nchi kwa ujumla iweze kunufaika. Hata hivyo, niipongeze Serikali kwa kutenge pesa kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima hususani mahindi ya kupitia *NFRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sekta pia ambayo imesahauliwa. Sekta ya misitu ilikuwa na mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi hii lakini hapa katikati

kumeyumba, tumekuwa tunagemea *export* za *species* chache sana kama mitiki, lakini wakati huo wanunuzi wa tiki na wachakataji wa tiki wamekuwa na usumbufu lakini bei za mazao yale katika mashamba ya Serikali zimekuwa ni kubwa zaidi kuliko hata bei za masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uwezo sasa kuiambia Serikali ifanye machakato wa kutosha kuona *specie* nyingine ambazo ziko kwa wingi katika nchi yetu. Na-*declare interest* mimi ni mdau katika sekta hiyo, zinaweza kutuondoa katika changamoto hii ya maduhuli ya Serikali kwa kiwango kikubwa sana. Miaka 2011, 2012 hadi 2013 ukiangalia katika mchakato mzima wa *export* ya nchi hii sekta ya misitu ilikuwa na mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea hapa katikati kumekuwa na *ban* za ajabu ajabu, zinafika mahali wananchi wajasiriamali na wenye viwanda sasa wanakosa malighafi katika viwanda ambavyo Serikali iliwashauri wananchi watoke kule ambako walikuwa wana *export* mazao ghafi. Sasa wamewekeza kwenye viwanda sasa hivi tena viwanda vile vile vimekosa malighafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya misitu kama itasimamiwa vizuri itakuwa na mchango mkubwa sana kama zilivyo sekta za utalii na wanyamapori katika uwindaji wa kitalii; lakini sekta hii ya misitu nayo naamini kwa weledi ambao kama watasimama vizuri Wizara ya Maliasili wataisaidia Serikali kama Wizara ambayo ina mchango mkubwa kwenye kukusanya maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu na kuunganisha mikoa ya nchi hii kwa kiwango cha lami bado ni changamoto. Suala la Mkoa wa Singida kuunganishwa na Mkoa wa Mbeya limekuwa likizungumziwa kwa muda mrefu. Wabunge wote wa miaka mingi ya nyuma, hata mwaka juzi mimi nilisimama na ilani hapa kuonesha, mwaka jana wakaonesha nia ya kutaka kujenga Barabara ya Mkiwa hadi Rungwa, kilomita angalau 56.9, ikawekwa kwenye bajeti ikatangazwa kazi mkandarasi akapatikana na

Mheshimiwa Rais akaja pale akazungumza na wananchi akaonesha dhamira yake ya kujenga barabara lakini mchakato ule ukafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi tunavyozungumza tumeona tu katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2018/ 2019 barabara hii imeonesha ukurasa wa 49 kilomita 56.9, lakini mpaka hivi wananchi wale wa jimbo ambalo mimi ni mwakilishi wao hawajui barabara hii itaanza kujengwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Serikali ioneshe dhamira ya kweli ya kuunganisha mikoa kwa njia ya lami, ndiyo itakayofanya wananchi wakimbie. Walipa kodi wa maeneo ya pembezoni watalipa kodi kwa sababu watakuwa wanafanya biashara zenye tija kwa kufuata biashara maeneo makubwa. Leo mji wa Dodoma ndio Makao Makuu ya nchi Dodoma imetangazwa kuwa jiji mikoa ya jirani kama mikoa na majimbo ambayo mimi natoka yatakuwa na manufaa sana kama yataunganishwa kwa kiwango cha lami na mikoa jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia niiombe Serikali iendelee kutia mkazo barabara hii ya kutoka Handeni, Kiberashi, Kijungu, Kibaya, Njoro, Olboroti, Mrijo Chini, Dalai Bicha, Chambalo, Chemba kwa Mtoro hadi Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuchumi barabara hii ina manufaa makubwa sana, ni njia ya mkato kabisa ya watu watakaokwenda Bandari ya Tanga; na tuna matarajio yetu kwamba tunajenga bomba la mafuta kutoka Hoima hadi Chongoleani Tanga. Kwa maana hiyo barabara hii kama itajengwa kwa kiwango cha lami itasaidia sana hata nchi jirani ya Rwanda, Uganda, Burundi kama watatumia Bandari ya Tanga kuondoa msongamano katika bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafsi na pia naomba niunge mkono hoja hii ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Kafumu atafuatiwa na Mheshimiwa Shabiby.

**MHE. DKT. PETER D. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pia nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama kuchangia kidogo hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema mambo matatu, lakini kabla sijasema naomba nimshauri kaka yangu Isdori kwamba msalaba aliopewa amepewa na Yesu mwenyewe, kwa hiyo amtegemee Yesu; yeye alisema njooni kwangu ninyi nyote mnaosumbuka na mizigo nami nitawapumzisha, lakini Yesu mwenyewe alipata msalaba mkubwa na alipokwenda Gethsemane alimwomba Mungu akasema nipishie huu msalaba lakini kwa mapenzi yako; na wewe umepewa msalaba huo na Yesu kwa kupitia kwa Mheshimiwa Rais, hebu asinung'unike, afanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichangie kwa kusema, bajeti ya Mheshimiwa Waziri imeonesha matumaini kidogo safari hii. Kwa sababu ameanza kusikiliza ushauri wa Bunge. Tangu Awamu ya Tano imeanza Bunge limekuwa likishauri mambo mengi; nitatoa mifano miwili tu kuonesha jambo jinsi ambavyo bajeti hii imefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ambao Bunge limekuwa likisema ni kuwasaidia wawekezaji waweze kujisikia wako nyumbani, kuweka mazingira bora ya uwekezaji; na nashukuru ukisoma kwenye kitabu chake utaona wameunda mpaka *blue print* maana yake wamewasilikiliza na wanazungumza nao kila baada ya miezi kadhaa. Kwa kweli tunaomba hii *blue print* basi mtuletee tuisoma na muitekeleze ili mazingira ya uwekezaji katika nchi yetu yaweze kuboreka na kweli uwekezaji uje katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni mfano ni kuhusu kodi. Mara nyingi tumekuwa tukisema

kwamba kodi na tozo zitazamwe na hasa kenye kilimo. Nimeona kuna baadhi ya kurasa hapa, kwa mfano ukurasa wa 46 amepunguza *corporate tax* kutoka 30 mpaka 20 kwenye mazao ya ngozi, jambo hili litachochea sana ukuaji wa sekta ya ngozi. Naomba basi Mheshimiwa Waziri pamoja na hilo basi apeleke na kwenye mazao mengine ya kilimo, uvuvi na ufugaji ili tuchochee shughuli za uanzishwaji wa viwanda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilitekelezwa mwaka jana ilikuwa ni *VAT* ilyokuwa imewekwa kwenye huduma za mizigo inayopita. Nakumbuka mimi nilipokuwa Mwenyekiti wa Kamati tulilisema na Serikali ikalisikia. Kwa kweli bajeti hii ya leo inaleta matumaini makubwa sana. Ipo mifano mingi sana ambayo ningeweza kusema lakini itoshe tu kuonesha kwamba bajeti inaleta mwelekeo wa kukuza viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe ushauri, kwamba pamoja na mwelekeo huo bado kuna mambo makubwa ambayo Wabunge wengi wameyasenma na mimi nataka niseme mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ili tuweze kujenga uchumi wa viwanda ni lazima bajeti ya kilimo, Waheshimiwa Wabunge wamesema, iongezwe. Kwenye ukurasa wa 80 amesema ni kipaumbele cha Serikali lakini bajeti ni ndogo asilimia sijui ngapi. Tafadhali Mheshimiwa Waziri hebu ajaribu kuongeza hiyo bajeti, bajeti ijayo kilimo tusikie kwamba kweli tumepewa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kujenga uchumi wa viwanda pia linahusiana na ile miradi ya kielelezo waliyoiweka; mmoja ukiwa ni mradi wa Makaa ya Mawe na mradi wa Chuma Liganga. Chuma tukiweza kukipata ni dhahiri kabisa tutaweza kuendeleza miradi mingi, hata mradi wa *Stiegler's Gorge,* mradi wa kujenga Reli, tutatumia chuma chetu, tutapunguza gharama kweli. Sasa tunauacha tu huu mradi unaendelea, kila siku, kila mwaka tunausema; na kwenye bajeti yako hapa hauoneshi. Kwenye bajeti ya

Mheshimiwa Mwijage haukupewa kipaumbele cha kutosha. Najua matatizo yake ni vivutio vya kodi, hebu wamalize hilo jambo; kuna matatizo ya fidia ya wananchi wamalize hilo, lakini pia *PPA* kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kusema kwa kifupi ni kuhusu *ETS. ETS* ni mfumo mzuri, kwa maana ya kuhesabu uzalishaji na hakuna mtu anae pinga humu kwamba huu mfumo ni mzuri kwa sababu tutaweza kupata kodi halisia. Hata hivyo, changamoto zilizopo zilizoelezwa na wadau ni lazima Serikali wazisikilize, wanapotekeleza wasikilize gharama ya uwekezaji kwenye mradi huo. Pia waangalie namna ambavyo wataweza kufanya kiasi kwamba wawekezaji hawa waweze kuwa na gharama ndogo ili wananchi wasiweze kupata kodi kubwa kwenye vinywaji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kutoka mwisho ni Akaunti Jumuifu *(TSA)*, ni jambo zuri kwa maana ya kuweza ku-*control liquidity* ya fedha katika nchi. Hata hivyo, kuna changamoto kubwa, kwa sababu ukitekeleza utalazimika ukaangalie na sheria nyingine, unaweza ukaangalia hata Katiba ya nchi yetu tunatawalaje, kwa sababu hii inaonesha kwamba inaweza kwenda kuua Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa kwenye Kamati ya Bajeti kule niliwaambia nchi ya Marekani ina *states* 50 na kila *state* ina Bunge na ina bajeti na wimbo wake wa Taifa. Sasa zile fedha kweli zinapelekwa kwenye Mfuko Mkuu ili zirudishwe kwenye *states*? Nikasema inawezekana kabisa *reporting information* ya matumizi lakini si hela ziende na kurudi. Kwa hiyo tunapotekeleza ni lazima tufikirie kurekebisha na sheria nyingine. Kwa hiyo ni jambo kubwa ambalo linahitaji Serikali watazame vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni hili ambalo wenzangu wamesema; mimi nimetoka kwenye sekta ya madini; jambo la dhahabu. Dhahabu ni fedha na ukiangalia sheria ya BOT inasema inatunza fedha za kigeni

lakini inatunza dhahabu safi. Niliwahi kusema nchi zote tajiri zina tani nyingi kweli za dhahabu kwenye *central Banks* zake, kwa mfano Marekani inatani zaidi ya elfu nane imetunza kwenye *Central Bank*. Uchina elfu moja mia saba, Ujerumani elfu tatu mia tano, Italy elfu mbili mia tano, Ufaransa elfu mbili mia nne; zote hizi zinaipa nchi ile nguvu ya kuwa tajiri. Sisi tuna dhahabu kwa nini tusitunze dhahabu?...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. DALALI P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Kafumu. Mheshimiwa Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Leo nitachangia kiasi tu. Kwanza nianze na ile shangwe ya akinamama kwa kuondolewa kodi ya taulo za kike. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutoa kodi hii, lakini bado tuna wasiwasi na sio wasiwasi kwamba bei itakuwa ipo pale pale. Kwa sababu ametoa kodi kwa nia nzuri, lakini cha msingi lazima aangalie aweke na bei, kwamba itauzwa bei gani? kwa sababu ukitoa kodi yule mwenye duka hawezi akajua hiyo kwamba imetolewa kodi wala haitofahamika na hivyo yeye atauza bei ile ile; kwa hiyo manufaa kwa wananchi hayatakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba aangalie namna ya kurekebisha, kwamba waweke na kiwango cha bei, kwamba hii itauzwa kiasi fulani ili wale wenye maduka wasiweze kujipatia faida hii ya ushuru ambao umetolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwenye Viwanda, kwa kweli ameonesha

nia nzuri sana ya kuweza kunyanyua viwanda vya nchi hii; na wale watu ambao kweli wana nia ya kuanzisha viwanda huu ndio wakati wao. Nasema hivi kwa sababu bajeti hii imeonesha kabisa na ipo wazi kabisa, kwamba kama unaweza kuanzisha viwanda anzisha na Serikali inakuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano kwenye mafuta, ameongeza ushuru kwenye *crude oil* na viwanda vya Tanzania vya ndani ya nchi kama mawese ametoa ushuru. Ila tunamshauri, hata kwenye mashudu nayo hajayaekezea vizuri, nayo atoe ushuru wake ule wa ongezeko la thamani *(VAT).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu nataka niwaambie wafanyabiashara, wakati huu wa Serikali ya Awamu ya Tano ndio wakati wa kufanya biashara. Kwa sababu bado watu wanadanganyana danganyana hali mbaya, *TRA* inafilisi, sijui nini, huku na benki nazo ndio zimeshusha *Interest.* Sasa huu ndio wakati wa kukopa, hela zimejaa, wakati watu wanaogopa sasa ndio wakati watu kukopa na kufanya biashara, ukichelewa hapa ndio biashara imekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa cha msingi tu, nataka nitoe ushauri na nataka niseme ukweli; kwamba hapa inaonekana kabisa Mawaziri wetu wanafanya kazi lakini ushirikiano haupo, ni *zero*. Kwa sababu unataka kuanzisha viwanda vya mafuta lakini ushirikiano wa Waziri wa Viwanda na Waziri wa Kilimo uko wapi? Maana unapiga kelele uanzishe kiwanda cha mafuta ya alizeti wakati kwa wakulima hamna lolote wala hakuna *support* ya aina yoyote ili wazalishe alizeti kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaanzisha kiwanda, kwa mfano kama hapa Dodoma ukiweka kiwanda inatakiwa kiwe kimoja tu na hata hivyo hakitoshi kwa sababu alizeti yote hii ya Dodoma inakwenda Singida. Kwa hiyo hata ukianzisha kiwanda kingine hawatoweza kupata alizeti za kutosha. Mbegu ya alizeti inayotumika Tanzania inatoa *22*

*percent* ya mafuta wakati South Africa kuna mbegu inatoa *60 percent.* Nataka kusema hapa Mawaziri hapa maneno mengi, ushirikiano hakuna, vitendo hakuna; huu ndio ukweli na lazima tuambiane ukweli; tusipoambiana ukweli hapa, tukianza kuogopana, tutasalimiana, tutakunywa chai lakini ukweli ndio huo; wengine ndio maana sasa wanafikia hamna sifa wanaenda kupima samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafanya tu, ukiangalia ile video inakuangalia hamna kitu. Nataka nimtafute Mheshimiwa Rais kwa wakati wangu, ntamwambia mzee hawakusaidii hawa pangua tena, si dhambi kupangua pangua Mawaziri mara nne, mara tano. Waangalie, maana Mawaziri ukiangalia kwenye nchi hii wanaofanya kazi kwa moyo kabisa hawazidi watano. Wengine nao wamekuwa walalamikaji kama sisi Wabunge, tukikutana humu, aaa' nchi hii', mimi naogopa', yaani hawahawa ndio wanaichafua, halafu mnapiga kelele; hawa ndio wanaomchafua Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bora hata upate adui mpinzani wa chama kuliko mpinzani wa ndani ya Serikali, mbaya zaidi kwa sababu humjui. Kwa hiyo, naomba Wizara hii, Mheshimiwa Dkt. Mpango ana shida sana, ana shida sana kutokana na Mawaziri wengine kutokupa *support,* huo ndio ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nilisikia kina tajwatajwa hapa, mimi nafanya biashara, kwa hiyo nitakiongelea kila siku kama nitaona kinaenda tofauti. Kuna Mbunge mmoja hapa nilikaa naye hataki yeye *TIPER* itumike, anataka mafuta yakija yaingie moja kwa moja kwenye madepo ya kampuni binafsi, hicho kitu hakiwezekani. *TIPER* imejengwa tangu enzi ya Mwalimu Nyerere kwa ajili ya kudhibiti kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mfumo unaotumika sasa hivi ndio mfumo sahihi, wakati ule hizi kampuni nyingi hazikuwepo. Ili Serikali ijue mapato yake lazima mafuta yote yaende sehemu moja, yakitoka kwenye

meli moja kwa moja yaende *TIPER*. Wakati huo ndivyo ilivyokuwa, hizi kampuni nyingine zote; *Oryx, Gapco*, zote hazikuwepo hizi. *Puma* zilikuwa hazipo, *Oilcom*, nani, hawakuwepo hawa. Kwa hiyo wakati ule yakienda *TIPER* ndio yanaenda *Esso,Agip* na *Shell*. Sasa hivi anakuja mtu anasema hiyo italeta *leakage,* sijui na nini. Yakifika pale *TIPER,* wewe kama una lita milioni tano utasubiri Milioni tano zako utapata zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie kwa nini wanafanya hivi? Wanafanya hivi kwa sababu kampuni chache hizi zinapanga hata bei, kwamba hawa sasa tuwagonge hivi. Sasa hivi vikampuni vya Watanzania vidogo vidogo hivi ndivyo vinavyoshusha, vinasababisha na wao washuke. Kwa hiyo nia yao ni kuuza kampuni ndogo ndogo ili wabaki wao; na kila mtu akiweka mafuta kwao wanachukua karibu kwa *metric tons* wanachukua dola ishirini. Kwa hiyo wanajua yakienda kule wao watakosa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Dah! haya bwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini nilikuwa sijamaliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dkt. Kiluswa**.**

**MHE. DKT. STEPHEN L. KILUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuchangia katika hii hoja ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa jinsi ambavyo inaendesha mambo yake katika kupeleka uchumi wa nchi hii mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nasoma hiki kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa nimeona kwamba nchi yetu kweli inaelekea kuzuri maana hakuna jua halijageuzwa katika kupeleka maisha ya Watanzania mbele. Sekta za elimu, madini, maji, barabara, usafiri wa anga, *you name them,* ziko nyingi; kwa hiyo napenda pongezi zangu za dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi pia naomba niipongeze Wizara. Mheshimiwa Waziri jina lake ni Dkt. Mpango na jina linaumba na mipango yake ni safi. Nimesoma hotuba yake imepangiliwa kweli kweli, ushauri wangu ni kwamba haya yaliyoandikwa humu tujipange basi sawasawa katika kuyatekeleza.

Mheshmiwa Mwenyekiti, pia naomba niipongeze Kamati, Kamati ya Bunge imefanya kazi nzuri na mahiri kabisa katika kuandika kitabu chake hiki, na yale mapendekezo yaliyopo nayaunga mkono na naomba yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo basi naomba nijielekeze katika baadhi ya mambo ambayo na mimi nimeya-*note* katika hotuba hii na ningeweza kutoa mapendekezo au ushauri wangu. Kwanza naomba pia kuungana na wenzangu ambao wamesifia marekebisho na mapendekezo ya kufutwa kwa kodi mbalimbali, ikiwemo ile ya taulo za kike kwa sababu tunaelewa itawasaidiaje watoto wetu wanaosoma shuleni na wale ambao itawasaidia katika kuzipata kwa bei ambayo naamini itakuwa na punguzo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kuondolewa kwa kodi ya virutubisho kwenye vyakula vya mifugo, isipokuwa nasikitika kwamba hii haitagusa wafugaji wa asili. Sasa huo msamaha usije ukachukuliwa kwamba wafugaji wana kitu kikubwa cha kushangilia hasa wale ambao hawafugi kisasa. Najua dhamira ilikuwa ni kuhamasiha ufugaji bora na wa kisasa, lakini naomba niishauri Serikali kwamba nchi hii kwa asilimia 99.9 bado inategemea mazao ya mifugo ya asili. Nyama inayoliwa ni asilimia 99.9 ya Watanzania ni nyama ya ng’ombe, mbuzi na kondoo

wanaochungwa kiasili. Kwa hiyo bajeti hii ifikirie namna ya kuinua uchumi huo wa mifugo kwa kuiongezea tija na kuiwekea mikakati thabiti ya kuilea hiyo sekta maana bado ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa sababu wanajitahidi katika kuwawezesha wafugaji wa asili kupata mbegu bora, lakini mbegu bora itakuwa haina maana kama vitu vingine muhimu vipaumbele vya mfugaji havijazingatiwa na vipo vinne nikivitaja kimoja kimoja. Kwanza ni malisho; malisho ni ya muhimu sana na malisho yabainishwe na kutambulika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni maji, kukiwa na malisho bila maji bado kutakuwa na mgogoro mkubwa wa jamii zetu za kifugaji kulazimika kuacha hata malisho yenye majani hasa katika yale mapori yetu katika wafugaji waliopo Ngorongoro, Longido, Monduli, Simanjiro, Kiteto wakaenda kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na kuleta ile karaha kubwa ambayo tunaona kila siku wakifukuzwa na kupigwa faini kubwa kubwa ambazo zinawadidimiza katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ili kushamirisha hii sekta ya mifugo ni kuhalikisha kwamba wanapatiwa dawa za tiba na dawa za chanjo na Serikali iiweke ruzuku kama inavyoweka katika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni masoko ya uhakika ya ndani, maana sisi tunaoishi mipakani kule katika Wilaya yangu kama ile ya Longido wafugaji wale hawana sababu ya kupeleka ng'ombe Kenya, wanakwenda kwa sababu hawapati soko la uhakika la ndani; na wanapata karaha kule. Kuna watu wanaitwa *middle men*, madalali wanachukua wale ng'ombe ndio wanauza sokoni wewe unakaa unangojea, unapewa kile ambacho kitakachopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya ndani yatakapoboreshwa na sisi Watanzania tutaweza kujivunia

ufugaji wetu na wafugaji ambao ni jamii kubwa na ambayo inafuga mamilioni ya ng'ombe inayofanya Tanzania iwe nchi ya pili katika ufugaji Afrika hawatakuwa na sababu ya kupeleka ng'ombe nje na watafarijika kuona kwamba Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilipenda kuchangia ni kwenye hili suala la asilimia kumi zinazotakiwa ziende kwenye miradi ya maendeleo ya akinamama, vijana na walemavu katika mapato ya ndani ya halmashauri zetu. Nimesoma hotuba ukurasa wa 40 nikaona kwamba niishauri Serikali kwamba hiyo asilimia kumi, pamoja na kwamba si kiwango kikubwa sana lakini imesaidia na tumeshaona matokeo yake katika Wilaya zetu, zile Wilaya ambazo hazina mapato ya kutosha ya ndani Serikali iwape ruzuku. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba basi iongezwe asilimia mbili ili iwe ni asilimia kumi na mbili kwa ajili ya kundi muhimu ambalo limesahahulika, kundi la wazee. Sasa fomula itakuwa kwamba, wanawake watapewa asilimia nne, vijana watapewa asilimia nne, walemavu watapewa asilimia mbili na wazee watapewa asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hicho kipengele cha wazee ni cha muhimu sana kwa sababu wazee wetu wanaona kama wao wamenyanyapaliwa, wakati wanawake wamebainishwa tofauti na vijana; na najua katika kundi la vijana kuna vijana wa kike na wa kiume. Katika kundi la wazee inaonekana hatujasema wanawake na wazee, tumesema wanawake tu, kwa maana hiyo wazee wamenyanyapaliwa katika hili, kwa hiyo naomba Serikali izingatie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni eneo la hii sekta ya utalii. Sekta hii ya utalii ni moja ya sekta muhimu na ni mhimili wa uchumi wa nchi yetu, ukichukulia kwamba ziko tatu za msingi, kilimo chenye mazao na mifugo na uvuvi ndani yake, utalii na

madini; hiyo ndiyo mihimili ya uchumi wetu. Sasa katika hili eneo la utalii ambalo linachangia asilimia 17.7 ya Pato la Taifa na asilimia ishirini na tano ya fedha za kigeni zinaingia katika nchi hii sijaona kwenye bajeti kama wameainishiwa vizuri mikakati iliyowekwa katika kuendelea kuitunza na kuiendeleza zaidi ya kutoa ahueni fulani kwa magari ya kitalii, sijaona mambo mengine ya msingi ambayo nilitegemea kwamba yangeongezwa ili sekta hii iendelee kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, ili hii sekta iendelee kuimarika na kuboreka, suala la miundombinu ndani ya *parks (National Parks)* zetu lipewe kipaumbele. Suala la kutangaza utalii ndani na nje lipewe kipaumbele, suala la kutanganza utalii wa fukwe zetu na liendelezwa lipewe kipaumbele, mambo ya kale, uwindaji, utalii wa kitamaduni, utalii wa usiku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**DKT. STEPHEN L. KILUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie pia kwa kusema una kero za kodi mbalimbali ambazo wawekezaji wa utalii wanalalamika...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, utachangia kwa maandishi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa leo ndio tumefika hapo, nafahamu upande wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kuna majina nimempelekea *Chief Whip* wao na huku kulikuwa na mmoja amesafiri, lakini tumejitahidi.

Waheshimiwa Wabunge nawakumbushia tangazo la Katibu wa Bunge kuhusiana na *fund raising* ambayo itaanza muda si mrefu kuanzia sasa hivi. Tunatakiwa tutekeleze wajibu wetu wa kufika pale si kukaa tu lakini kuchangia kwa kadri

utakavyowezekana, lakini pia tuone na mambo mengine baada ya kazi nzito ya wiki nzima. Leo mtafurahi sana pale, kwa hiyo nawaombeni sana tuwe pale.

Waheshimiwa Wabunge baada ya tangazo hilo naahirisha Bunge hadi siku ya Jumatatu tarehe 25 Juni, saa tatu asubuhi. Waheshimiwa tukumbushane ninapowaaga na nyie mnanijibu.

*(Saa 12. 00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 25 Juni, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*